

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**Verbatim Report Of**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, NDIA CONSTITUENCY,  
HELD AT KIBIRIGWI P.C.E.A CHURCH**

ON

17<sup>TH</sup> OCTOBER 2002

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, NDIA CONSTITUENCY, HELD AT KIBIRIGWI  
P.C.E.A CHURCH ON 17<sup>TH</sup> OCTOBER 2002

Secretariat Staff in Attendance

- |                      |   |                         |
|----------------------|---|-------------------------|
| 1. Eunice Gichangi   | – | Programme Officer       |
| 2. George Wachira    | – | Asst. Programme Officer |
| 3. Josephine Ndun'gu | – | Verbatim Recorder       |
| 4. Mercy Njoka       | – | District Co-ordinator   |

Meeting was called to order at 10:40 a.m.

**Mercy Njoka:** Tunataka kuanza mkutano wa siku ya leo. Kwa wale ambao hawanijui, majina yangu ni Mercy Wanjiku Njoka na ni mimi District Co-ordinator wa mambo haya ya marekebisho ya katiba. Nitamuuliza Reverend Maringa atufungulie kwa maombi ili tuweze kuendelea.

**Rev. Maringa:** Hebu tuweze kusimama tuombe.

*(Prayers)* Mungu Baba tunasema ni asante asubuhi ya leo, tarehe kumi na saba mwezi huu wa kumi, ya kwamba umetukutanisha mahali hapa tena ili tuweze kuangalia mambo yale ambayo tuliweza kuzungumza juu ya Katiba wakati huu tunapofikiria juu ya marekebisho ya katiba.

Baba tunajipeana kwako asubuhi hii ya kwamba ukatawale fikara zetu na nia zetu, ili ya kwamba tunapongea, tukaweze kuongea mambo yaliyo sawa. Tunajua kuna mambo mengi yanapinga, ya kwamba tusiweze kupata Katiba mpya, na tunaomba ya kwamba vizuizi vyote ukaweze kutuondolea na ukatusaidia ya kwamba mambo yale tumeyaongea kama watu wanaojua taifa lao na wanaopenda kuwa na taifa lililo na mwelekeo. Ya kwamba Mungu wa Rehema, ukayafanye yote yaweze kuzuiwa nawe na ukasaidia kwamba maoni ya watu wako yakaweze kutekelezwa na kufanyika kuwa Katiba la kuitawala taifa yetu.

Tunaomba ya kwamba wakati huu tunapongea tuongee tukiwa tumelindwa nawe. Na tunaomba baada ya kwamba tutaweza kufikia wakati tutakapopata Katiba hata wakati imetekelezwa katika parliament. Tunaomba ya kwamba hata wakati huu parliament yetu isivunjwe kwa wakati huu kabla kufikia kikomo ya kwamba Katiba yetu imekuwa ni rahisi kutumiwa.

Tunaomba ya kwamba utusaidia, hata tunapowasikiza wakiongea kule parliament ya kwamba itafikia wakati waseme kweli Katiba hii ndiyo ya kutumiwa hata wakati wa uchaguzi. Tunajipeana kwako siku hii ya kwamba tuongee tukilindwa nawe. Maana tumeomba katika jina la Yesu Kristo, Mwokozi wetu, Amina.

**Mercy Njoka:** Asante sana Reverend Maringa kwa kutuongoza kwa maombi. Sasa tunataka kuanza kupindi chetu cha kwanza ambapo tutapata wageni wetu wakituendeleza. Kabla ya kuanza nitawauliza Committee members ambao wamefika ambao tumekuwa tukifanya nao kazi, waweze kusimama mahali walipo ili wageni wetu waweze kuwaona halafu tutaendelea. Asanteni sana, hao wengine wako pale nje.

Nitawajulisha wageni wetu wa siku ya leo ambao watakuwa wakitufunza, wakituelimisha mambo ya Katiba, the draft Constitution ambazo wengi wenu mko nazo. Tuko na verbatim recorder anaitwa Josephine Ndun'gu, halafu tuko na Assistant Programme Officer ambaye atatuongoza kwa kipindi cha kwanza, anaitwa George Wachira anaweza kuwasalimu.

**George Wachira:** *Muriega?*

**Response from the audience:** *Turiega.*

**Mercy Njoka:** Halafu tuko na Madam Eunice Gichangi, pia yeye ni Programme Officer na ni yeye atatuongoza kwa kile kipindi kirefu ambapo atatufunza mambo ya ndani ambayo yako kwa hiyo draft Constitution.

Kwa hivyo ningewasihhi wakati wote watasimama kutufunza, tuwe makini ili tuweze kuelewa na wakimalizia, mtakuwa na wakati wa maswali, na maoni yenu. Tunahakika mambo yote yataendelea vizuri. Kwa hivyo wakati huu nitampatia George Wachira ili aweze kutuongoza kwa kipindi cha kwanza. George karibu. Asante.

**George Wachira:** Habari zenu tena. Kama vile mmeambiwa mimi ninaitwa George Wachira na tunasaidiana na Eunice kuwaelimisha. Yeye ndiye atawaeleza kila kitu kuhusu ule mswada wa Katiba ambao tumetengeneza baada ya kuyasikiliza maoni yenu. Yale mawasilisho mliotupatia zile siku mbili tulipokuwa hapa, tuliyasikiliza, tukasikiza vile mlikuwa mnataka, tukazunguka kila pahali nchini mwetu.

Hasa hapa tulikuja siku mbili, siku ya tarehe kumi na saba na tarehe kumi na nane mwezi wa nne mwaka huu tulikuwa hapa hapa kwa hii kanisa Kibirigwi PCEA church, na tena tukaenda Catholic church ya Kiburu. Tuliyasikiliza maoni yenu. Kama tulivyowahaidi tutarudi tena na tumefanya hivyo leo.

Tumerudi kuwaambia ni gani ama ni mambo gani ambayo tuliweka kwa ule mswada wa Katiba tuliyoandika. Ni mambo gani mliotupatia tukaweka katika huo mswada. Ili kabla katiba mpya haijapendekezwa au kabla hiyo Katiba ifanywe, ni mambo gani watu wa hapa Kibirigwi, watu wa hapa Ndia Constituency, mliyotuaambia na tukaweka kwa huo mswada. Nitayasoma kwa kifupi, kwa muktasari tu ndio tujue kama vile tulisema ni mambo gani yaliwekwa na ni mambo gani hayakuwekwa.

Yale hayakuweko na vile tuliyaweka, Eunice atawaambia ni vipi tuliyaweka na tena mtauliza maswali. Mtauliza juu ya yale mambo mmesikia tuliwaambia na pia aitha hamjatosheka ama aitha hivyo sivyo mlikuwa mnataka. Na halafu yale mngetaka tuwaambie ni vipi tuliyaweka na tuliyaweka kwa njia gani, mtupatie.

Lengo letu hapa leo sio kuwaambia ni kwa sababu gani hasa tuliweka hayo mambo. Tumekuja hapa leo kusikiliza maoni yenu pia kuhusu huo mswada. Kuna mambo mengine ambayo tuliweka katika huo mswada ambayo aitha hayawaridhishi na mngetaka pia tuendeleo kuyaangalia katika huo mswada. Ndio maana mliambiwa tarehe ishirini na nane kutakua na Constitutional Conference ambako watu wote kutoka Kenya nzima, wale delegates ambao mliowachagua kama ni Nyeri District ama Kirinyaga District hapa, wale watu tuliochagua, wabunge wetu wakienda pale kwa National Conference ni mambo gani pia sisi tungetaka waende pale wawaeleze wale watu ambao watakuwa wakijadiliana kutoka hapa Kibirigwi, Ndia Constituency ni mambo gani tena tungetaka yapelekwe.

Kwa hivyo tutachukua repoti tena, na ndio maana mimi niko hapa kuchukua repoti yenu pamoja na Josephine pale tukisaidiana pamoja na Eunice ili tuweze kujua ni mambo gani tena watu wa hapa mngetaka kujua.

Kwa hivyo kama nilivyowaambia hizo siku mbili tulikuja hapa tukayasikiliza maoni yenu, tuliandika maoni ya watu sabini na tisa,

wale waliotupatia maoni yao. Watu waliofika walikuwa ni wengi lakini watu sabini na tisa pekee ndio tuliandika maoni yao. Kuna wengine waliandika kivyao wakatuma Nairobi lakini hizo siku mbili tulipokuwa hapa tuliweza kuandika maoni ya watu sabini na tisa.

Kuna wale ambao waliwasilisha maoni yao kwa njia ya kuongea na sisi tunayaandika. Sauti zao, yaani maoni yao yalinaswa katika hiki kidude cha redio na pia kuna wale wengine ambao walipeana mawasilisho, yaani walipeana maoni yao kama yameandikwa vile nitafanya leo na tukayapeleka Nairobi na yataangaliwa tena. Kwa hivyo in terms of memoranda, tulichukua memoranda (57) hamsini na saba. Wale waliongea walikuwa ishirini na mmoja. Wanaume walikuwa sitini na tisa na wanawake kumi walipeana maoni yao na mawasilisho.

Kama wale ambao wanahizi miswada ya Katiba ambayo imeandikwa kwa kijigazeti kuna mswada tutawapatia ambao tumeandika kama hiki kitabu. Hii ni report yenyewe, bali sio draft Constitution. Draft iko katika hii gazeti lakini tutawapatia kijitabu ambacho kimeandikwa draft yenyewe ambayo ishatayarishwa na mtapewa baadaye. Lakini kwa muda huu, mtachukua hayo magazeti ambayo tumewapatia msome na muangalie kwa sasa.

Wale ambao walikuwa wakifuata kile kitabu chekundu, kile ambacho watu wa civic education waliwapatia ni utaratibu ambao wangufuata kuyajibu maswali. Katika hiyo draft mtaona vitu kama preamble, supremacy ya Constitution na nitaufuata huo utaratibu kuwaeleza yale mambo ambayo nyinyi watu wa hapa Kibirigwi mlituambia, na ni mambo gani tena tuliandika katika hiyo draft Constitution.

Mlikuwa mmetuuliza katika preamble, that we should express the sovereignty of all Kenyans. Ie iwe Wakenya sisi wenyewe katika draft Constitution iwe inasema kuwa sisi ndio watu wenye umuhimu zaidi, sisi ndio wenye nchi hii na hakuna mtu yeyote anaweza kuja kutoka nje na kusema kuna mtu mkubwa ama kuna mtu ambaye ana uwezo mkubwa kutuliko sisi Wakenya ambao tumeitengeneza hii Constitution. Ndio maana tukasema hii Constitution, hii draft Constitution, ni yenu nyinyi wenyewe ndio maana tuliwauliza maswali na ni nyinyi wenyewe ndio mmeandika hii Constitution, sisi ni ku-facilitate tu pekee yake.

Kwa hivyo, kwa preamble mliuliza the Constitution should recognize the sovereignty of all Kenyans. Ndio nyinyi watu wa hapa Kibirigwi mkatuuliza tuandike kwa ile draft na tukaandika vivyo hivyo. Mliuliza kuhusu katiba, kama ile ambayo iliyoko sasa, ilikuwa inabadilishwa tu na wabunge. Nyinyi watu wa Kibirigwi mkatuuliza, hiyo Katiba mkishaiandika isiwe tu ni wabunge tu wanaenda pale kwa bunge na wanaibadilisha vile wanavyotaka. Wakitaka mambo fulani wanaibadilisha hao wenyewe.

Mkatuuliza kwa hii draft mpya hii tuandike kuwa tutakuwa tunarudi kwenu nyinyi, tunawauliza je huu mpangilio fulani, tuabadilisha au la? Pia mliuliza in terms of English, that there should be a public referendum to change the Constitution or to amend the Constitution. Hiyo tumeweka katika hii Katiba mpya.

Tukasema kuna vipangilio fulani kama Bill of Rights, kuna vipangilio fulani kama devolution of powers. Mmesikia sasa Serikali itakuwa yenu nyinyi katika wilaya. Serikali itakuwa yenu nyinyi kama watu wa kijiji, watu wa Location na watu wa district. That is what we are calling devolution of powers. Kwa hivyo kama devolution of powers, kama Bill of Rights, nyinyi wenyewe, hakuna mtu anaweza kuibadilisha hii Katiba bila yetu sisi kurudi kwenu nyinyi na kuwauliza kama mngetaka hivyo vipangilio vibadilishwe. The new draft of the Constitution therefore will hold a public referendum ku-change kama hizo mbili ambazo nimewaambia. Kuna zingine Eunice atawaambia pia.

Mlikuwa mmeuliza kwa citizenship vile mtu anaweza kuwa Mkenya. Kama inawezekana wale watu ambao wamezaliza hapa nchini mwetu, hao ndio watakuwa Wanakenya. Nyinyi watu wa kibirigwi mkatuuliza na tukaandika vivyo hivyo kwa Constitution. Mkatuuliza pia kuna wale watu ambao ni wetu sisi, aitha wameenda Ulaya ama wameolewa Ulaya ama vijana wetu ama wazee wetu ambao wameoa watu wa Ulaya na wako hapa Kenya yetu. Na wakioa, hao watu wameoa ama hao watu wameenda nje, tuwanyanganye kuwa Wakenya? Mkatuuliza watu wa Kibirigwi hapa, tuweke kwa Constitution kusema hao watu pia wakuwe na citizenship ya kule wameenda kama ni America na kama umeoa msichana ambaye ni wa nchi nyingine na amekuja hapa Kenya yetu akue pia na citizenship.

So you had asked that the new Constitution should recognize dual-citizenship. Hiyo haiko katika hii Constitution ambayo tunatumia sasa. Ilikuwa kama umeenda Ulaya, citizenship yako ya Kenya inaisha. Kwa hivyo ukirudi Kenya wewe ni kama mtalii na pengine ulizaliwa hapa kwetu. Kwa hivyo we recognize that there should be dual-citizenship kwa hii new Constitution. Watu wa Kibirigwi mlituuliza hivyo na tukaweka kwa hii Katiba mpya.

Mlituuliza na wale watu ambao hawana watoto, wakanunua, sisi husema hununua. In good English tunasema adoption. You adopt children from outside the country. Hao nao tukiwa-adopt wakuje Kenya na mimi ni Mkenya, huyo mtoto ni Mkenya sasa? Mkatuuliza nyinyi watu hapa tuweke kwa Constitution hii mpya ati hao watoto tukiwachukua aitha mimi sina mtoto ama ningependa mtoto mwingine kutoka ngambo na nimemleta sasa ni mtoto wangu, awe pia ni Mkenya. Tukaweka hiyo pia ndani ya hii draft Constitution.

Defence and National Security; yale mambo ya jeshi yetu, mambo ya security ya watu wa nchi yetu. Mlikuwa mmetuuliza, unajua kitambo kabla ya hii draft Constitution, president mwenyewe ange-issue a decree of emergency. Angeamuru aitha hapa Kibirigwi ama hapa Ndia kuna state of emergency, peke yake akiwa pale Nairobi. Sasa kwa Constitution mpya mkatuuliza, iweke kipangilio ama kipengele ambacho kitasema kama president ameona kuna emergency pahali, si yeye pekee yake anasema hivyo, anauliza parliament pia na Defence Council ama National Security Council ambayo tumeweka kwa hii kipangilio mpya ya Constitution ya kusema lazima kwanza awaulize, apate mawaidha pia kabla ya ku-issue state of emergency. Nyinyi watu wa hapa mkatuuliza na tukaweka kwa hii draft Constitution.

Mlikuwa mmeuliza, polisi wako corrupt sana; Constitution mpya inaweza kufanya nini? Corruption kwa hii draft Constitution

tumeweka mambo mengi. Kuna Ethics and Integrity Commission, kuna vile wale watu wanahonga, wanachukua hongo, ni vipi Constitution mpya inaweza kuwaangalia? Kama police force tukafanya police force iwe na recognition kwa Constitution mpya.

Tukafanya police force iwe na independence sana, sio ati rais mwenyewe ndiye husema na anam-appoint Commissioner wa polisi na kusema vile polisi watafanya. Hiyo District Council mmeambiwa vile hizo government za wilaya, za raia kama vile za district ziwe ndio zina employ polisi wao wa district na district yenyewe ndio inawaangalia. Tena kuwe na a constitutional office ya Commissioner of police. Mkatuuliza nyinyi wenyewe tukaweka kwa huu mpangilio mpya wa Constitution.

Mkatuuliza kuwe na community policing nyinyi wenyewe na ndio tukaweka kwa huo mpangilio mpya. Ati kutakuwa na District Police Officers wale ambao ni sisi wenyewe tunajua wanawezaje kujua usalama wa wananchi uko vipi, na ndivyo tukaweka kwa hii Katiba mpya.

Political parties, vyama vya kisiasa, mlikuwa mmetuuliza vyama vya kisiasa visikuwe tu vile wakati wa campaign, election time ndio wanakuja sasa tupate kuwajua. Mlikuwa mmeuliza kuwe na formulation ya formation management na conduct, vile zitakuwa zikiendeleza biashara zao. Mkauliza tuweke hiyo kwa hii draft ama katiba mpya. Watu wa Kibirigwi mkatuuliza vile na tukaweka kwa new draft.

Mlikuwa mmetuuliza pia, saa zingine kile kinafanya vyama vya kisiasa visikuwe na uwezo wa kuendeleza shughuli zao ni kuwa hawana pesa. Wana-depend kwa serikali, au kwetu sisi ambao hatuna pesa. Sisi pengine kama wakulima hakuna pesa ya kahawa, hakuna pesa za majani chai, ni vipi tena tutaweza kuzi-manage ama kuzipatia pesa. Mkauliza nyinyi wenyewe Serikali pia iwe inawapatia pesa, vile vyama vya kisiasa ambavyo vina maadili ambayo inatufaa. Vile vyama vya kisiasa tena ambavyo tunaona vinafanya kazi, viwe vinapewa pesa na serikali. Mkatuuliza nyinyi wenyewe na tukaweka kwa hii draft Constitution.

Mlikuwa mmetuuliza tena kuhusu structure na systems of government. Serikali mpya iwe na rais, Prime Minister na deputy Prime Ministers, nyinyi wenyewe watu wa Kibirigwi mkatuuliza hapa. Hiyo draft ya Constitution mkiaangalia wale wanasoma na wale wamesikia, hiyo pia tumeweka.

Mkatuuliza tena, Vice President, asiwe tu rais anakaa pale Nairobi, anamteua yule anayetaka basi. Aitha kisiasa ama vile anataka. Sisi wenyewe wananchi tuwe kwamba sisi ndio tunamteua makamu wa rais. Kwa hivyo president sasa katika hii draft Constitution tumeulizwa nanyi wananchi tuweke iwe, wale ambao watakuwa vice president, watakuwa ni running mate. Kwa hivyo hiyo ndiyo tuliweka kwa hii draft ya the new Constitution.

Mlikuwa mmetuuliza tena, zile branches ama arms of the government; kuna Judiciary, kuna Legislature na kuna Executive. Zisiwe ni kama ni moja peke yake, bali ziwe ziko independent, kila moja iko kivyake. Independent Judiciary, independent Legislature na independent Executive. Mkatuuliza nyinyi wenyewe na tumeweka hivyo katika hii new Constitution. Kwa hivyo rais hatakuwa akikaa anawachagua judges, au ana-appoint ma-ministers vile anataka. Sasa kutakuwa na mpangilio fulani na

tumeweka kwa hii draft Constitution. Nyinyi wenyewe mkatuuliza na tukaweka.

Mlikuwa mmetuuliza tena elections za parliament na za president zisikuwe siku moja bali ziwe siku different. Kwa hivyo vile tunachaguana urais, na ma MP, viwe sio siku moja na ndio tukaweka kwa hii new Constitution. Wale watasoma tena mtaona we have staggered elections.

Mkatuuliza tena kwa bunge, the Legislature, kuwe na nyumba mbili za bunge. Kuwe na upper house na tena kuwe na lower house. Upper house tumeiweka pale ndio iwe ikiangalia hizi serikali za wilaya ambazo tumeweka, devolution of powers. Hatuwezi kuwa na devolution of powers, ikiwa hizo serikali za wilaya hazina mtu wa kuziangalia. Na ndio sasa tunasema hizo serikali za wilaya zitakuwa zikiangaliwa na upper house. Tena upper house itakuwa inaangalia vile tunawachagua wale MPs ambao wanaenda lower house.

Halafu tutakuwa na representatives wa every region, kwa sababu Wakenya wengi, nyinyi pia mkatuuliza kuwe na majimbo. Tukaangalia tukajiuliza ni majimbo wananchi wanataka ama ni urais ama ni serikali wanataka wawe pia na nguvu ya kushauri na kuangalia vile inafanya. Ndio tukaona sasa afadhali tuwaletee serikali ya wilaya, District Councils, na ndio tumewaletea.

Mkatuuliza tena kuhusu parliament, wale watu ambao wanachaguliwa na rais, ile siku anaamka anachagua, sijui amaemchagua nani hapa, sijui amamemchagua nani hapa kama MP ama kama minister ama kama head of the Civil Service au asimamie sijui university gani. Nyinyi wananchi mmetueleza hiyo hamtaki, kwamba mnataka wale watu ambao wanachaguliwa wachaguliwe kufuatia mpangilio fulani. Aitha wamehitimu, wamefunzwa vizuri yaani they are ethically and morally right.

Parliament pia, hiyo house ya bunge iwe inawaangalia na ichunguze kama hawa watu wamechaguliwa wanafaa kweli kuwa kwa those appointments. You had therefore asked that parliament should vet all public appointments na ndio tukafanya kwa hii new Constitution.

Watu wa hapa mkauliza that the Constitution should reserve a number of seats for women, na mkauliza precisely a third. Na mkiangalia kwa hii draft report ambayo nitawarudishia msome, hivyo ndivyo tumefanya. Na Eunice atawaelezea zaidi ni vipi tumeweka hiyo.

Mlikuwa mmeuliza kwamba nyinyi wenyewe mara nyingi huwachagua wabunge, wanaenda pale bunge na wanalala, hawafanyi ile kazi ambayo waliwaahidi watafanya, sijui watatengeneza mabarabara, watajenga mashule na kadhalika. Mkauliza nyinyi wenyewe, wale wabunge tukishawaweka pale na halafu hawafanyi kazi vile tulivyo wauliza wafanya kwamba tuwe na nguvu ya kuwaita, that is recalling of non performing MPs., nyini wenyewe ndio mlituuliza, na tumeweka katika hiyo draft Constitution.

Tena mkatuuliza ma-judges wakiwa appointed lazima kuwe na vetting process ya parliament na Judicial Service Commission



ambayo iko na authority imewekwa na parliament, mkatuuliza tu nyinyi wenyewe na tukaiweka kwa hii Constitution.

Mlikuwa mmeuliza pia, nyinyi watu wa Kibirigwi, kwamba ma-MPs wawe na at least Form IV education bali sio watu ambao wamefika Class two au three ndio wanenda pale bunge kutuwakilisha. Nyinyi watu wa Ndia mkasema hapana, hiyo hatutaki. Kuwa mnataka MPs wakuwe at least wamesoma mpaka Form IV na hiyo ndio tumeweka kwa hii draft Constitution.

Mliuliza tena kwa Executive, kuwe na a code of conduct. Wale watu ambao wanachaguliwa, kuna mpangilio fulani ama kuna vile vitu ambavyo wanahitajika kuwa lazima wawe wamehitimu? Sio rais corrupt, sio mtu mwingine sijui alikuwa wapi na ni lazima awe kuwa amezaliwa Mkenya. Sio wale wa adoption sasa, sio wale watu ambao wali-acquire citizenship kupitia njia nyingine. Wale watu ambao walizaliwa Kenya, wanatabia nzuri, sisi wenyewe tumewajua, hao ndio mlisema wawe waki-appointiwa president, na ndio tulifanya kwa hiyo draft Constitution.

Mliuliza pia, nguvu za rais zimekuwa nyingi sana. Watu wa Kibirigwi hamkuwa na furaha na hiyo na mkasema hizo powers za president mngenda zipunguzwe kiasi na functions zake zile yeye hutekeleza, ziwe kwa utaratibu wa hii Katiba mpya, na ndio tumewaekea kwa hii new draft ya Constitution. Mlikuwa mmeuliza for example president asiwe chancellor wa university ati yeye ndiye anapatiana degrees. Nyinyi watu wa Kibirigwi mliuliza vile na tukaiweka kwa hiyo draft Constitution.

Tena mkauliza tukishawaweka wabunge pale halafu pengine rais hafanyi kazi vile sisi tunaona inafaa wawe na powers za kumtoa, that is impeachment of the president, kama vile America wanawafanya rais wao. Nyinyi pia watu wa Kibirigwi, mlikuwa mnataka hiyo iendelezwe hapa Kenya. The draft Constitution, hii Katiba mpya, ukiangalia vizuri tushaiweka ile.

Mlikuwa mmeuliza kuwa rais awe na vipindi viwili vya miaka mitano tu, kwa hivyo a-serve ten years maximum. Sio kwamba a-serve ten years halafu anataka miaka mingine mitano. Hiyo nyinyi wenyewe mkauliza na tukaiweka kwa draft Constitution.

Mlikuwa mmesema haya maneno ya ma-chiefs, na provincial administration, sijui P.C., D.O. nani, mlisema hamtaki. Mlikuwa mmesema hamtaki, mnataka District Council. Hao tumewatoa wote tukawapatia vile mlikuwa mnataka. Kwa hivyo ma P.C., D.O. nani, hawako tena kwa hii new draft Constitution.

Mlikuwa mmeuliza tena president asichaguliwe kama hana degree from a recognized university, sio mtu ambaye hata hatujui amesoma wapi. Hiyo pia tumeweka kwa hii draft Constitution. Tena mliuliza sisi wenyewe hawa District Council, kama hao machief wametolewa nani tena watakuwa na usukani wa kuendeleza maneno ya vijiji, maneno ya districts na divisions. Sisi wenyewe tukauliza, tuwe na power ya ku-vote. Wale watu tunawapigia kura ndio wanatusimamia. Eunice hapa atawaelezea vizuri vile tume-devolve power kutoka kwa central government, tumewaletea nyinyi wananchi. Kwa maana mnataka serikali ambayo inawaangalia, serikali ambayo inawajua kabisa. Eunice atawaambia vizuri about devolved government.

Mlikuwa mmeuliza tena that the new Constitution should specify the number of ministries. Tena tumeweka hii na tukasema

nyinyi mkiwa mmejitisha kwamba tuwe na eighteen ministries. Tukasiliza maoni kutoka kwa wananchi wengine wote, lakini hao wengine wakawashinda kidogo wakasema hao walikuwa wanataka kumi na tano. Kwa vile wengi waliwashinda tuliamua sio eighteen bali ni fifteen. So the new Constitution has stated there will only be fifteen ministries. Eunice tena atawaelezea zaidi mbona tulionelea hivyo na mbona tuliweka hivyo. Lakini pia nyinyi wenyewe mlikuwa mmetuuliza tu-specify the number of ministries.

Mkatuuliza tena the Judiciary, wale majaji ambao tena wanasema hapana hawaitaki Constitution. Wamekuwa corrupt sana, wanafanya kazi ambayo sisi wananchi wa hapa Kibirigwi, wananchi wa Ndia na wananchi wa Kenya wote hawafurahii. Tena mkauliza si hao watu wakuwe independent sio lazima president anawaambia hapana kesi hii fulani endeleza hivi vile unataka, kama huyu mtu ana pesa hapana ua huyu. Nyinyi watu wa Kibirigwi mkauliza the independence of the Judiciary na hiyo tukaweka pia.

Mkauliza tena, hao majaji wakuu ambao wanakuwa appointed na Judicial Service Commission ambayo pia ni independent na parliament pia ina powers juu yao. Kwa hivyo wabunge wetu pia watakuwa na power ya kuangalia the Law Society of Kenya, vile watu wamepatiwa the Judicial Service Commission wako vipi na wale watu wame-appoint. Ndio tukauliza majaji wote kwanza waende, wa reapply afresh tuhakikishe they are ethically right, sio watu corrupt, watu ambao wanataka na wanaonelea wananchi wako vipi. Kwa vile tunataka wananchi wawe na mwendeleo mzuri, justice and power to the people, nyinyi wenyewe mkauliza na tukaweka kwa Constitution.

Tena mkauliza, kuhusu local government, zile serikali za wilaya zilizokuwako. Mayors, na ma chairman, ma Councillors ndio walikuwa tu wanakaa pale, sijui wanachukua kitu kidogo, nini na nini, wanamchagua mayor, na chairman wa County Council hao wenyewe. Nyinyi wenyewe watu wa Kibirigwi, watu wa ndia, watu wa Kenya wote wakauliza, nyinyi mnataka muwe ni nyinyi wenyewe ndio mnawachagua wale. Hiyo ndio tukaweka kwa new Constitution. Kwa vile mliuliza, Wakenya wote waliuliza na tukawawekea hivyo tena.

Pia mliuliza hao tunaowachagua wawe na nguvu za kuwaajiri wale ambao wanafanya kazi pale. Kitambo ilikuwa kwamba serikali ya local government kutoka kwa ministry iliyoko Nairobi huko, hao ndio wanaowachagua na wanawaleta, watu hata pengine hawajui kazi na hatujui wametoka wapi. Nyinyi wenyewe mkauliza, hao watu tumewachagua ndio wanazijua shida zetu, wanajua vile tunataka kwa hivyo tunataka hao watu tumechagua ndio watakuwa waki-appoint chief officers kwa local government. Na hizo ndizo mtaambiwa hapo na Eunice zimekuwa devolved government na ndio district councils hiyo mtaambiwa. Local government, hiyo nimemaliza.

Twende kwa electoral systems na process, na ndio mkauliza na niliwaambia kitambo. Mliuliza zile kura tunazompigia rais, tunawapigia wabunge zisikuwe siku moja. Ndio at least tukishawachagua wabunge kwanza ama rais kwanza tujue ni vipi. Hiyo tena tumeiweka presidencies (inaudible). MPs, pia tumewawekea siku yao ndio maana kuna national council na

the assembly, hiyo parliament, lower house na upper house. Upper house itakuwa na miaka minne na lower house itakuwa na miaka mitano ili hakuna wakati wowote kutakuwa na vacuum, ati hakuna ma MP wakati fulani. Hiyo tuliweka tena vile tu mlivyotuliza.

Tena mkauliza kuwe na watu ambao wanaweza kujisimamia wenyewe yaani hawako kwa party fulani kwa vile pengine wanaona hao wenyewe kuna vyama ambazo hazitaki wakuwe wanachama wao na wangetaka kusimama huku kama mtu wetu wa huku Kibirigwi na hauna chama, independent candidate. Watu wa hapa Kibirigwi, watu wa Kenya wote wakatuuliza tuweke hiyo kwa Constitution. Ati nikiwa peke yangu kulingana na vile imewekwa kwa Constitution ninaweza kusimama tu bila chama na nichaguliwe kama mbunge. Hiyo tena tuliweka kwa Constitution vile tu mlivyotuliza.

Tena mkatuuliza tukisha chaguana pale kwa polling station, kule sisi huenda tunapiga kura, mara nyingi tunaona zile kura zinachukuliwa na zinaenda Kirinyaga au Kerugoya kuhesabiwa ili waamue mshindi. Mlionelea pengine wakati mwingine wakati hizo kura zinasafirishwa huenda zinaibiwa, zingine hutupwa na zingine haijulikani hupelekwa wapi. Watu wa Kibirigwi mkatuuliza na hiyo draft Constitution ambayo ni yetu, tunataka tukishaweka kura pale kwa polling station, kama inapigiwa hapa Kibirigwi kwa hii church, hizo kura zihesabiwe pale na tuambiwe ni nani ameshinda. Hiyo tuliweka kwa hii draft Constitution.

Mkauliza tena na hizi masanduku sisi hatuwezi kuona ndani, zingine ni black na zingine ziko na rangi aina aina. Mlisema mnataka zile ziko clear kama glass ili muweze kuona na kuthibitisha kama kulikuwa na chochote ndani au la, transparent ballot boxes. Watu wa Kibirigwi mkatuuliza hivyo na tukaweka kwa draft Constitution. Kwa hivyo in the coming elections, kama tutafanya na hii draft Constitution, tukisha weka kura tutakuwa tunaweza kuona na kuthibitisha nini kiko ndani ya sanduku hizo. Sio kuambiwa hapo ndani hakuna kitu lakini tunaona ziko black. Hiyo nyinyi mlituuliza na tukaweka.

Tena mkatuuliza date ya general elections iwe specified kwa Constitution. Na sinimewaambia, pia hiyo tumeiweka kwa Constitution. Sio kwamba tunakaa siku moja na mtu tu anaamua elections ni kesho. President sasa hana power ya ku-dissolve parliament vile anataka. Akifikiria kama sasa, kutumia hii Consitution ya sasa, vile tumeketi hapa saa hii, anaweza kuenda bunge na aseme bunge imevunjwa na tufanye elections na hii Constitution nzee. Lakini kwa hii Constitution mpya hawezi kufanya hivyo, hana hizo powers tena. Nyinyi watu wa Kibirigwi, pamoja na Wakenya wote mlituuliza hivyo, na tukaweka ndani yake.

Pia mkatuuliza, kuwe na code of conduct ya ku-check wale watu ambao wanafanya campaign, kwamba wasizue vita na ghasia, hivi vikundi kama Mungiki na zingine kama hizo. Hivyo vikundi vikundi vya watu ambazo hujihusisha na wanacampaigners ambao wana violence Constitution inaweza angalia aje? Elections violence pia Constitution imeangalia.

Mkatuuliza kwa basic rights, zile rights zetu sisi kama wananchi. Kuwa mngetaka elimu ya primary school. Wananchi wa huku Kibirigwi pamoja na Wakenya wengi, watoto wao wengi hawasomi. Sio kwamba hawataki masomo lakini ni kwa sababu

hawana zile pesa na tunalipa tax, kuna pesa nyingi kwa serikali isipokuwa wanatumia pesa vibaya. Tunataka serikali na mkauliza serikali kuwa kwa hii Constitution kuwe na basic rights, na masomo ya primary yawe ni ya bure. Jambo hili mkatuuliza na tukaweka.

Tena mkatuuliza kuwe na freedom of worship, human rights for all Kenyans, mkasema kuwe na basic health care, mkatuuliza kuwe na maneno ya basic food, clothing, shelter, manyumba na nini. Watu ambao wanaousoma mswada huu wa Katiba hii mpya, mkiangalia vizuri, hayo yote, basic rights, tume-expand kuliko ile iliyokuwa hapo, iko ndefu sasa. Mkiuliza maswali mkiangalia mtaona kuhusu basic rights, hii draft Constitution imewashughulikia wananchi kabisa.

Kuhusu rights za vulnerable groups, wale watu ambao hawajiwezi, watu ambao hawaoni, walemavu ambao wanatumia wheel-chairs, Constitution imewaangalia vipi? Hii draft Constitution ikaangalia vizuri, ikaangalia premises, kule watu wanatembea. Wale watu ambao hawaoni hata kusoma kwao kuwezeleshwe, vile wataendelea vizuri, Constitution imeangalia hiyo. Na hata one example, tulikuja hapa na wale watu ambao hawaoni, wasiseme yale mambo ambayo nimesema, au yale mambo nimesoma hapo nyinyi mnaweza kuja muangalie kama vile nimesoma kuwa ni hakika ama kwamba ninasoma mambo yangu. Hawa watasoma wapi na hawaoni? Niko na Braille na ndio hii hapa. Wale watu ambao hawaoni watasoma kwa mkono, pia Constitution tumewaandikia, iko hapa na tukaandika hayo maneno kuwa lazima Constitution i-recognize the rights of vulnerable groups, the disabled, wale watu wazee ambao wamezeeka kabisa, youth, young children na women wote wameshughulikiwa na Constitution.

Mkauliza tena kuhusu wale watu ambao wako jela, prisoners. Mara nyingi sio kwamba wako pale kwa kupenda kwao. Hiyo Constitution ambayo tunataka ibadilishwe haikuwa inawaangalia. Mkauliza nyinyi watu wa Kibirigwi, hao watu hata baada ya kuachiliwa siwatakuwa tu wako bado ndani ya ile serikali ambayo sisi tulichajua na hao hawakuhusika. Mliuliza Constitution iangalie rights zao na mkasema, the new Constitution iwapatie the right to vote, na ndivyo tumeandika kwa hii draft. Rights zao zingine nyingi tumeangalia kwa hivyo mkisoma mtaziona zote hapo.

Mambo ya mashamba, land na property yote, watu wa Kibirigwi mlikuwa na maneno mengi ya kusema. Mkasema mashamba, kila Mkenya kokote yuko, kama uko Kibirigwi, Nyeri au kokote kule, ukitaka kununua shamba Nakuru, Molo au kwingineko, uwe na right to access land anywhere in this country. Hiyo tuliweka kwa Constitution vile mlituuliza.

Equitable distribution of land, pia hiyo mlituuliza. Watu wengi sana pia walituuliza kuwe na land ceiling. Hiyo hatukuweka lakini ni mambo tunasikia sasa kwa vile kulikuwa na watu wachache ambao walikuwa waangalie ni vipi mambo hayo yataangaliwa, na Eunice atawaeleza mengi juu ya hayo, ni kwa nini hatukuweka land ceiling na vile tunaweza kuendelea tena kuchukua maoni tena. Kwa vile sio ati tumekuja finally, hii tu ni draft bali sio final copy. Land ceiling hatukuweka lakini Eunice atawaeleza kindani juu ya jambo hilo.

Tena mkatuuliza, watu wote, hata wanawake wawe na right ya ku-inherit property. Wawe wanagawiwa mashamba na mali pia kwa sababu pia hao ni binadamu na wengine hawaolewi na wanamahitaji fulani. Hii Constitution mpya, wanawake wa hapa Kibirigwi, hata wazee na kila mtu akauliza, kila mtu aangaliwe na hii draft Constitution na ndio tumefanya kwa hii draft.

On cultural, ethnic and regional diversity, mkatuuliza na zile mila zetu na utamaduni wetu ambazo sisi tunaona ni ya muhimu, utaangaliwa vipi na hii Constitution? Ile Constitution ambayo tunataka kubadilisha haikuangalia hayo maneno. Kwa hii mpya tuliangalia tukasema positive traditional values, Constitution ina respect na inarecognize na nyinyi wenyewe ndio mliotuliza na tukaweka pale.

Management and use of natural resources mkatuuliza kuwe na equitable distribution of natural resources. Tumezoea vile wale wamechaguliwa kuunda serikali zile pesa tunalipa tax, kama ni madini ambayo yamepatikana pahali fulani washachukua mapato yanatokana nayo, wanaendeleza sehemu fulani. Kwa vile aitha walivote serikali, nyinyi wale ambao hamkuvote serikali mabarabara zenu hazifanyi. Hii katiba mpya inasema all Kenyans own those natural resources, ziwe Mombasa, Kisumu au hata kama ni Lake Victoria au kama ni hii Lake Sagana ambayo inatoa electricity huko, sio ati watu wa Kirinyaga pekee yao ndio wanafaidika. Mkakuwa wazuri sana mkasema hata nyinyi watu wa Nairobi na sehemu zingine zote mpewe.

Lakini tena mkauliza, sisi tena kwa vile tuko karibu na hivyo vitu, mbona kwanza ziende Nairobi au Kisumu, ili hali sisi hazitunufaishi? Constitution mpya inasema local communities, wale watu ambao wanaishi karibu na hizo natural resources, wawe wa kwanza kupokea manufaa ya hivyo vitu ndio maana kuna district councils kuhakikisha hivyo. Sasa kama hiyo electricity, sisi watu wa Kirinyaga tunawapelekea watu wa Nairobi, hayo maji na stima inatoka tu hapa. District Council tutaiendeleza vipi?

Sio tax pekee yake kwa vile hatuna pesa nyingi. Lazima iwe ina charge wale watu ambao wanapelekewa stima. Districts kama Nairobi, na Muran'ga kwa vile hawana, tunastahili kuwauzia ndio tuweze ku-maintain our District Councils, kulipa mishahara, kuangalia mabarabara yetu vizuri na kadhalika. So local communities watakuwa wakipata manufaa ya vile vitu, madini, hayo maji au nini zote ambazo ziko karibu na sisi kabla ziende pengine. Kwa hii Constitution, nyinyi ndio mliuliza, watu wa Kibirigwi na Wakenya wote na tumeweka kwa hii draft.

Tena mkauliza, watu huajiriwa kwa sababu wanajuana na rais au wanajuana na ministers? Mkasema nyinyi wenyewe mnataka watu waajiriwe vile wamehitimu. Wakili aajiriwe kwa sababu amehitimu kama wakili, daktari au mwalimu aangaliwe vizuri na ihakikishwe amefuzu kwa kazi hiyo.

Pia mliuliza waalimu wafanywe vipi? Constitution mpya ikaangalia Teachers Service Commission ni ya serikali, imekuwa a branch of the government na serikali ambayo inatawala wakati fulani, aitha haipendelei mpango fulani. Tukaangalia hiyo na waalimu wengi nchini kote. Wa Kibirigwi, wa Kisumu wa Nyeri, kote kote. Walipendekeza tupate a Teachers Service

Commission ambayo iko independent na tukawapatia vivyo hivyo. Kwa hii draft Constitution tumeweka a constitutional office ya Teachers Service Commission, ambayo itakuwa independent, na itafanya kazi vile inafaa na waalimu wote watahugulikiwa kimasomo, kifedha na kadhalika. Wanahitaji Teachers Service Commission ambayo hakuna mtu anawaambia hapana, hamuongezwi mishahara. Hiyo ndio iko independent, na wale Commissioners ambao wamechaguliwa wako independent. Na tumefanya hivyo kwa hii Constitution mpya.

Mkauliza the appointment of cabinet ministers iwe ni ya watu ambao wako qualified, wanahead ministries kwa vile wako na qualifications fulani. Hiyo pia tumeangalia. Mkasema wale watu ambao wanachaguliwa, kama marais ama public officers, kabla wachukue mamlaka, wanahitaji waseme wako na utajiri wa aina gani. Nyinyi watu wa Kibirigwi mkatuuliza hivyo na tumefanya hivyo.

Kuhusu environmental na natural resources mkatuambia kama misitu, Mount Kenya hii na misitu ile iko hapa hata kama kuna Kibirigwi forest kwa mfano, zote ziangaliwe na Constitution na tumefanya hivyo.

Pia mkatuuliza kuhusu international relations, yale mambo ambayo yanahusu nchi yetu lakini zimepelekwa huko nje in terms of treaties, conventions, zile agreements ambazo zinafanywa nje ya nchi yetu na ni sisi zinatuhusu. Mkauliza Constitution mpya iangalie vizuri na tukafanya vile vile.

Constitutional commissions, institutional offices, mlikuwa mkauliza office inayoitwa ombudsman. Nyinyi watu wa Kibirigwi mlituuliza na tukaiweka. Lakini Ombudsman sio jina la Kiingereza, na sisi tulitaka nyinyi wenyewe kwa vile nyinyi ndio mliandika na mlituuliza ile Constitution tutaandika tuandike kwa lugha ambayo nyinyi pia mtafahamu na kuelewa vizuri, easy and simple language. Ni ombudsman lakini tukamwita people's protector na tukamweka pale kwa Constitution. So the people's protector is the format of an ombudsman na hiyo ndio iko kwa new Constitution.

Mkauliza tena kuwe na a permanent Constitutional Commission. Hii Commission ikiondoka, ni watu wagani wataangalia hii Constitution ambayo tumeishi miaka mingi itengenezwe? Itaendelezwa vizuri and it will be applied to the letter. Constitution ya watu watano, hii sio kubwa kwa sababu hii itakuwa ni ya just to ensure that Constitution inafuatwa inavyotakikana. Eunice atawaeleza zaidi. Kuna Constitution ya watu watano ambayo tumeweka, ambayo itaendeleza huu mswada wa Katiba na Katiba mpya ambayo tutaifanya iwe ni katiba mpya.

Tena mkatuuliza tuwe na supreme court. Kenya tuko na district courts, kama zile tunajua hapa Kerugoya kuna moja, Nyeri kuna pia High Court halafu tunaenda Court of Appeal na zinaishia hapo. Mkauliza wakati mwingine nyinyi watu wa Kibirigwi na Ndia na Kenya nzima wanapeleka kesi zao, zinafika pahali na hawaridhiki na uamuzi. Ni wapi tena wanaweza kuwasilisha malalamiko yao? Nyinyi watu wa Kibirigwi mkatuuliza hamuwezi kuweka korti ingine ambayo inanguvu? Tukawaekea Supreme Court.

Mkauliza tena succession and transfer of power. Ethics is justice and Speaker wa national assembly ule wakati wa transition. Sio ati rais ako hapa, yeye ndiye amesimama na tena anataka kuchaguliwa tena na bado amekalia kiti. Kama pengine rais ameenda na hakuna Vice President, nani tena atashikilia huu usukani? Mkauliza Chief Justice na Speaker. Lakini Kenya yote hawakukubali Chief Justice, wakauliza Speaker wa national assembly awe ndiye ameshikilia usukani. Kwa hivyo hatukuweka Chief justice vile mliuliza lakini kwa vile mmeuliza watu wawili, tuliamua kumuwekea mmoja wa wale mlikuwa mmeuliza. Speaker of the national assembly now will be the head of government during the transition period.

Nikimalizia, mliuliza haki za wanawake nazo ziko vipi? Wanawake wa hapa Kibirigwi wakauliza they are very much discriminated against. Ni vipi Constitution mpya inaweza kuwaangalia? Tukaangalia vizuri tukasema all forms of gender abuse are discriminatory practices na Constitution mpya imekataa hizo. Tukaweka kwa new Constitution. Wanawake pia tumewapatia haki ama right ya ku-inherit property pia hao wanaweza kugawiwa mali. Eunice atawaelezea vizuri mambo ya women rights.

On legal systems mlikuwa mnauliza kesi ama courts, or the legal process imekuwa very discriminatory. Wale watu wanapesa, wale watu wa kijiji ambao hawajui mambo mengi, those who are ignorant ambao hawajasoma kamwe, wanadanganywa, wanahadaiwa na wale wajuaji wa hapa. Mnataka Constitution mpya iangalie iseme all Kenyans irrespective of gender, race, and economic resources tukue equal. Na Constitution iwe ikiwaangali nyote ni sawa. Watu wa Kibirigwi mliuliza vile, watu wa Ndia wakauliza, Kirinyaga wakauliza, Muranga vile vile, Kisumu na hata Mombasa, kila Mkenya akauliza vile na ndio tukaweka kwa hii new Constitution.

Kwa muktasari, hayo ndiyo mambo mliyotuuliza na tukayaweka na yale mliyotuuliza na hatukuweka Eunice atawaelezea zaidi kwa dakika chache tena. Halafu yale mambo ambayo aitha nimesema ama wale ambao wamesoma kwa vile ni lazima kuwe mtu amesoma na hawajaelewa na wangetaka tena yafafanuliwe zaidi, Eunice yuko hapa kwa hiyo. Hii report yenu iko pages one hundred and seventeen, mia moja kumi na saba. Hii ndio report yenu.

Hiyo report ya Kenya nzima nimewaambia iko eight hundred pages. Constitution iko na reports zenyewe, zingine za Kiswahili, hivyo vitabu mkonavyo ni toleo fupi, kwa uchache au muktasari tu lakini repoti yenyewe iko page mia nane. Na mmeona nyinyi wenyewe mlitoa page mia moja, kumi na saba na hii ndiyo repoti yenu. District Co-ordinator wa hapa, Mrs Njoka atawaeleza vizuri vile mnaweza kuipata na kuna vitu vingine pia viko kwa ofisi yake ambavyo mnaweza kusoma. Asanteni sana wananchi.

*Clapping from the audience.*

**Mercy Njoka:** Asante sana George Wachira kwa hayo maelezo mazuri na nina hakika mmesikia... ninafikiri kuna watu ambao wamekuja kwangu ofisini na wameniambia kwa kweli niliona maoni yangu kwa draft Constitution. Vile mmelezewa



maoni mliyopeana, haya mambo alikuwa akiwaelezea ni yale mambo tuliyochukua huku wakati tulikuwa huku na mengine ambayo tulikuwa tumechukua kule Kiburu Catholic Church.

Kwa hivyo, hayo mambo mengine yako kwa draft na mengine pengine hayakuwekwa kwa sababu pengine hakukuwa na support ya kutosha kutoka sehemu zingine za Kenya. Kwa hivyo wakati huu nitampatia mwalimu wetu, Madam Eunice Gichangi, ili aweze kuendelea kwa hicho kipindi kingine. Karibu Madam Gichangi.

**Eunice Gichangi:** Habari yenu watu wa Ndia?

**Response from the audience:** Mzuri.

**Eunice Gichangi:** Ninafikiria mnanisikia hata wale mko nyuma, tuko pamoja. Mnanisikia ama hamnisikii? Mnaniskia, ninaona nyote mna-turn nyuma kwa hivyo mnanisikia. Leo tumefurahi kuwa nanyi, asante George Wachira. Vile George ametueleza, ametuonyesha ya kweli kwamba maoni ambayo mlitoa kama watu wa ndia yalikuwa ni maoni ambayo yalitumiwa kuiandika au kuibuni ile draft ambayo mmeshika. Copy yangu ni tofauti kidogo lakini kila mtu, au hata kama huna utaketi pahali ambapo kuna mtu ambaye yuko nayo.

Wengi watawaambia ya kwamba hiyo tume ya Ghai, hiyo Ghai Commission, ati hata hayo maoni yenu hawakuyachukua. Walienda tu kule Mombasa vile walisema, wakalala, wakaamka na wakakuja na document. Lakini vile ambavyo mmesikia George akisema, si ni kweli maoni yenu yalikuwa ya muhimu? Eeh, tena file iko hapo tutamwachia District Co-ordinator mtapata kuisoma. Tulichukua maoni yenu yote. Wengine mlikuwa hapa mkaongea, mkasimama sijui ni upande ule, mkaongea, tuka-record kwa machine ambayo Josphine anashughulikia na ndiye alikuwa hapa siku hiyo, aka-record. Na atawaambia kwamba alienda akayaandika tena kwa computer, yakawekwa ndani, ndio sasa George amekuja na hayo maoni. Na tuliyasoma na tumeyafahamu sana. Ukiniuliza nitakwambia hayo maoni hata kama nimefunga macho kwa sababu tumeyasoma na tukajua kila constituency, kila area ya Kenya, Wanakenya walisema nini.

Kwa hivyo leo ni siku yenu kama Wakenya kusikiliza vile draft ya Constitution inasema ama vile inaprovide, ndio tunasema kwa Kiingereza. Ninaamini kila mtu amekaa pahali ambapo ataweza kuangalia hiyo draft ndio uamini mwenyewe. Leo tumekuja na drafts ambazo ziko kwa lugha ya Kiingereza, lakini tayari tumetafsiri na sasa ziko pia kwa lugha ya Kiswahili.

Hatukuweza kuja nazo, ziko tayari lakini ziko chache. Zitakuwa available through your Co-ordinator Mrs Njoka ambaye anafanya kazi kubwa sana huku na ataweza kuwapatia hapo baadaye muweze kusoma. *No ona hau thutha ri, nitukageria guthondeka* summaries, ndio muweze, yule haelewi Kiingereza au Kiswahili, tutajaribu tukipata muda tupate summary za hizo lugha zingine ndio kila mtu aweze kuelewa.



Kama mlivyosikia George ametueleza, pia tuko na Braille copy ya ndugu zetu na dada zetu ambao wanatumia copies za Braille.

Kwa hivyo mtanipatia muda mchache, na nitawaelezea tu. Vile nitafanya ni kusisitiza yale ambayo ni mapya katika hiyo draft ama yale ambayo tumebadilisha kabisa. Hapo baadaye muda utakuwa ni wenu, hii ni siku yenu kuuliza maswali ama kupeana proposals. Pahali ambapo patawaridhisha ama patawafurahisha, mtatueleza. Pahali ambapo mnasikia hapo hapakuji kabisa, pia mtatueleza. Kwa hivyo siku ni yenu, na muda ni wenu kusikiza. Sitapoteza wakati, kwa hivyo wale ambao tuko na draft tutaenda pamoja. Wale ambao hamna saa hizi, mtasikiza na mtapata kujua.

Tukianza kabisa, kwanza ningependa kuanza kwa utangulizi na ninafikiria iko kurasa ya pili, page number two. Ukiangalia Katiba ambayo tuko nayo sasa, haina utangulizi. Katiba ambayo tuko nayo sasa unapoifungua inaanza tu straight kukueleza mambo yale ambayo tunataka serikali ifanye ama mambo yale ambayo wewe mwananchi unatakiwa ufanye. Lakini sasa tumesema Katiba yetu na tumeona maoni yenu mlisema tuwe na utangulizi ama preamble. Na tumesoma pia Katiba za nchi zingine wamesema wanataka utangulizi.

Ukiangalia, tunaanza na huo utangulizi na ni utangulizi mfupi. Ni kwa ufupi tu. Tumesema ya kwamba, tunaanza kwa kusema ‘we the people of Kenya...’. Yaani sisi watu wa Kenya. Tunaanza na kumtambua raia, mwananchi wa Kenya. Maoni yenu nimesikia mlisema mnataka Mkenya, raia atambulike kikatiba. Katiba tuliyonayo haimtambui Mwanakenya, haimtambui raia wa Kenya.

Sasa tunasema tunaanza kwa kusema, sisi watu wa Kenya kwa sababu sisi ndio tumeiunda hii Katiba, ni Katiba yetu. Halafu tunaendelea, laini ya kwanza tunasema, sisi Wanakenya tuko tofauti sana. Tuko na tofauti za kikabila, mimi ninaweza kuwa nimetoka sehemu za Kikuyu, mwingine ni Mluhyia, mwingine ametoka Turkana, hata dini zetu ni tofauti. Wengine ni Catholics, wengine ni PCEA, wengine Wahindi, wengine Waislamu na wengine hata hawaamini Mungu. Pia mila zetu ni tofauti na kadhalika. Tuko tofauti kama Wakenya.

Lakini tunasema kikatiba, sisi sote ni Wakenya, however different. Hata tukiwa na tofauti hizo, sisi sote bado ni Wakenya. Tena kwa huo utangulizi, tunamalizia kwa kumtambua Mungu. Na tunasema Mungu aibariki Kenya, God bless Kenya. Na huo ndio utangulizi wako. Ni utangulizi ambao sio mrefu, hakuna utangulizi ambao ni wa pagi kumi. Kwa hivyo tulijaribu kuweka mambo ambayo ni ya muhimu katika huo utangulizi.

Tukielekea kwa chapter ya kwanza, ambayo itapatikana kwa page nne, page number four. Ninataka twende pamoja ndio muamini msiseme tulikuja tukaongea na hamkuyaona. Ninataka tuamini tukiwa pamoja. Ukurasa wa nne, chapter ya kwanza, chapter 1, inaongea juu ya ile kwa Kiingereza tunasema sovereignty, na tena maoni yenu nimesikia mmeongea mambo ya sovereignty of the people.

Yaani kwa chapter ya kwanza, tunasema ya kwamba katika hii Katiba, tunatambua ya kwamba, raia wa Kenya ndiye mwenye

nguvu zote. Raia wa Kenya. Katiba tuliyonayo sasa nimesema haimtambui raia wa Kenya kama yeye ndiye mwenye nguvu. Sasa tunasema raia wa Kenya ndiye mwenye nguvu zote. Na hizo nguvu ni za kufanya nini?

Ana nguvu za kuiunda bunge. Yaani wewe raia wa Kenya ndio utakuwa na nguvu za kuiunda bunge, kuvunja bunge na kadhalika. Pia, Mwanakenya ndiye mwenye nguvu za kuiunda serikali. Kwa mfano, kusema ya kwamba kutakuwa na rais, hakutakuwa na rais na kadhalika. Ninaona wengine wanatoka, copies ambazo ziko ni chache usipopata copy yako leo, keti karibu na mtu ako na copy na hapo baadaye mtapata copy. Sidhani kuna copies za kutosha.

Hebu tuketi sasa ili tuendele. Okay, ninafikiria tuko pamoja sasa. Wale wamepata ni vizuri mmepata, yule hajapata usijali. Tulikuwa tumetengeneza draft nyingi sana lakini zote zimeisha. Inaonekana Wanakenya siku hizi wamejua haki zao zaidi. Kwa sababu zilikuwa zimejaza board room yetu, zimeisha lakini bado tunaendelea kutengeneza zingine. Na nimesema mtapata hata ile iko kwa lugha ya Kiswahili. Kama hujapata kwa wakati huu, tafadhali keti karibu na yule yuko nayo, atakusaidia.

Kwa hivyo tukiendelea, sasa tuko kwenye kurasa la nne. Kurasa la nne nimesema tunaanza kwa kuongea juu ya sovereignty of the people. Yaani kusema ya kwamba raia wa Kenya ndiye mwenye nguvu zote. Nguvu zote nchi, zimewekwa kwako wewe raia wa Kenya. Kwa hivyo hapo tumebadilisha ndio isiwe ya kwamba mtu yeyote anafikiria nguvu zote ziko kwa sehemu yoyote ya serikali kama bunge, majaji, rais ama yeyote mwingine. Nguvu zote ziko ndani yako, wewe kama Mwanakenya. Kwa hivyo tunaanza hii draft kwa kumtambua Mwanakenya na nguvu ambazo uko nazo kama Mwanakenya. Wewe ni mtu muhimu sana ukiwa raia wa Kenya.

Tukiendelea Article ya pili, ama ibara ya pili, bado katika huo ukurasa, utaona namba zimeandikwa hapo kando. Ukiangalia ya pili ambapo tunasema supremacy of the Constitution. Hii ni kusema ya kwamba, hii Katiba, hii draft ikiwa Mungu ataijalia iwe ndio sheria ya Kenya, hii draft ama hii Katiba ndio itakuwa na nguvu zote kuliko sheria zote nchini. Tunajua ya kwamba kuna sheria nyingi ambazo zinatumiwa nchini. Kuna sheria ambazo zinaundwa na bunge, kuna sheria zetu za kimila na kadhalika, lakini tunasema ya kwamba Katiba ndio itakuwa na nguvu zaidi, nguvu zote nchini. Na ukumbuke hiyo Katiba imeundwa na sisi wananchi. So hii sheria yetu ndiyo iko na nguvu zaidi nchini.

Tukiendelea, ninasema ninasisitiza tu yale ambayo ni ya muhimu. Sasa tunaendelea chapter ya pili, kurasa ni hiyo, hiyo tu ya nne. Ukiangalia hiyo ibara ya sita, article number six, tunaongea juu ya Republic of Kenya. Yaani tunaanza kwa kujiuliza na tulijiuliza sisi wanatume, nchi yetu ya Kenya ndio gani? Tukasema ya kwamba lazima tutambue ile ardhi ambayo tunaita Kenya ndio tusiseme tu tuko na Katiba ya Wanakenya na hatujui Kenya ni ardhi gani. Which mass of land constitutes Kenya.

Ndio hapo tunaanza kwa kuitambua nchi ya Kenya. Na mkiangalia hapo baadaye, mkienda na hizo draft nyumbani, mtaona kwamba huko nyuma tuliuliza utaalamu kutoka kwa ofisi ambayo inahusiana na mambo ya kigeographia. Wakatueleza Kenya inaanza kwa upande gani, mpaka wetu kule juu na Somalia, Ethiopia umefika wapi, kule kwingine umefika wapi. Na mara

nyingi tunasikia watu wa Uganda wanasema ya kwamba Uganda umekuja ikafika wapi? Hamjasikia hivyo?

**Response from the audience:** (Inaudible)

Ati imefika mpaka Naivasha, uplands, wengine wanasema uplands. Hivyo ndio tunasikia. Sasa hata ukiangalia Katiba yao hivi sasa, na nishaisoma mimi mwenyewe, ukiangalia Katiba yao ambayo wameunda hivi majuzi, ardhi ambayo wanayotambua kuwa Uganda, imeingia kidogo ndani ya Kenya. Haijafikia Naivasha lakini imepenya kidogo ndani ya Kenya. Nasi tukasema tunataka tuijulisha dunia nzima ardhi ya Kenya ambayo tunaitambua kuwa Kenya. Kwa hivyo tumeanza kwa kuitambua nchi yetu ya Kenya.

Tena katika ibara ya saba, article 7, jambo ambalo tumefanya hapo ni kutambua mipaka ambayo iko ndani ya nchi yetu. Ukiangalia hivi sasa, wakati mwingine watu huamka na tunatangaziwa kuna districts zingine mbili zimeundwa pahali fulani, mipaka imebadilishwa, constituency tunasikia ni zingine. Sasa tunasema ya kwamba, kama Wakenya, tunataka tuzitambue districts, provinces na constituencies ambazo zimetambulika kikatiba na kisheria hivi sasa.

Kwa hivyo hapo mbeleni, ama hapo baadaye mtaweza kuona ya kwamba katika hiyo draft kwenye kurasa za mwisho, tumeweka orodha ya district zote ambazo tumezitambua kuwa ni districts za Kenya ambazo ni sabini, sitini na tisa na Nairobi ndio ya sabini. Pia tumezitambua provinces zote ambazo ni nane na tukaziweka hapo. Ndio mtu akipenda kubadilisha aongeze district, province ama abadilishe mipaka, lazima arudi kwa katiba ambayo iliundwa na mwananchi kwa hivyo lazima arudi kwa mwananchi. Kwa hivyo tumezitambua hapo ndio tuzilinde kitaifa.

Tena katika ibara ya tisa, article 9, tumesema ya kwamba lugha ambazo zitatumia katika nchi yetu ni lugha mbili. Yaani mambo yote ambayo ni official, mambo yote ambayo ni public yatatumia lugha hizo mbili. Moja ni Kiingereza na lugha ile ingine ni Kiswahili. Na sisi kama wanatume tumeanza huo mtindo. Documents zetu zote kama vile Bwana Wachira aliwaonyesha repoti zetu, zimechapishwa kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Draft ya katiba, nimesema mko na ya Kiingereza, ya Kiswahili iko njiani.

Kwa hivyo mambo yote yatakayotengenezwa ambayo ni official, yawe kwa hizo lugha mbili ndio tuweze kumaliza ignorance, yaani kutojua mambo. Tulisema wakati wa kupewa Uhuru, tunataka kumaliza ujinga sindio tulisema, kutojua. Hali hiyo ya kuwa hujui mambo. Na tukasema sasa Mwanakenya yeyote apate kujua mambo kupitia hizo lugha.

Tena tumesema ya kwamba zile lugha zetu za kimama, zile lugha kama Kikuyu, kijaluo, Kisii na kadhalika, serikali itapewa jukumu ya kutusaidia kuzikuza ili tusizisahau. Ni lugha ambazo ni za muhimu, watoto wetu, wajuu wetu waweze kuzielewa. Kwa hivyo hapo tumeipatia serikali jukumu ya kutusaidia kuzikuza.

Nikiangalia ibara ya kumi, article 10, hapo tunaongea mambo ya dini. Tumesema ya kwamba hakuna dini ambayo itakuwa iko juu ya ile nyingine. Dini zote ambazo zimetambulika, na dini hutambulika aje? Dini yoyote ambayo imepewa registration na serikali, na ikatambulika kuwa ni dini, hizo dini zote zitakuwa na haki sawa. Hakuna dini ambayo itakuwa na haki zaidi kuliko ile ingine. Na mkumbuke ni zile ambazo zimetambulika kikatiba, zimepewa registration.

Ibara ya kumi na tatu, article 13, tunaongea juu ya siku ambazo hivi sasa tunaziita public holidays. Ukiangalia katiba tulionayo, haina orodha yoyote ya public holidays. Kwa hivyo hivi sasa tunaweza kubuni mpya, tukaziongeza na tumeona zikiongezeka. Lakini sasa tunasema kikatiba tunataka kuzitambua siku ambazo tutaziita national holidays, siku zetu sisi Wakenya ambazo tunataka kukumbuka. Zile ambazo sisi Wanatume tumezipendekeza na hapo baadaye mtaniambia ni gani mnataka ziongezwe, zipunguzwe au hata zitupiliwe mbali, mtanipatia maoni yenu.

Ya kwanza ni ile ya 1<sup>st</sup> June, na hiyo ndio siku ile ambayo tulipata Madaraka. Ya pili ni ile ya 12<sup>th</sup> December, na siku hii ndiyo ile tulipewa Jamhuri, Jamhuri day. Ya tatu ambayo ni mpya ambayo tunapendekeza tumepropose Katiba day, hii itakua ni siku ambayo hii draft ya katiba itakuwa sheria yetu, katiba yetu. Maana ya ku-propose hivyo ni hii, ile katiba ambayo tuko nayo sasa tulipewa mwaka wa 1963, kule Lancaster. Wazee wetu na wale ambao ni wazee katikati yetu watatukumbusha, waliwatuma wazee wenzao kule Lancaster. Ilikuwa ni wakati mgumu, kulikuwa ni mambo ya haraka ndio tupewe Uhuru. Hatukupewa nafasi sisi Wakenya kujijulisha ama kupeana maoni. Tulipata tu kuna document ambayo ni katiba na ndio imeendela kutuongaza mpaka hivi sasa.

Sasa tunasema hii Katiba tumeiunda sisi Wanakenya, kwa hivyo tunataka tuwe tukikumbuka vile ambavyo tuliunda na ndio maana tuka-propose tuwe na hiyo siku ya katiba Day. Hapo baadaye mtanipatia maoni yenu.

Tukienda chapter ya nne, Ukurasa ni wa tano, page 5, hapo tuna mambo mengine ya muhimu, ibara ni ya kumi na sita, article 16; Citizenship. Yaani ni nani ambaye anaweza kuwa raia wa Kenya. Na hapo tumebadilisha kidogo. Ya kwanza tukasema ya kwamba unaweza kuwa raia wa Kenya kwa sababu umezaliwa na mzazi ambaye ni raia wa Kenya. Iwe huyo mzazi ni mama au baba yako, ikiwa mmoja wa wazazi hao ni Mwanakenya, basi wewe unahaki ya kuwa raia wa Kenya. Kwa mfano ikiwa mimi nitaolewa na mtu ambaye si raia wa Kenya, mtoto wangu atakuwa na haki ya kuwa raia wa Kenya. Ikiwa Bwana Wachira ataoa mwanamke ambaye si raia wa Kenya, watoto wao watakuwa na haki ya kuwa raia wa Kenya.

Tena kuna jambo lingine ambalo tumebadilisha. Katiba tuliyonayo hivi sasa, mwanamume, raia wa Kenya, kama Bwana Wachira hivi, akisema amuo ama akipenda kumwoa mwanamke ambaye sio raia wa Kenya, huyo mwanamke ana haki ya kuwa raia wa Kenya. Lakini mwanamke akiamua kuolewa na mwanamume ambaye sio raia wa Kenya, huyo mwanamume hana haki ya kuwa raia wa Kenya. Na nyinyi pamoja na watu wengine waliuliza ni kwa nini?

Hapo tukabadilisha na tukasema ya kwamba yeyote ambaye anaoa ama kuolewa na raia wa Kenya, atakuwa na haki, huyu mtu wa ng'ambo, atakuwa na haki ya kuwa raia wa Kenya. (*Clapping from the audience*). Lakini pia tukasema ya kwamba, asante mama, pia tukasema ya kwamba huyu mtu ambaye anaoa ama kuolewa na raia wa Kenya atakaa miaka mitatu kabla ya kuwa na hiyo haki. Yaani, mimi nikiolewa na mwanamume ambaye sio raia wa Kenya au mwanamume akimwoa mwanamke ambaye sio raia wa Kenya, watakaa katika ndoa miaka mitatu ndio tujue wako serious na sio mchezo. Baada ya hiyo miaka mitatu, basi atakuwa na haki ya kuwa raia wa Kenya. Basi hiyo miaka mitatu tunawapatia ndio tuone kama kweli anatafuta tu uraia wa hii nchi yetu nzuri ama ni kweli amempenda huyo ambaye amemuoa ama kuolewa naye.

Tukiendelea pia katika hiyo sehemu ya uraia tunaongea juu ya yale ambayo kwa Kiingereza tunaita dual-citizenship. George alipitia hapo na akatoa mapendekezo yenu. Hapo vile ambavyo tunasema ni hivi, raia Mwanakenya ana haki ya kuwa raia wa nchi nyingine. Hivi sasa vile sheria ilivyo, ikiwa wewe ni raia wa Kenya na uende ng'ambo na ubarikiwe kupata uraia wa nchi nyingine, ule uraia wako wa Kenya unaishia papo hapo. Ukija huku unakuwa kama wewe ni mgeni, tourist kama wale wengine.

Niko na cousin yangu, mtoto wa uncle yangu ambaye alienda kule America, akapata kazi nzuri na akapewa uraia. Akija huku kwa sababu sasa uraia wake wa Kenya uliisha anakuja kama mgeni. Siku zake zikimalizika akienda airport, anaulizwa wewe Wanjiru, ulikuwa unafanya nini huku, wewe sio Mkenya, wewe ni raia wa America. Sasa tunasema ya kwamba, raia wa Kenya akibarikiwa na uraia wa nchi nyingine bado ataendelea kuwa raia wa Kenya.

Tukienda kwa chapter ya tatu, inaongea juu ya malengo ambayo serikali yetu tunaipatia, ni kurasa ya nne, nimewarudisha nyuma kidogo kwa national goals, kurasa ni ya nne, ibara ni ya kumi na nne, article 14. Hapo tunasema ya kwamba kuna yale malengo ambayo tunataka serikali yetu ifuate. Kwa mfano, wengi wenu mlisema na tumesikia leo asubuhi, mlisema hamtaki corruption, mmesema mnataka serikali ifanye hiki, na hiki na kile.

Hivi sasa ukiangalia katiba yetu, huwa tunasema serikali inajuhudi ya kujenga mabarabara nchini kote, mahospitali na kadhalika. Lakini katiba tuliyonayo hatujaipatia serikali malengo yoyote. Sasa tunasema kikatiba tumeweka katika ibara ya kumi na nne malengo ambayo tunataka serikali iangalie. Lakini hapo tukaongeza tukasema ya kwamba kila mwaka rais wa jamhuri ya Kenya atakuwa akisimama bungeni na anatoa repoti ya kuonyesha kwa mfano kama ni mashule, yamejengwa mangapi. Kwa hivyo kama ni mashule ataasema pengine ni kumi, moja iko Garissa, ingine iko Ndia, ingine iko Wajir, ingine Nakuru na kadhalika. Kwa hivyo kila mwaka tumempatia rais jukumu ya kuonyesha bunge na taifa lote yale ambayo serikali imeweza kufanya. Hilo ni jambo mpya ambalo haliko kwa katiba tuliyo nayo kwa sasa.

Ibara ya kumi na tano, tena inafanya jambo lingine ambalo ni mpya kabisa. Hapo tunakupatia wewe mwananchi pia, kwa sababu hii katiba ni yako, sio ya serikali, ni yako pia. Tunasema pia wewe unajukumu fulani kikatiba. Ya kwanza, wewe mwananchi umepatiwa jukumu ya kuijua hiyo katiba yako. Na tumeanza kukujulisha hiyo katiba hata kwa wakati huu ambapo

bado iko in the draft stages, yaani iko katika mswada. Bado haijakuwa sheria na umeanza kuijua. Na hata ikiwa sheria umepatiwa jukumu ya kuijua na kuulinda kikatiba.

Jukumu ingine ambayo umepewa kikatiba ni ile la kupiga kura. Mara nyingi huwa tunaenda kupiga kura siku ya kura na unawasikia wengine wakisema mimi nilichoka, nilingoja na ilipofika saa saba, nilihisi njaa nikaenda kula. Na si fulani tu ndiye atachaguliwa, hivyo ndivyo sisi huwa tunasema. Sasa tunasema tumekupatia jukumu, wewe Mwanakenya ya kupiga kura kwa sababu bunge ni yako wewe Mwanakenya, na uchaguzi ni wako wewe Mwanakenya.

Tukiendelea kwa chapter ya tano, ambayo iko kurasa ya sita, page 6. Chapter ya tano tunaongea juu ya haki zako wewe kama Mwanakenya. Wewe unahaki gani kama raia wa Kenya? Ni mara nyingi sisi Wanakenya tunanyang'anywa haki zetu na hatujui ya kwamba hiyo ni haki yako Kikatiba. Sasa tunataka tuzijue na tuzielewa ndio mtu akikupokonya, unajua hiyo ni haki yako. Nitasisitiza zile ambazo ni za muhimu zaidi.

Ukiangalia ibara ya thelathini na mbili, article 32, hapo tunasema ya kwamba, kila raia wa Kenya ana haki ya kuwa hai. Wewe nami, sisi sote tunahaki ya kuwa hai. Hapo tumebadilisha tena jambo lingine. Tukasema ya kwamba ile hukumu ya kifo, the death penalty, tumeiondoa na tukasema ya kwamba sasa hakutakuwa na hukumu ya kifo. Mtanipatia maoni yenu baadaye. Lakini hatusemi ya kwamba wale wamehukumiwa kifo, ati ya kwamba tunasema tumeiondoa hiyo hukumu ati hii Katiba ikija ndio sheria mtakutana pale sokoni. Tunasema ya kwamba tumeibadilisha iwe ni jukumu ya kifungu cha maisha, life imprisonment. Kwa hivyo ikiwa kuna mtu ambaye amehukumiwa kifo, hiyo hukumu haitatekelezwa, itabadilishwa iwe hukumu ya maisha.

Tena hapo katika ibara ya thelathini na nne, tumeongea juu ya haki za Wakenya. Yaani tukasema kila Mwanakenya ana haki sawa na Mwanakenya mwenzake, iwe ni wa kabila fulani ama ingine wote wanahaki sawa. Iwe mmoja ni wa dini fulani, ama ingine haki zao ni sawa, iwe huyu Mwanakenya ni mlemavu, ana haki sawa na yule mwingine. Iwe ni kijana, mwanamke, mwanamume, haki ni sawa kwa Wakenya wote.

Tena tukaendelea kwa kutambua sehemu fulani ama sehemu mbali mbali ambazo tumesema, zinahitaji usadizi kidogo ili ziwe sawa na Wakenya wale wengine. Sehemu ya kwanza ambayo tumeitambua ni ile ya kina mama katika ibara ya thelathini na tano, na maoni yenu tuliyasikia hapo mbeleni kuhusu kina mama.

Katika hiyo ibara tumesema ya kwamba wanawake watakuwa na haki sawa na wanaume. Kwa hivyo ikiwa ni mambo ya kurithi, mtoto wa kike, mtoto wa kiume mtoto wa kike ambaye hajaolewa, na mtoto wa kiume wote wanahaki sawa za kuridhi.

Kwa hivyo usawa wa wanawake na usawa wa wanaume.

Tena tukaendelea hapo kuongea juu ya sehemu ingine ama kundi lingine ambalo tumesema lazima isaidiwe kikatiba ndio iweze kupata haki sawa na wengine. Hicho ni kile kikunde cha wale ambao ni wazee kati yetu. Kwa hivyo tukasema ya kwamba watu wazee watakuwa na haki za kushiriki katika mambo ya taifa letu. Kama ni kijijini na mtu ni mzee na anataka kujishirikisha

pengine kanisani, mambo ya kujenga mashule, mambo ya katiba na kadhalika, ana haki sawa na mwenzake.

Lakini pia tukasema ya kwamba hiyo sehemu ya watu wazee, ina haki ya kulindwa kwa sababu wanahitaji kulindwa pengine zaidi kidogo kuliko wenzao. Inahaki ya kulindwa na familia zao. Kwa hivyo ikiwa umetoka kwa familia ambayo iko na mtu mzee, ukumbuke ya kwamba sasa kikatiba tunakupatia jukumu ya kuwalinda watu ambao ni wazee katika familia yako. Iwe ni mama, baba, nyanya na kadhalika.

Pia, tulisema serikali iko na jukumu ya kuwalinda watu ambao ni wazee. Hapo pia tukasema kila mwaka, wawe wakituonyesha vile ambavyo wameendelea kuona ya kwamba haki za watu ambao ni wazee katika taifa letu zinaendelea kulindwa.

Katika ibara ya thelathini na saba, article 37, ukurasa wa saba, tunaongea kuhusu haki za watoto. Watoto wana haki gani? Ya kwanza tukasema ya kwamba watoto wote wanahaki sawa. Iwe huyo mtoto amezaliwa kwenye familia ambayo ana baba tu hana mama, ama amezaliwa kwenye familia ambayo ana mama tu, hana baba. Au hata iwe ni mtoto ambaye hatuwajui wazazi wake ni nani, tulilmpata njiani akilia na tukamwokota. Huyo mtoto na watoto wengine wote wana haki sawa. Haki moja ambayo tumesema ni sawa na mtaipata kwa ibara ya hamsini na nane, ni ile haki ya elimu.

Katika ibara ya hamsini na nane, tumesema ya kwamba, watoto wanahaki ya kupewa elimu ya bure ya primary. Hivi sasa tunaambiwa elimu ya primary ni ya bure. Huwa mnalipa? Nyinyi ni wazazi. Huwa mnalipa elimu ya primary? Lakini ukiangalia katiba, hakuna jukumu yoyote katika katiba tuliyonayo yakupeana hiyo elimu ya bure. Ndiposa tukasema ya kwamba, katika hii draft tume-propose kuwe na elimu ya lazima na ya bure.

Ya bure kumaanisha ya kwamba mtoto wako akifukuzwa, ati ametolewa shuleni kwa sababu hujalipa deni fulani, hii katiba ikiwa ndio tutajaliwa iwe sheria, hapo serikali itakuwa na la kujibu kwa sababu elimu ya primary ni ya bure. Na wewe mzazi ukipatikana ati mtoto wako ako shambani kwa sababu ni wakati wa kupanda, umesema leo asiende shuleni, akusaidie kupanda, hata wewe utakuwa na la kujibu. Ni ya bure na ya lazima. Hivyo ndivyo tume-propose.

Lakini elimu ya hapo baadaye, secondary, university, ma-college, tumesema ya kwamba kila mwaka serikali itakuwa na jukumu ya kutuonyesha imeendeleaje kuhakikisha ya kwamba mashule yanaendelea kujengwa na watoto wanapata nafasi kwa hiyo elimu ya hapo baadaye.

Sehemu ingine ya mwananchi ambayo tumeitambua ni ile ya wananchi ambao wako na disability, persons with disability. Na hapo tukasema ya kwamba ikiwa pengine ni mtu haoni, mtu ambaye anahitaji kutembea na cane ama na wheel-chair na kadhalika, tunasema huyo mwananchi ako na haki sawa na wananchi wenzake. Kusiwe na ubaguzi wowote hata kwa sector hiyo. Tena tukasema ya kwamba, na George alikuwa amegusia hapo, pahali popote pa public ambapo patajengwa, kwa mfano iwe ni hoteli na ni hoteli ya gorofa tano, lazima watilie maanani ya kwamba kuna uwezekano kuje mtu ambaye hatawezakuzipanda hizo gorofa. Kwa hivyo kikatiba, tumewapatia jukumu wawe wakijenga wakijua huyo mtu atapitia wapi.

Ikiwa ni basi, na matatu ambazo tunatumia, hii katiba ikijaliwa iwe sheria, nao wajue na wafahamu kuna uwezekano wa kuwa



na mtu katika hiyo basi ambaye atahitaji kukalia wheel chair, kwa hivyo waache nafasi atakayoweza kutumia. Kwa hivyo tumesema kikatiba kuwa hao watu tumewa-recognize na tumesema ya kwamba walindwe na wawe na haki ambazo ni sawa na wenzao.

Pia katika hiyo sehemu ya haki, nimesema ninasisitiza zingine. Tukiangalia kutoka ibara ya hamsini na saba, ukurasa wa tisa, vile tumefanya hapo, tumeleta haki zingine za Mwanakenya ambazo haziko kwenye katiba ambayo tuko nayo sasa. A new generation of rights, mpya kabisa na tena ngumu kabisa. Hapo tumesema ya kwamba kuna haki za matibabu. Serikali kila mwaka inatuonyesha ya kwamba inaendelea kuwapatia wananchi matibabu ambayo yanafaa kila mwaka.

Pia tumesema ya kwamba, kukitokea mambo ya emergency, yaani kwa mfano kuna pahali ambapo ajali imetokea na mtu amekimbizwa kwenye hospitali fulani ambayo iko karibu, mara nyingi tunasikia kwamba huyo mtu aliulizwa na pengine yuko katika hali mahututi anaulizwa alete deposit ili wapate kumsaidia. Sasa tunasema ya kwamba hakuna mtu ambaye anaweza kukatazwa hivyo huduma wa kwanza katika hospitali yoyote ambayo huyo mtu anahitaji kupelekwa.

Kwa mambo ya chakula, article 60 tukasema kila Mwanakenya anahaki ya kuwa hana njaa. Hatusemi Wanakenya wapewe chakula aina fulani, ama aina ile nyingine, ama ile ya hoteli kubwa ama ile ndogo. Tunasema hakuna Mwanakenya atakuwa kwa hali ya kukumbwa na njaa. Kila mwaka, serikali katika bunge itakuwa ikituonyesha imeendeleaje, kuhakikisha kuwa kila Mwanakenya ana chakula na maji ya kutosha. Kwa hivyo hizo ni haki zako wewe kama Mwanakenya. Ni nyingi zaidi, nimesema ninasisitiza tu chache, zingine utapata kuzisoma hapo baadaye, na nitakusihi kama Mwanakenya uzielewe, na uzijue, ndio tukijaliwa hii iwe sheria yetu uwe umwezijua na kuzifahamu, usipokonywe haki zako.

Nitaendelea sasa kwa sehemu nyingine, ambayo ni sehemu inayohusika na mambo ya uchaguzi. Chapter 6, mambo ya uchaguzi ambayo iko ukurasa...

**(Interjection from the audience):** (Inaudible)

**Eunice Gichangi:** Ni tofauti na yangu, usijali ninafahamu lakini niko na watu watanisaidia hapa. Yangu ni ile aina ingine, sio ile ya gazeti.

Tukiangalia chapter 6, page 11, aha, kurasa ni ya kumi na moja, page number 11. Hapo tunaongea juu ya the Electoral system and Process. Hapa ningependa tuelewe kwa sababu wengi wamepeva hadithi nyingi ambazo sio za kweli. Nikiendelea kusoma gazeti hata leo ninaona ya kwamba kuna wale ambao hawaelewi vile ambavyo tuna-propose. Kwa hivyo ninataka muelewe, ndio msidanganywe na yeyote.

La kwanza tunasema hivi, ni juu ya vyama vya kisiasa, katika article 89. usijali hata kama hutaiona sasa, nita summarise kutoka chapter ya sita, ya saba na ya nane. Ya kwanza ni kuhusu vyama vya kisiasa. Kuhusu vyama vya kisiasa tunasema hivi, kila chama cha kisiasa kitakuwa kikiomba registration kutoka kwa Tume ya Election, Electoral Commission. Hapo ndio watakuwa wakipata registration.



Qualifications za chama chochote, ili kiweze kupata registration ni kwamba, lazima kionyeshe ya kwamba kiko na ile tunaita kwa Kiingereza national character. Yaani kimeweza kuonyesha katika manifesto ya kwamba kitajaribu kuwavutia Wakenya wote. Tena, tunasema ya kwamba hicho chama lazima kionyeshe kwa manifesto ya kwamba kitajaribu kuulinda katiba na kuzilinda haki za Wanakenya.

Jambo ambalo ni mpya na tumeliweka katika katiba yetu ni lile ambalo mtalipata katika article 90, ibara ya tisini. Hapo tumesema ya kwamba na hapo baadaye, kila chama cha kisiasa kitahitajika kiweke hesabu sawasawa, ili kila wakati kiweze kutuonyesha ya kwamba hizi ndizo pesa ambazo tulizipata, na hivi ndivyo ambavyo tulizitumia pesa hizo ambazo tulizipata. Hivi sasa tunajua ya kwamba huwa tunasikia chama fulani kimepata pesa, kimefanya mambo fulani, lakini hatuelewi hizo pesa zimetoka wapi na zimetumiwa kivipi. Kwa hivyo tunasema ya kwamba hata hivyo, vyama vya kisiasa lazima viwe accountable kwa mwananchi. Tuwe tukiona vile ambavyo wanatumia pesa.

Pia tume-propose, na hayo nilisikia pia mliyapropose kama watu wa Ndia, tumepropose ya kwamba, kuwe na political parties fund. Yaani kila mwaka, budget ikisomwa, kuwe na pesa ambazo zimetengwa kutumiwa na vyama vya kisiasa, na hizo pesa zitakuwa ni 0.3% ya national budget. Zitengwe, ziwekwe kwenye account, ziwe ni pesa za kutumiwa na vyama vya kisiasa. Lakini chama chochote ambacho kitapenda kuwa qualified ama kupata njia ya kutumia hizo pesa zetu, kwa sababu ni zetu sisi Wanakenya, lazima kionyeshe ya kwamba kimepata asilimia tano, 5% of the national votes ili kiweze kufungua njia ya kupata sehemu ya hizo pesa. Kwa hivyo tumesema kuwe na hiyo fund lakini chama kipate asilimia tano ya kura zote nchini.

Jambo lingine ambalo ni la muhimu sasa ni kuhusu jinsi ya uchaguzi, ni jinsi gani tume-propose kuhusu uchaguzi? Hayo mtapata kwenye chapter ya sita na ya saba, ni mengi lakini ninataka ni summarise ili tuweze kuelewa.

Hivi sasa vile ambavyo tunafanya uchaguzi, tukienda kupiga kura siku ya uchaguzi, watu ambao wanataka kuchaguliwa kuwa wabunge huwa wanatajitokeza sivyo? Na huwa tunafahamu fulani na fulani na fulani ndio wanapigania hicho kiti cha ubunge. Hao watu wakijitokeza, sisi tunawapigia kura, tunampigia yule ambaye tukimwangualia huyo mtu awe ni mwanamume au mwanamke tunaona kuwa yeye ndiye ametufurahisha na tunampigia kura huyo mwananchi. Hiyo ndio system ambayo tunaitumia na yule ambaye anapata kura nyingi zaidi ndio anateuliwa kuwa ndiye tumemchagua na ndiye mbunge wetu.

Nchi zingine huwa zinatumia system tofauti kabisa. Ukiangualia nchi zingine, vile ambavyo zinafanya ni hivi. Kabla ya uchaguzi, kila chama cha kisiasa kinatengeneza list ama orodha ya watu ambao wangependa wachaguliwe wawe wabunge kwa tikiti ya hicho chama. Kwa hivyo chama kama tumseme kwa mfano chama A, kitatengeneza orodha tuseme ya kwamba mkikichagua chama chetu, wale ambao mtawachagua wawe wabunge ni number one, number two, number three mpaka wa mwisho. Chama kile kingine B, kinatengeneza orodha, kinaonyesha wale watu ambao watachaguliwa kutoka number one mpaka wa mwisho. Chama kile kingine kinafanya vivyo hivyo.

Siku ya uchaguzi, wananchi wa nchi hizo huwa hawaendi kumchagua mtu binafsi, bali wanaenda kukichagua chama. Wanaangualia ile orodha ama ile list ambayo imewafurahisha kabisa, wakiangualia wanaona ya kwamba kweli nikikichagua hiki

chama na kipate kuwaingisha watu wengi zaidi kwenye bunge kiko na watu ambao wamenifurahisha. Ikiwa pengine wewe ni mtu uko na disability, unaangalia kile chama ambacho kimewakumbuka watu ambao wako na disability. Ikiwa wewe ni kijana, unaangalia kile chama ambacho kimekumbuka watu wa aina hiyo. Kwa hivyo mtu huenda kupigia kura chama ambacho kimependeza.

Tulisoma sana, tukaangalia hizo systems zote, tukafanya research hata tukawaita wataalamu kutoka nchi jirani na halafu tukaona ya kwamba tungependa tuwe na system ambayo inatumia hiyo mitindo yote. Kwa hivyo tumepropose tutakuwa tukiendelea na uchaguzi hivi.

Ya kwanza tumesema kuhusu bunge, tunataka kuwe na nyumba mbili za bunge vile mlikuwa mmelezwa mbeleni. Wakati wa independence, tulikuwa na nyumba mbili, the lower and the upper house, kwa hivyo tutakuwa na nyumba mbili. Ile nyumba ya chini, mapendekezo yetu ni haya, kwanza Wakenya wanataka kuendelea kuwachagua wabunge, yaani yule mtu ambaye wamemwangalia wakaona anafaa kuwa mwana bunge wa constituency yao. Kwa hivyo tumesema ya kwamba kila constituency itaendelea kumchagua mwanabunge. Kwa hivyo tutakuwa bado na wale wanabunge mia mbili na kumi, two hundred and ten, kutoka kwa kila constituency.

Lakini tukaongeza viti vya hiyo nyumba ya chini, tukasema kutakua na viti mia tatu katika hiyo nyumba ya chini. Viti mia mbili na kumi, tayari tumetenga tumesema vitatoka kwa kila constituency. Hivyo viti vinavyosalia, viti tisini, tumesema ya kwamba tutatumia ile system ya party list. Kwa sababu gani? Sababu ni kwamba tunataka vyama ambavyo vina national outlook. Isiwe kuna chama cha kisiasa ambacho kina wafuasi kutoka Ndia pekee, tunataka vyama vijulikane katika kila pembe ya nchi yetu.

Kwa hivyo hivyo viti tisini, those ninety seats, tunasema ya kwamba kila chama cha kisiasa, kabla ya uchaguzi, kitahitajika kutengeneza orodha ya wale ambao tungependa wachaguliwe kuwa wabunge kupitia kwa chama chao. Halafu wakifanya campaign pia, wanatuonyesha hiyo orodha. Tukifika siku ya uchaguzi, tutakuwa tukipiga kura mara mbili, moja unampigia mbunge wako kupitia kwa constituency yako kama kawaida. Kura ya pili unapigia chama ambacho kimekufurahisha. Ukiangalia hiyo orodha unaona ya kwamba kweli nikikichagua hicho chama kitanisaidia sana bungeni, wako na watu ambao ninaona ni bora zaidi. Baadaye kile chama ambacho kitaweza kupata kura nyingi zaidi, kitaweza kupata viti vingi zaidi kupitia vile viti tisini.

Kwa hivyo sasa vyama vyote vitahitajika vijulikane katika kila pembe, sasa watakuwa forced. Hakutakuwa na chama cha Ndia constituency pekee yao, ama Central, ama Eastern, hapana. Sasa watakuwa wakijaribu kuwavutia Wakenya wote kutoka kila sehemu. Hiyo ndiyo bunge yako ya chini, the lower house ama the national assembly.

Tena katika ile orodha, tumesema kila chama kitakuwa kikitengeneza orodha. Tume-propose ya kwamba, jina la kwanza katika ile orodha ikiwa litakuwa ni la mwanamume, la pili liwe ni la mwanamke, la tatu mwanamume, la nne la mwanamke na kuendelea hivyo. Hiyo ni kuhusu bunge ya chini. Ninataka uielewe kabisa. Tumesema viti ni mia mbili na kumi ambavyo tumetoa katika kila constituency, na viti tisini ambavyo tumetoa katika ile orodha ambayo imetoka katika kila political party.

Hiyo ndiyo bunge yako ya chini.

Nimetaja jina kama nomination pahali?

**Response from the audience:** Hapana.

Na ninasikia ya kwamba mnaambiwa kuwa hawa watu ni wabaya. Wameongeza nominations zikawa tisini. Ni kweli? Hapana, hakuna nominated seats. Kwa hivyo tumesema vile viti ninety vinatoka kwenye orodha.

Sasa tunaenda kwa nyumba ya pili. Na kama George alivyowaeleza, hiyo nyumba ya pili ya bunge tumeiunda kwa sababu wananchi walisema ya kwamba wanataka serikali iletwe karibu nao. Na nyinyi ninasikia mlisema hivyo pia, ati serikali iletwe karibu. Ile serikali ya Nairobi iko mbali, hatuielewi hebu serikali iletwe karibu na sisi. Na baadaye mtaenda mtajisomea chapter ya kumi, lakini hivi sasa nitaomba niwapatie summary ama muktasari wa vile ambavyo tume-propose.

Vile ambavyo tumepropose ni hivi. Serikali sasa tumeileta ndio ianze kutoka kwa village na village tumesema iwe ndiyo sub-location. Kwa hivyo sasa tumependekeza ya kwamba, kila sub-location itakuwa na kabunge kake kadogo. Chapter 10 is on page 26, ukurasa wa ishirini na sita. Kwa hivyo vile tunasema ni hivi... kutoka ibara ya 213, nitawapatia summary. Vile tumesema ni kwamba kila sub-location ambayo tumeita village, kijiji kwa sababu watu wa sub-location huwa wanajuana wote. Kwa hivyo tumesema sub-location ndiyo kijiji chetu katika hii draft.

Kila sub-location itakuwa ikiwachagua watu wasiopungukia sita na wasiozidi kumi, 6 – 10 people ambao wanaketi kwenye Village Council. Halafu pia kutakuwa na village administration. Hiyo ndiyo village administration na Village Council, si iko karibu sasa?

Kutoka kwa village ama sub-location, tumesema tutakuwa na Locational Council. Tumetoka sub-location, tumeenda location na location tukasema kuwe na Locational Council. Hiyo Locational Council, wale ambao wataketi katika hiyo Council ya location watakuwa wametolewa kutoka kwa kila sub-location. Kila sub-location itawateuwa watu wawili ambao wataenda kuketi kwenye Locational Council, mmoja wa hao watu akiwa ni mwanamume na yule mwingine ni mwanamke.

Tena tukitoka hapo tunaenda kwa district. District ndiyo itakuwa kiini cha serikali, the focus of devolution katika Kiingereza. Hapo tunasema ya kwamba, kila district itawachagua watu wasiopungua ishirini na wasiozidi thelathini, 20 – 30 people ambao wataketi kwenye District Council na pia kutakuwa na district administrator. Kwa hivyo kiini cha serikali tumesema ni district, lakini pia huko chini tumetambua ya kwamba kutakuwa na Locational Council, locational administrator, Sub-location ama Village Council na village administration. Tuko pamoja?

Lakini pia, kila district itakuwa ikiwachagua watu wawili kutoka kwa District Council ambao wataenda kwa Provincial Council, mmoja mwanamume na yule mwingine mwanamke, na wataketi kwenye Provincial Council. Lakini pia ukumbuke ya kwamba kiini cha serikali, kiini cha devolution katika Kiingereza ni ile district, district government. Tukemuja mpaka kwa district. Hapo

tulijadiliana sana katika Tume, siku za mwisho tukiwa kule Mombasa kwa vile wengine walikuwa wanasema iwe province.

Lakini tena tukaangalia, province mara nyingi huwa iko mbali sana na watu sindio. Kama Moyale na Eastern Province wakija kule Embu, ni mbali sana. Ndio tukasema ya kwamba district ndio itakuwa karibu lakini hata tukitoka kwa district tunaenda chini kidogo mpaka kwa village.

Sasa hapo ndio tunasema ya kwamba kutoka kwa hicho kiini cha serikali, from that focus of devolution, kila district itakuwa ikifanya uchaguzi na tulielezwa na George. Kila district inafanya uchaguzi, inamchagua mwanabunge mmoja. Kwa hivyo mtakuwa mkichagua mara nyingi na hamtachoka. Mnamchagua mwana bunge mmoja ambaye mtampeleke straight anaenda kukaa katika ile nyumba ya bunge ya pili, the upper house, na tumepropose iitwe National Council.

Kwa hivyo katika hiyo National Council, kutakuwa na wanabunge sabini ambao kila mmoja ametumwa na district yake, amechaguliwa kutoka kwa district. Lakini viti vya National Council ni mia moja, kwa hivyo sabini tumepatia kila district imchagua mwana bunge mmoja, lakini tukasema hivyo viti thelathini vitengewe kina mama.

Kila province itahitajika kuwachagua kina mama wanne waende kuketi katika National Council. Lakini wakichaguliwa wanne kutoka kila province watazidi vile viti thelathini kwa hivyo tukasema Nairobi itawateua kina mama wawili kwa sababu tayari Nairobi imeshapata advantages zingine hapa na pale. Kwa hivyo hiyo ndiyo nyumba yako ya pili ya bunge. Mtapata nafasi na mtanieleza kama inawaridhisha au vipi hapo baadaye. Kwa hivyo nyumba ya pili ndio hiyo tumesema iko na viti sabini, kutoka kwa kila district, mwanabunge mmoja na viti thelathini, kutoka kwa kila province wanawake wanne.

Jambo lingine muhimu ni hili, ni nani ambaye anaweza kuwa mwanabunge? Na hapo vile ambavyo tumependekeza ni hivi, mtu ambaye atakuwa mwanabunge awe kwanza ni raia mzaliwa wa Kenya. Niko kwenye article 108, ibara ya mia moja na nane, nimerudi tena nyuma, kurasa ni ya kumi na nne. Tutaendelea kutoka hapo pamoja.

Yule ambaye atateuliwa awe mwanabunge tumesema la kwanza awe raia mzaliwa wa Kenya, kurasa la kumi na nne. Pili, awe ikiwa atakuwa mwanabunge wa ile nyumba ya chini, the National Assembly, lower house, basi awe amefikisha miaka ishirini na moja. Ikiwa ni mwanabunge wa ile nyumba ya pili, National Council, awe amefikisha miaka thelathini na tano. Hapo tuliona ni vizuri tuongeze kidogo miaka juu ya experience. Mambo ya masomo, tukasema kila ambaye atapenda kuwa mwanabunge lazima awe amesoma, na tulikuwa tumeelezwa mbeleni, awe amehitimu O level education, Form IV na awe na shahada ama certificate ya kuonyesha kwamba alipata pass, alipita. Kwa hivyo hapo tumeweka minimum ya O level education.

Lakini pia awe ni mtu ambaye anaelewa kabisa, anaweza kuongea, na hata kuandika kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Ili akienda bungeni na waseme wanatumia Kiingereza na akirudi mmulize maswali atakuwa mko pamoja na yeye, alielewa. Tena tunasema lakini ikiwa ni mtu ambaye anatumia sign language, lugha ya ishara amabayo inatumiwa na ndugu zetu ambao ni bubu, tunasema huyo pia atakuwa qualified na ikiwa ni Braille pia yuko qualified.

Tena hapo tuliongezea katika article 112, na tulielezwa hapo mbeleni na George, ya kwamba ukipenda ama constituency

ikimchagua mwanabunge na wanataka kumwondoa kwa sababu pengine wanaona pengine hafanyi yale ambayo walimtaka afanye, ya kuwa hatendi yale ambayo aliwaahidi, watakuwa na uwezo wa kumwondoa. Ikiwa asilimia thelathini, 30% ya wale ambao ni registered voters, wamejiandikisha kupiga kura watasign, wataweka kidole kwa karatasi ambayo tunaita petition.

Hiyo petition itapelekwa mbele kwa Speaker, awe ni wa nyumba ya chini ama ile ya juu kulingana na pahali ambapo huyo mwanabunge anaketi. Kufuatia hiyo petition, huyo Speaker atanzisha uchunguzi wa hadhara ule ambao tunaita public inquiry. Na atatoa repoti ya kusema ya kwamba ni kweli vile hao voters walisema au sio kweli. Ikiwa ni kweli, huyo mwanabunge hajatenda yale ambayo alitakiwa atende ataweza kuondolewa na mwingine achaguliwe, bado na hao registered voters. Tuko pamoja?

**Response from the audience:** Eeh.

Tukiendelea sasa kwa sehemu ya serikali ambayo tumepropose, chapter 8 ibara mia moja na hamsini, ukurasa wa 19. Tukienda kwa serikali, muundo wa serikali ambao tunaopendekeza ni huu. Ya kwanza tunasema katika ibara ya mia moja na hamsini, article 150, ya kwamba kutakuwa na rais wa Kenya, hapo hatujabadilisha. Huyo rais atakuwa ndiye the head of state, mkuu wa nchi yetu, hatujabadilisha. Pia tukasema ya kwamba yeye atakuwa amri jeshi mkuu, Commander-In-Chief of the defence force, hatujabadilisha. Tena tukasema ya kwamba huyo rais tukimwangukia tunataka tuwe tukiona ya kwamba yeye ni mtu ambaye anatuonyesha umoja wetu kama wananchi. Tukimwangukia tunaona katiba yetu inaendelea kulindwa, umoja wetu, national unity.

Kwa sababu hiyo, tumependekeza ya kwamba rais akichaguliwa kuwa ndio rais wetu, hatakuwa mfuasi wa chama chochote. Jambo ambalo tunasema ni hili, mtu ambaye atapenda kuchaguliwa awe rais, anaweza kuchaguliwa akipitia kwa njia ya chama. Kama vile ambavyo tumeona hivi majuzi vyama vimeanza kuwapendekeza marais wao. Basi tunasema huyo rais anaweza kupewa nomination ama kupendekezwa na chama chake.

Lakini pia tume-introduce jambo mpya. Tumesema ya kwamba sio lazima yule ambaye angependa kuchaguliwa awe rais ama hata awe mwanabunge, awe amefanya hivyo kupitia chama chochote. Anaweza kuwa amejisimamia pekee yake, yeye sio mfuasi wa chama chochote, yaani independent candidate. Sio lazima mtu awe mfuasi wa chama eti ndio achaguliwe. Anaweza kuja awaambie mimi ninaitwa Eunice na ningependa niwe mbunge wenu na mimi sio mfuasi wa chama chochote na mnaweza kumchagua.

Hapo pia tunasema rais anaweza kupendekezwa na chama chake ama ajipendekeze mwenyewe, awe independent candidate. Lakini akichaguliwa, hatakuwa tena mfuasi wa chama chochote, hatakuwa ofisa wa chama chochote, atakuwa ni head of state ambaye ni symbol of national unity. Hatutakua tukikumbushwa ya kwamba yeye ni mfuasi wa chama chochote. Kwa hivyo hiyo ni proposal moja ya urais.

Jambo lingine ambalo tumependekeza kaitika ibara ya mia moja hamsini na sita, 156, ni nani ambaye anaweza kuwa rais wa

Kenya? Ya kwanza ni kuwa lazima awe raia aliyezaliwa Kenya, ama mnataka kuongozwa na raia wa nchi zingine? La, raia mzaliwa Kenya. Ya pili tukasema ya kwamba kuhusu miaka awe amehitimu zaidi ya miaka thelathini na tano, hapo kuna experience kidogo, lakini pia asiwe amezidi miaka sabini. Kwa hivyo siku ya nomination akija lazima miaka yake iwe haijapitisha sabini, iwe iko kati ya thelathini na tano, na sabini.

Hapo pia mmedanganywa mkaambiwa ya kwamba hao wanatume wamewakataza watu wengine ambao tayari tunawajua wanataka kuwania hicho kiti, na pengine wamehitimu na kupita hiyo miaka, ati tumewakataza. Hayo sio mambo ya kweli. Vile ambavyo tumesema ni hivi, katika uchaguzi ambao utafanya baada ya ule wa 1997, si uchaguzi wa mwisho ulikuwa 1997? Na hivi sasa hatujui uchaguzi ujao ni wa siku gani na hatujui kama utafanywa chini ya hii katiba ama ile nzee.

Lakini ikiwa huo uchaguzi utafanywa chini ya hii katiba mpya ambayo tunapropose, basi tunasema ya kwamba, mtu yeyote ambaye anapigania kiti chochote cha kikatiba, urais, ubunge na kadhalika, qualifications zake kwa hiyo mara ya kwanza hatutaziangalia katika hii katiba mpya bali tutatumia ile katiba nzee. Tuko pamoja?

**Response from the audience:** Ndio.

Lakini uchaguzi ambao utakuwa wa pili na watatu na kuendelea, lazima atajipanga, aangalie kila kitu ajue niaje. Kwa hivyo hapo msidanganywe.

*Murmuring from the audience*

Jambo lingine ni... inaonekana mmefurahishwa na jambo hilo? Mlikuwa mmefungiwa, hamjafungiwa.

*Clapping from the audience*

Jambo lingine tunasema ya kwamba, katika hii Katiba yetu ambayo tunaipropose, yule ambaye atapenda kupigania kiti cha rais, lazima awe amesoma mpaka akahitimu shahada ya degree. Hatusemi ni degree ya area gani ama gani, lakini amesoma, amefika university, amemaliza na akafuzu na degree. Lakini tena hapo uchaguzi wa kwanza baada ya ule wa 1997 hatutakuangalia sana, lakini wa pili na wa tatu na kuendelea mpaka sheria ibadilishwe, lazima mtu awe amesoma mpaka hiyo level.

Tena mambo mengine ambayo tumesema ni haya ya kamba yule ambaye atateuliwa, ama yule ambaye atapenda kuteuliwa awe rais wa nchi ya Kenya, lazima awe amemtambua makamu wake kutoka hapo awali. Kwa Kiingereza tunasema running mate. Yaani ikiwa mimi nitapenda mnichague niwe rais wa jamhuri yetu, lazima niseme ya kwamba mkinichagua, Bi Mercy ndiye atakuwa naibu wangu. Ili mkienda kunipigia kura, mtajua ya kwamba mtakuwa mmempigia Bi Mercy ambaye ni naibu wangu. Halafu mimi nikiingia kazini sitakuwa na uwezo wa kumwondoa Bi Mercy kwa sababu alichaguliwa kwa uwezekano wenu. (

*Clapping from the audience*). Hiyo ndiyo inaitwa running mate kwa Kiingereza.

Kwa hivyo mkienda kuchaguana kutumia hii katiba mpya, lazima mtamwangalia sana yule ambaye anachaguliwa kuwa makamu.

Na mnaangalia, mkichaguana mnawachagua kama team, yaani wakiwa wote wako pamoja.

Pia jambo lingine na mlikuwa mmelezewa na George hapo mbeleni, tunapendekeza ya kwamba siku ya uchaguzi wa rais iwe imetambulika kikatiba. Yaani tunasema ya kwamba hii katiba ikija iwe ndio katiba yetu mpya, tunasema ya kwamba, mika mitano ikiisha tunajua ya kwamba huo ni mwaka wa uchaguzi wa urais. Sasa hiyo miaka mitano ikiisha, tukifika mwezi wa Agosti, juma la pili la huo mwezi, Jumanne ikifika yaani Tuesday ya huo mwezi wa Agosti basi hiyo siku tutakuwa tunajua ni siku ya uchaguzi. Wewe unajua, mimi ninajua, rais anajua, na kila mtu anajua. Kwa hivyo tutakua tunajua kwamba hiyo siku hatuendi kazini bali tunaenda kumchagua rais. Na mkiangalia article 155, hivyo ndivyo tumeandika.

Tena tukasema ya kwamba yule ambaye atachaguliwa awe rais lazima apate nusu ya kura za nchini kote. Pia tukija kwa maprovinces apate asili mia ishirini ya kura za nusu za province ambazo tuko nazo. Provinces tuko na nane, kwa hivyo apate kura asili mia ishirini kutoka kwa province nne ndio aweze kuchaguliwa awe rais.

Jambo lingine mlikuwa mmelezewa ya kwamba katika article 153, rais anaweza kuondolewa ikiwa ametenda jambo ambalo sio la kikatiba ama sio la kisheria. Ikionekana ya kwamba ametenda jambo kama hilo anaweza kuondolewa ikiwa asili mia sitini na sita ya wanabunge watakubali hiyo motion. Kwa hivyo ikiwa asili mia sitini na sita ya wabunge watatizama waone ya kwamba rais ametenda jambo ambalo sio la kikatiba, sio la kisheria, basi wataweza kumwondoa.

Lakini pia tunapendekeza ya kwamba ikiwa rais, wanabunge wataangalia pia waone ya kwamba pengine afya yake imezoroteka na akashindwa kuendelea na kazi, katika article 162, ikiwa nusu ya wanabunge watapendekeza ya kwamba rais aondolewe kwa sababu afya yake imedhoofika Basi hilo pendekezo lao watampatia hakimu mkuu, Chief justice, naye ataunda committee ya madaktari ambao watakuwa watano, wataiangalia afya ya rais, waandike certificate ya kuonyesha vile ambavyo wameona. Ikiwa kweli afya ya rais haimruhusu aendelee na kazi basi ataondolewa.

Pia tukapendekeza ya kwamba, katika article 164, ikiwa rais ataondolewa ofisini kwa sababu za kikatiba na kisheria, basi yule ambaye atachukua ofisi ya urais ni nani? Makamu wake. Ndio maana nilisema mkienda kwa uchaguzi mmangalie sana makamu, kwa sababu huenda ikawa yeye ndiye atakuwa rais wenu ikiwa rais atashindwa na kazi yake kabla muda wake haujaisha. Huyo makamu akiuchukua urais ataendelea kwa muda ambao umesalia. Kwa hivyo ikiwa rais aliondoka baada ya miaka miwili, hiyo miaka ingine mitatu tutaongozwa na makamu wake.

Ikiwa makamu kwa sababu yoyote atashindwa na hiyo kazi ya urais, basi ndio George alitueleza Speaker wa nyumba ile ya chini, atashikilia hiyo ofisi for a temporary basis ili tuweze kwenda kwa uchaguzi tena. Speaker wa nyumba ya chini akishindwa, basi Speaker wa nyumba ya juu lakini kutoka hapo bahati yetu sio mbaya sana, tunakomea hapo.

Tukienda kwa jambo lingine ambalo tumelipendekeza ni lile la ofisi ya Prime Minister. Tukasema ya kwamba tunapendekeza tuwe na Waziri Mkuu, Prime Minister. Na huyo Prime minister atakuwa akichaguliwa kutoka kwa chama ambacho kilipata viti vingi zaidi katika bunge. Kwa hivyo kutoka kwa kile chama ambacho kilipata viti vingi zaidi katika bunge, rais ndiye atakuwa na uwezo wa kumteuwa yule mkubwa wa kile chama awe ndiye Prime Minister ama Waziri Mkuu.



Waziri Mkuu akichaguliwa, naye anawateuwa manaibu wake wawili, deputy Prime Ministers ambao watafanya kazi pamoja naye. Pia huyo Prime Minister, Waziri Mkuu, ndiye atakuwa na uwezo wa kuwateuwa mawaziri, ministers kumi na watano. Na tuliambiwa ya kwamba wizara hazitazidi kumi na tano, a maximum of fifteen ministries na hazitakuwa mingi kuliko hizo.

Tena mawaziri, sijui hivi sasa tuko na mawaziri wangapi lakini ninajua ni wengi sana, sivyo. Sasa tunasema ya kwamba wizara zitakuwa kumi na tano na mawaziri pia watakuwa kumi na watano. Yaani wanaweza kuwa chini ya kumi na watano, ikiwa Prime Minister, Waziri Mkuu atapendelea aendelee na serikali ambayo iko na waziri watano, sawa hatumkatazi. Ikiwa anataka kumi, sawa lakini hana uwezo wa kuzidi kumi na watano.

Pia huyo Waziri mkuu atawateua manaibu wa waziri, deputy ministers. Na pia hao tumesema watakuwa kumi na watano. Hawatazidi kumi na tano, hiyo ndio maximum ya waziri manaibu.

Tukiondoka hapo tunaenda mambo ya Judiciary, chapter ya tisa. Tukiangalia mambo ya Judiciary, yale ambayo ni mapya hapo, na ndio maana mmevaa hizo baji za yellow, ni mambo kadhaa. La kwanza tunasema ya kwamba, tumeunda korti mpya ambayo hatukuwa nayo hapo mbeleni, na hiyo ni korti ya Supreme Court ambayo itakuwa ndio korti kubwa zaidi nchi. Lakini pia tukasema ya kwamba, kukija mambo ya wale ambao watateuliwa wawe majaji, tumesema ya kwamba yule ambaye atateuliwa, lazima awe amesomea sheria. Akasoma na akafuzu na degree ya kisheria. Hivi sasa, katika katiba tuliyonayo, unaweza kuteuliwa uwe jaji hata ingawa wewe hujasomea sheria.

Kuhusu miaka ya kustaafu ya majaji, katiba iliyoko sasa inasema wanastaafu wakiwa na miaka sabini na nne. Tukasema ya kwamba ipunguzwe ije mpaka sitini na tano. Kwa hivyo watakuwa wakipewa retire wakifikisha miaka sitini na tano.

Tukija kwa makorti ya Kiislamu, Kadhis court, yale mapya ambayo yako hapo ni kwamba tumeongeza korti za Kiislamu. Hivi sasa tuna korti kumi na mbili za Kiislamu na tumesema ziongezwe ziwe sitini na sita, (66) kwa sababu ilionekana kunahitajika hizo korti kwa sehemu mbali mbali nchini.

Jambo lingine ambalo ni jipya hapo, mkiangalia article 208, ibara ya mia mbili na nane,

Ukurasa ni ishirini na tano, page 25. Tunasema ya kwamba kuna ile ofisi ya Mkuu wa Sheria, Attorney General. Mkuu wa Sheria hivi sasa nchini kwetu ana kazi nyingi sana. Yeye huketi kwenye bunge akiwa kama ex-officio member, hiyo ni kazi moja. Kazi nyingine ni kwamba yeye ndiye hupa serikali mawaidha ya kisheria, legal advisor to the cabinet. Kazi ya tatu, yeye ndiye mwenye uwezo wa kuanzisha, kuendeleza na kumaliza kesi zote za criminal. Hata ikiwa mara nyingine anawatumia ma-agents hapa na pale, yeye ndiye mwenye uwezo huo wote.

Hizo ni kazi nyingi sana katika ofisi moja. Sisi tumependekeza ya kwamba tugawe hizo kazi. Ndipo tukasema ya kwamba tuwe na ofisi ya Director of Public Prosecution. Hiyo ofisi na ofisi zote ambazo tutazitaja za kikatiba, tumependekeza ya kwamba itakuwa ni ofisi ambayo ni huru. Huru kwa njia gani? Huru kumaanisha ya kwamba haitakuwa na uhusiano wowote na serikali, na wabunge, na majaji na kadhalika. Ofisi ambayo ni huru. Wale ambao watateuliwa kuketi kwenye hiyo ofisi, jina



linaproposiwa na rais, lakini hilo jina lazima lipitishwe kwenye bunge, ndio bunge isema kama ingependelea huyo mtu kweli aendelee kushikilia hicho kitu ama haijapendekeza.

Kwa hivyo ofisi ya kwanza ni hiyo ya Director of Public Prosecution. Na kazi yake itakuwa ni kuanzisha, kuendeleza na kumalizia kesi za criminal. Lakini tukasema ni ofisi huru na haina uhusiano wowote na serikali, imejisimamia yenyewe.

Ofisi ingine ambayo ni mpya katika hiyo section ya legal system ni ile ofisi ya Public Defender. Public Defender ni nani? Wanakenya wengi walisema ya kwamba gharama ya kupeleka kesi kortini eti ni kubwa sana. George, walisema hivyo, katika maoni yao, sivyo? Eti hiyo gharama ni kubwa, sinikubwa? Ukienda kule kortini, filing fees, kumlipa wakili na kadhalika.

Sasa tunasema ya kwamba kuna wale Wakenya ambao wanashida tofauti za kisheria, lakini hawana uwezo wa kifedha, yaani pesa za kuanzisha kesi zao. Hiyo ofisi ya Public Defender tumeiunda ikiwa ni ofisi ambayo imejisimamia yenyewe. Kazi ya hiyo ofisi ni hii, ikiwa Mwanakenya yeyote hana hiyo nguvu ya kuanzisha kesi yake, basi hiyo ofisi tumeipa uwezo wa kuajiri hata mawakili, na itaanzisha na hata kumaliza makesi na kadhalika, kwa niaba ya Mkenya ambaye hana uwezo.

### *Clapping from the audience*

Lakini, sio Wakenya wote bali ni yule ambaye imeonekana na imedhibitishwa kisheria ya kwamba anahitaji usaidizi. Na katika national budget itakuwa ikitenga pesa ambazo zinapewa Public Defender za kuanzisha na kuendeleza kesi kama hizo.

Kutoka hapo nitaenda kwa chapter ya kumi na moja, nimesema ninasisitiza yale ambayo ni ya muhimu. Chapter ya 11, kurasa ni la ishirini na nane, page 28, inaongea juu ya ardhi. Jambo la kwanza ambalo tumesema juu ya ardhi ni kuhusu mmiliki halali wa ardhi fulani. Hivi sasa sisi huketi tunasema ya kwamba mimi nina ardhi yangu pahali na niko na title deed yangu. Lakini kusema kweli, hivi sasa kulingana na katiba tuliyonayo sasa, ardhi yote ni mali ya nani? Ya serikali.

Sasa katika katiba, tumesema ardhi iwe ni mali ya Mwanakenya. Tunajua ya kwamba kuna Tume ambayo inaangalia sheria za ardhi sivyo? Tume ya Njonjo. Hiyo ni sentensi ambayo ni ya muhimu sana kwa sababu inasema sasa ardhi itakuwa mali ya Wanakenya. Kupitia hapo pia tukasema ya kwamba kuna wale ambao sio Wanakenya, na huwa wana ardhi nchini kwetu. Wengine tunasikia kwa mfano kule Coast Province, na hata huku Central na kwingineko, ya kwamba kuna watu ambao sio Wanakenya na wamepewa leasehold ya miaka mia nane, tisini na tisa, yaani miaka elfu moja kwa kifupi. Washikilie na waendelee kuitumia ardhi yetu.

Hapo tukasema ya kwamba, mtu ambaye sio raia wa Kenya, ndio, anahaki ya kuwa na ardhi, lakini hiyo haki yake itakuwa ya miaka tisini na tisa tu na haitazidi hapo. Ndio yale mambo ya mika mia tisa, tisini na tisa tumalize iwe mwisho ni miaka tisini na tisa. Kwa sababu tena tunaona ya kwamba kuna uwezekano huyo mtu ambaye sio raia wa Kenya aje atusaidie, ajenge kiwanda, atupatie kazi za kufanya na kadhalika. Lakini miaka yake tisini na tisa ikiisha, lease hold yake inaisha, na ardhi inarudi kwa Mwanakenya, raia wa Kenya ambaye ndiye mwenye ardhi.

Tena tukasema ya kwamba, tume-propose kubuniwe tume ambayo tumeita National Land Commission. Kwa kweli tulisikia mambo mengi kuhusu ardhi na mmesomewa yale ambayo mlisema kama watu wa Ndia kuhusu ardhi. Mambo ya ardhi ni mengi kutoka kila area ya Kenya na tukaona njia ya kuwasaidia Wanakenya ni kuunda tume ambayo inaitwa National Lands Commission. Tume hii itakuwa ikiangalia shida za ardhi. Ikiwa mtu alipokonywa ardhi yake miaka mitano iliyopita, miaka kumi au arobaini iliyopita, basi atakuwa na haki ya kujipeleka kwenye National Lands Commission na hilo jambo liangaliwe na litatuliwe. Kwa hivyo hiyo ni Tume ambayo tena imejisimamia yenyewe, yaani haina uhusiano na serikali.

Wanatume wa hiyo Commission, Lands Commission, watakuwa wakichaguliwa na rais, lakini majina yao yanapitishwa kwa bunge, ndio bunge ikiangalia hiyo orodha inasema huyu hatumtaki, huyu tunamtaka na kadhalika. Ili hiyo Tume iwe iko huru na haina interference kutoka kwa sehemu yoyote ya serikali.

Jambo lingine ambalo ningependa kusesitiza, nimesema tunaendelea tu kusesitiza ya kuhimu, chapter ya kumi na tatu ambayo iko kwa kurasa la ishirini na tisa, inaongea juu ya public finance, yaani pesa zetu ambazo tuko nazo, na tulipata maoni mengi kuhusu pesa. Kuhusu pesa tunapendekeza hivi: ya kwanza tunapendekeza ya kwamba pesa zote zitakuwa zikigawanywa katika sehemu zote nchini. Tumesema hapo mbeleni, serikali ije karibu na mwananchi ili tuwe na serikali mpaka kwa district.

Kwa hivyo pesa zikigawanywa, ziwe zinagawanywa sawa, kutoka kwa district moja hadi nyingine. Ili isiwe kwamba, district moja inaendelea tu na maendeleo na ile nyingine inabaki nyuma, ndio kila sehemu ya nchi iweze kuwa pamoja.

Tena katika article 249, tunaongea juu ya madeni yetu, yaani pesa ambazo tunaomba kutoka kwa nchi zingine au kutoka kwa organizations za kidunia. Hivi sasa tunajua ya kwamba tunaambiwa deni yetu ni kubwa sana, sivyo? Ninasikia ya kwamba kila Mkenya anadaiwa twenty thousand. Eti ile deni tuko nayo, kila Mkenya akiweza kutoa shilingi elfu ishirini, sisi sote tutaweza kuilipa na tutaisahau.

Sasa tumesemaje kuhusu kuombwa kwa pesa. Eti serikali ikipenda kuomba pesa kutoka nchi fulani au kutoka organization yoyote, serikali lazima kwanza ilete hilo pendekezo kwenye bunge. Ili bunge iangalie hilo pendekezo na iweze kuamua tupewe hizo pesa au la hizo pesa hazitatusaidia tusipewe. Tuko pamoja? Kwa hivyo tunasema pendekezo la kuomba pesa lazima lipitishwe bungeni ili wabunge wawe tayari wameangalia hizo pesa na wamesema aitha tupewe ama tusipewe.

Jambo lingine ni hili, tumependekeza ya kwamba kuundwe ofisi ingine ambayo tunaita ya Controller of the Budget. Hivi sasa tunaofisi ambayo tunajua inaitwa Auditor and Controller General, sivyo. Na kila wakati ukifika, huyo Auditor wa serikali huwa anatoa hesabu ya kuonyesha vile pesa zetu zilitumiwa. Hapa anatuambia tuliibiwa sana, pesa zilipotea na hapa hata ndio pabaya sana. Lakini hakuna ambalo tunaweza kufanya, tunasikitika tu kama Wakenya.

Sasa tunasema ya kwamba kuwe pia na ofisi ya Controller of Budget. Controller of Budget, kazi yake itakuwa ni hii, kila mwaka serikali ikiendelea kutumia pesa, Controller of Budget anaangalia vile ambavyo pesa inatumiwa. Ukumbuke, huyo Controller of Budget, kama ofisi zile zote ambazo tunapendekeza, ni ofisi ambayo ni huru kabisa. Hana uhusiano na serikali.

Kwa hivyo pesa zikitumika, anaangalia vile ambavyo zinatumiaka na anapendekeza hapa pengine mmetumia sana, hapa hamjagawa vizuri, na kadhalika.

Tena tunasema mwisho wa mwaka ukifika, naye Auditor General anazichukua zile hesabu, anaziangalia, na anatengeneza repoti yake. Tena huyo Auditor General tumeibuni ofisi yake upya iwe imejisimamia yenyewe, hana uhusiano na serikali. Anakuwa appointed na rais lakini, jina lazima liwe limepitishwa kwa bunge ili bunge iidhinishhe hiyo appointment. Kwa hivyo Auditor General mwisho wa mwaka anatengeneza repoti, anaipeleka kwa bunge.

Bunge tumeipatia miezi mitatu ijadili hiyo repoti. Ikijadili, inatengeneza mapendekezo kuhusu hiyo repoti. Kwa mfano ikiona afisa fulani alizitumia pesa vibaya au hata pengine aliziiba pesa za Wakenya, inakuwa pendekezo kwa Director of Public Prosecution, na kumbuka ni ofisi ambayo imejisimamia yenyewe, huyo Director anaandika kesi ya criminal na huyo mtu anastakiwa kortini. Kwa hivyo, hivyo ndivyo tumejaribu kuzilinda kikatiba pesa ama fedha za Wakenya.

Sasa ninataka tuendeleo kwa chapter ya 14, ambayo inahusu public service. Kurasa ni ya thelathini na mbili, page 32. Ukiangalia kwa sehemu hiyo, vile ambavyo tunasema ni hivi. Wanakenya walitoa malalamishi mengi, eti mimi nilienda kutafuata ID, eti mimi nilienda kutafuta passport, mwingine akasema ooh, nilienda kwa ofisi kutafuta title deed, nikaambiwa njoo kesho, nikaambiwa leta kitu kikubwa na kadhalika.

Sasa tunasema ya kwamba, maafisa wetu wa public, tunataka wawe na malengo ambayo watayafuata, na hayo tumeyaweka kwenye katiba. Professional ethics. Watu ambao hawana corruption, watu ambao wamefuzu kuifanya hiyo kazi ambao wamepewa elimu ambayo inafaa kufanya ile kazi ambayo wanaifanya na kadhalika.

Lakini pia ile commission ambayo inajihusisha na kuwaajiri maafisa wa public, kuwatoa kazini wakishindwa na kazi, kuwatia discipline ikiwa wamekosea, hiyo tume ambayo inaitwa Public Service Commission, tumeibuni upya kikatiba. Tukasema ya kwamba iwe imejisimamia yenyewe. Hivi sasa iko na uhusiano sana na serikali. Sasa tumesema iwe independent, huru kabisa.

Ili ikifikia mambo ya kuwaajiri Wanakenya, inaangalia nchini kote, na inawatafuta wale ambao kweli wamepata qualifications. Ikifika wakati wa kuwaondoa kazini, wakishindwa na kazi wanaondolewa haraka sana. Ikiwa ni discipline cases zinaangaliwa. Kwa hivyo independent Public Service Commission.

Area ingine ambayo kulingana na vile nilisikia asubuhi iliwatatiza watu wa Ndia sana ni ile ya Polisi. Mkiangalia article 264, tumesema kwanza tunataka kubadilisha kwa Kiingereza, kubadilisha jina ambalo tunatumia kutambua police yetu. Kwa Kiingereza huwa tunasema 'The Kenya Police Force' yaani ni kusema watumie nguvu zote ambazo wako nazo. Sasa tunasema tunataka tuiite 'The Kenya Police Service', yaani kutoa huduma, utumishi kwa wote. Na pia tukawawekea malengo ambayo watakuwa wakiyafuata na tukasema ya kwamba baada ya hii katiba kuwa ndio katiba yetu mpya, sheria zote ambazo zinahusu polisi, lazima zitabadilishwa kulingana na mapendekezo yetu na malengo ambayo tumeyaweka hapo yakiwa ni malengo ya area ya police service.

Pia mkuu wa Kenya Police Service, tumesema ya kwamba tunataka huyo mkubwa, the Commissioner of the Kenya Police Service awe na qualifications zifuatazo.

Ya kwanza, awe ni mtu ambaye amefanya kazi katika police service kwa miaka isiyopungua kumi ili awe anaelewa hiyo police service inafanya kazi kiviipi. Ya pili, awe ni mtu ambaye amechaguliwa na rais lakini jina likapitishwa kwa bunge, na bunge ndiyo iko na idhini na mwisho, the final approval inatolewa na bunge. Ya tatu awe amesoma mpaka akafika level ya university na akafuzu na degree, hatutaji ni gani lakini awe amesoma na akafuzu na degree.

La nne, awe ni mtu ambaye ataifanya hiyo kazi kwa miaka kumi tu. Yaani kwa Kiingereza tunasema his tenure will only be for ten years. Miaka kumi ikiisha, tutasema asante ameifanya kazi vizuri, na tutamteua mwingine awe Commissioner of the Police Service.

Jambo lingine ambalo tumependekeza ni kuhusu sehemu ya magereza. La kwanza tukasema tubadilisha jina ya sehemu hiyo ya magereza. Hivi sasa tunasema prisons, yaani magereza, tunawatupa watu huko, tunawasahau, wanafungiwa, wengine vifungu vya maisha na wengine kwa muda. Sasa tunataka tuiite, sio prisons, yaani kuwafungia tu, ni kujaribu kuwarekebisha, ndio warudi tena waendeleo na kazi ya kujenga taifa. Kwa hivyo tunasema tuwe tukiita the Kenya Correctional Services. Yaani, kazi yetu kama Kenya Correctional Services itakuwa kurekebisha tabia za wale ambao wamepelekwa kwenye area hiyo. Tena tukasema yule director of Correctional Services, pia jina lake linateuliwa na rais na pia linapelekwa kwenye bunge, ndio bunge inatoa idhini ya mwisho.

Chapter ya 15, kurasa ni la thelathini na tatu, page 33 inaongea juu ya the Defence Forces, yaani ile ambayo sasa tunaitambua kuwa Armed Forces. Hapo hatubadilishi jina, bado wataendelea kuitwa Defence Force kwa sababu hawa ndio wanajeshi ambao wanalinda nchi yetu ikiwa tunasumbuliwa na yeyote. Awe ni *Al Qaeda* au ni mtu gani yeyote yule, tunasema tunawatuma huko waende na nguvu zote, ndio wawalinde Wanakenya.

Lakini kama vile tulivyoielezwa na George, tumbuni council ambayo tunaita National Security Council ambayo itakuwa ikiketi na rais kujadiliana mambo ambayo ni ya muhimu kuhusu wanajeshi wetu. Kwa mfano, itawatuma wananchi waende nchi jirani wakasaidie pahali ambapo kuna matatizo ama kwa wakati huu tunataka waende pengine kule North Eastern tunasikia kuna mambo fulani, fulani yanahitajika na kadhalika. Kwa hivyo tunasema mambo ya kijeshi tutakuwa na National Security Council ambayo itakuwa ikiangalia maswala ya kijeshi pamoja na rais wa nchi yetu.

Nikiendelea kwa chapter ya kumi na saba, inahusu tume ambazo tumependekeza ziundwe kikatiba, Constitutional Commissions. Vile ambavyo nilitaja hapo mbeleni, hizi ni tume ambazo ni huru, hazina uhusiano na serikali, na bunge, na majaji, ziko huru na watu ambao wataketi kwenye hizo Tume wanachaguliwa na rais lakini majina lazima yapitishwe bungeni ndio kutolewe idhini kama ndio wataendelea kuwa wanatume. Kwa hivyo ni tume ambazo ni huru.

Hizi Tume, sababu ya kuziunda ni kwa sababu ya malalamishi mengi ambayo tulisikia kutoka kwa wananchi. Ya kwanza na ile

ambayo tunaita kwa Kiingereza, the Commission on Human Rights and Administrative Justice. Yaani Tume ya kuziangalia haki zako kama Mwanakenya. Hiyo Tume ni ya muhimu sana, huwa ninasema hata ukizisahau Tume zile zingine, usiisahau hiyo kwa sababu hiyo tumeiunda ikiwa yako wewe Mwanakenya kabisa.

Ikiwa haki yako itapokonywa na mtu yeyote, utakuwa na haki ya kukimbia kwenye Commission of Human Rights, Tume ya Haki Zako, na utoe malalamishi, yaangaliwe na kurekebishwe mahali ambapo mambo yalikuwa yameenda vibaya. Ndio maana tunasema hiyo ni Tume yako. Hiyo Tume tumependekeza ya kwamba, itakuwa na branches mpaka kwa district level. Sio ati utakuwa ukikimbia kwa provincial headquarter ama kule Nairobi kuwasilisha malalamishi ati umepokonywa haki, la. Tumesema kila district itakuwa na ofisi ya Commission of human Rights ndio haki yako ikipokonywa na mtu yeyote unakimbia huko.

Haki ni kama gani? Kwa mfano, ikiwa wewe unadisability, umepokonywa haki yako, kimbia huko. Ikiwa wewe ni mtoto na haki yako ya kikatiba imepokonya, unakimbia huko. Ikiwa umeenda kuajiriwa na ukaambiwa hutapewa hiyo kazi kwa sababu wewe pengine ni mweupe au mweusi, au ni wa dini fulani au kuwa wewe ni kabila fulani ama ingine, kimbia huko, hiyo ndio Tume ya kuangalia haki zako.

Tume ingine ambayo tume-propose, ni ile ambayo ni ya Ethics and Integrity. Wanakenya wengi walisema na tumeambiwa hata nyinyi watu wa Ndia, wanataka viongozi ambao wanatabia hii, ambao wanafanya kazi hivi, na kadhalika. Sasa kulingana na hayo maoni, tukasema kuwe na Ethics and Integrity Commission. Kazi ya hiyo Tume ni gani?

Ya kwanza, ikiwa wewe ni raia wa Kenya na umemwona kiongozi ambaye ametenda jambo ambalo sio la kisheria au la kikatiba, kwa mfano ameitisha hongo na kadhalika, utakuwa na uwezo wa kukimbia kwenye Ethics and Integrity Commission, unatoa malalamishi, investigations inanza. Ikipatikana kwamba ni kweli huyo kiongozi aitha hafanyi kazi yake yeye huketi tu kwa ofisi, ama anaacha tu koti kwa ofisi anaenda zake, basi ataweza kuondolewa kwa hiyo ofisi.

Jambo la pili ambalo ni la muhimu na tulielezwa na George asubuhi, yeyote ambaye atachaguliwa awe kiongozi, iwe ni rais, iwe ni Prime Minister, iwe ni waziri, naibu wa waziri, Permanent secretary, deputy secretary, au kama ni mwanabunge, basi huyo atakuwa akienda kabla hajakuala kiapo anaenda anatoa orodha ya mali yake. Yaani kusema mimi nimechaguliwa niwe rais wa Kenya, kabla sijakua kiapo, ninaenda kwa Ethics and Integrity Commission, ninasema ya kwamba mimi nina nyumba nne na nilizipata kwa njia fulani. Pia niko na magari mawili na niliyapata kwa njia fulani, ili tuweze kujua viongozi wetu wametoa mali yao wapi.

Na ikiwa huyo kiongozi ataanguka huo mtihani, basi hatakula kiapo, tuatamtafuta mwingine. Kila baada ya miaka mine na huyo kiongozi bado ako ofisini, miaka mine ikiisha, kama ni rais anaenda anasema basi miaka minne imeisha, bado niko ofisini kama rais, hiyo miaka minne iliyopita pia nimenunua ka-plot kengine na niliinunua kwa njia hii. Tena nikanunua nyumba mbili nikanunua kwa njia hii, orodha ya mali. Lakini sio mali yake tu, anatoa orodha ya mali yake, orodha ya mali ya bibi ama bwana yake na pia orodha ya mali ya watoto wake ambao hawajaoa.

Maana ni kwa sababu, wengine watakwambia hawana mali lakini ukiangalia vizuri yote ameiweka kwa bibi ama bwana yake. Kwa hivyo lazima yote ya kiongozi, ya bibi au bwana yake na watoto ambao hawajaolewa, orodha lazima ipelekwe kwa Ethics and Integrity Commission. Sio rahisi kuwa kiongozi sasa, eh, ni ngumu.

Tume nyingine ambayo tunaipendekeza ni ile ya Salaries na Remuneration. Yaani Tume ambayo itaangalia mishahara. Hivi sasa tunajua tuna crisis ambayo inahusu mishahara ya waalimu. Na tunapendekeza ya kwamba, na tulifanya research, tukaangalia na tukafanya research ya migomo ambayo tumekuwa nayo, ya madaktari, waalimu wa university, waalimu, civil aviation na kadhalika. Tumependekeza ya kwamba, na pia tukaambiwa na Wanakenya wengine, kwamba kuna watu ambao huketi na wanajiongezea mishahara, hivyo ndivyo Wanakenya walisema sio mimi.

Kufikia hapo tukasema ya kwamba, sisi tumependekeza kuwe na Salaries na Remuneration Commission, Tume ambayo itakuwa ikiangalia mishahara ya public servants wote. Yaani kuanzia president, Prime Minister wanabunge, wale ambao wanafanya kazi katika wizara, wale ambao wanafanya kazi ya public, hata karani ambaye anafanya kazi katika wizara fulani na kadhalika, mishahara benefits na pia pension zitakuwa zikiangaliwa na kuwekwa na hiyo Tume ya kuangalia mishahara. Kwa hivyo uwezo wa kijiongezea mishahara utakuwa umetolewa. Hiyo Commission ambayo ni huru ndio itakuwa ikiangalia mishahara ya watu wote.

Tena tukasema ya kwamba Teachers Service Commission ambayo hivi sasa iko katika Act ambayo inaitwa Teachers Service Commission Act, sasa tumesema ipewe status ya kuwa ni Tume ya katiba. Ili pia iweze kuwa ni huru na haina uhusiano na serikali, na bunge au chochote kile. Kwa hivyo hiyo ni Teachers Service Commission.

Tume ya mwisho ambayo ni ya muhimu zaidi, ni ile ambayo tunaita Constitutional Commission. Hiyo Tume uwezo wake ni huu. Katika hii draft kuna mapendekezo mengi sana, mengine nimeyataja leo na mengine hatuwezi kuyataja kwa sababu ya muda ambao tuko nao. Lakini hayo mapendekezo yote, hatutaki eti hii katiba ikiwa ndio sheria yalale tu. Ati tuwe tukisikia kwa katiba tunasema tuna Commission on Human rights lakini ukienda kwa district huoni kwa sababu haijawahi kubuniwa.

Tunasema ya kwamba Constitution Commission, tume-i-propose ndio itaangalia na ihakikishe ya kwamba miaka tatu baada ya hii katiba kuwa sheria, kila jambo ambalo limeahidiwa raia wa Kenya, litakuwa limetendwa. Ili hii katiba isiwe kwamba tumefanya kazi halafu iende ikalale tu kwa ma-shelves. Ionekane ya kwamba kila kitu kimetendwa baada ya miaka mitatu.

Jambo lingine la muhimu ambalo pia liliguziwa hapo mbeleni ni lile la kuibadilisha katiba. Ukiiona katiba ambayo tulipewa wakati wa independence, wakati wa Uhuru, ukiangalia hiyo katiba halafu ulinganishe na katiba ambayo tuko nayo sasa, ambayo ni hiyo hiyo tu lakini imeendelea kufanyiwa mabadiliko, huwezi kusema zimetoka pahali pamoja. Hii ni kwa sababu ile katiba yetu ya Uhuru, the independence Constitution, kama umeisoma utaona imebadilishwa. Karibu kila sehemu imebadilishwa.

Sasa Wanakenya wengi waliuliza baada ya kuiunda hii katiba tumetumia pesa, wakati, na nguvu itaenda kule ibadilishwe halafu

tena iwe sio kazi ya mwananchi. Ndio maana tukasema tuilinde katiba yetu kikatiba ili njia ya kuibadilisha iwe ni ngumu. Kwanza tumesema kuna sehemu ambazo ni muhimu kabisa, na ukiangalia article 294, kurasa bado ni 36, mtaona ya kwamba kuna sehemu ambazo tumesema ni za muhimu sana na hizo sehemu kama zitabadilishwa, lazima hilo swala lirudishiwe wananchi, waelezwe, na wapate kujua ya kwamba hii ni sehemu inahitajika kubadilishwa. Tena wapewe muda wa kupiga kura waamue kama wanataka ibadilishwe au isibadilishwe. Hiyo ni ile tunaita kwa Kiingereza national referendum.

Kwa hivyo tumesema sehemu kama zile ambazo zinatambua nchi yetu, the territory of Kenya, sehemu ambazo zinamtambua Mwanakenya kuwa ndiye mwenye nguvu zaidi, sehemu kama zile zinazotambua haki zetu, sehemu ambazo zinasema ni nani anaweza kuwa raia wa Kenya, na zinginezo. Hizo sehemu tunasema ni muhimu sana kwa Mwanakenya na ikiwa zitabadilishwa, basi lazima hilo swala lirudishiwe Mwanakenya. Yaani lazima tutarudi hapa tuje tuelezwe katika Ndia Constituency, wanataka kubadilisha nini, kwa nini halafu tuilizwe na tupige kura. Tuko pamoja? Hizo ni zile sehemu za muhimu.

Kuna sehemu zingine ambazo tumepatia bunge uwezo wa kubadilisha, na njia ya kubadilisha ni hii. Hiyo motion ikianzishwa kwenye bunge, itapitia kwanza kwenye ile bunge ya chini, itasomwa mara ya kwanza, ikisomwa mara ya pili watapiga kura. Ikiwa asili mia sitini na sita wa hiyo nyumba ya chini watapendekeza kubadilishwe basi, hiyo motion itaendelea. Isomwe mara ya tatu, baada ya hiyo tena wapige kura na ikiwa asili mia sitini na sita watakubali, iendele. Kisha itaelekea kwa ile nyumba ya pili, ifuate hiyo process tena, isomwe mara ya kwanza, ya pili, ya tatu, wapige kura na kadhalika. Hiyo kweli ni njia rahisi? Ni njia ambayo ni ngumu kidogo kuliko ile ambayo tulikuwa nayo.

Hivi sasa, ikisomwa tu kwa bunge na asili mia sitini na sita wakubali, katiba imebadilika na ni kwa sababu hiyo tumekuwa na mabadiliko mengi sana. Kwa hivyo tumejaribu kuulinda katiba ndio isiwe inabadilishwa ovyo ovyo ili iwe ni katiba yako wewe mwananchi.

Kwa hivyo ninafikiria nitakomea hapo. Nilisema ni siku yenu sio siku yetu, mpate nafasi pengine ya kutoa comments. Hizo comments ambazo mtatoa ni kuhusu draft, yaani ikiwa kuna sehemu ambayo pengine unaona ni bora unaweza kusema na ikiwa kunasehemu ambayo unaona haiukufurahishi, tafadhali utueleze. Ikiwa unaona kuna sehemu ambayo tulisahau kabisa, tueleze. Tutaandika tukisaidiana pamoja na George na Josephine yuko hapa anarecodi. Sauti yako itakuwa hapa ndani na tutaenda hata kukusikilia tukiwa kule Nairobi ndio tuweze kuyasikiliza maoni yenu kuhusu hiyo draft. Kwa hivyo tunasema asante, mmekuwa watulivu mmesikiliza na mmeona kwa kweli mmeielewa katiba yenu. Asanteni.

### *Clapping from the audience*

**Mercy Njoka:** Asanteni sana kwa yale mmetueleza. Kwanza ningependa kumshukuru Madam Gichanji kwa sababu ametuelimisha sawa sawa, sindio? Sasa ninauhakika ya kwamba kila mmoja wenu akiulizwa nini kiko kwa draft Constitution anaweza kuelezea vizuri. Hapo mbeleni mtu angekuwa amevaa hii yellow ribbon tumevaa na akiulizwa anaivaa kwa nini, wengine hawangejua ni kwa nini tunaivaa. Baada ya leo ninatumahi tukitoka hapa tutaenda tukihubiri mambo yote ambayo tumefunzwa na tutaenda kuwaeleza wale ambao tumewaacha nyumbani kuwa kwa kweli hii Constitution ni yetu, ni sisi tulipeana



maoni na kwa hivyo ni lazima tuilinda.

Kwa wakati huu sitaki kuchukua muda mrefu, nitawapatia nafasii hii ili muweze kuuliza maswali na pia mtoe maoni yenu. Kabla ya hiyo nitampatia Bwana George fursa hii ili aweze kusema maneno machache halafu tutaweza kuendelea na maswali. George.

**George Wachira:** Asante sana kwa kunipatia tena muda huu kuongea na nyinyi na ninatumaini ya kuwa mtakuwa mmenielewa katiba hii vizuri. Hapa nimeona kuna watu wengi sana, in fact kote tumeenda over the past two weeks hatujaona watu wamefika wengi vile mko hapa. Kwa hivyo asanteni sana kwa kufika.

Pia ninajua kuna wengi sana hawajafika leo kwa maana hiyo ningetaka kusema mmefundishwa vizuri, na yule amewafundisha vizuri ni wakili na tena ni mwalimu wa sheria. Mimi pia nimefunzwa sheria na yeye alikuwa mmoja wa wale waalimu walionifunza sheria. (*Clapping from the audience*) Na alinuliza leo, kwa vile alinifunza nije hapa leo nimsaidie kuwafunza watu sheria, kwa hivyo vile amewafunza, mmekuwa kama wanasheria pia. Kwa hivyo mnaweza kuwafunza wale ambao hawajafika leo ili wajue hii Constitution yetu vile imesema. Kwa vile watu wengi wamedanganywa, wengi hawajaambiwa ukweli. Nyinyi mmeambiwa ukweli na kile hamjajua mtauliza maswali. Kama nimewaambia yeye ni mwalimu wa sheria hivyo basi anajua kujibu maswali vizuri. Asante sana.

### *Clapping from the audience*

**Mercy Njoka:** Asanteni sana. Sasa tutaendelea na watu wote ambao wako na maswali. Tutakuwa tunachukua maswali na maoni yenu kama matano hivi, halafu tutampatia mwalimu wetu nafasi ya kujibu halafu tutaendelea hivyo. Ninawahakikishia ya kwamba kila mtu ambaye ako na swali, tutampatia nafasi ya kuuliza na tutaendelea hivyo. Kwa hivyo tutachukua maswali ya kwanza matano. One, two, three, four na upande huu five.

Okay, as you do that, lazima utambie jina lako kwa sababu tuna-record. Tutaanzia hapa kwa number one. You can ask as many questions as you want.

**Joseph Kimiti:** Thank you very much. Jina langu ni Joseph Kimiti. Swali langu ni kuhusu historia ya nchi hii. Katika preamble ya hii draft Constitution sikuona chochote kinagusia kupigania Uhuru, ati kulikuwa na Mau mau na hawa watu wangestahili kuandikwa kwa hii draft.

Swali langu la pili ni kuhusu uraia wa Kenya. Huu uraia wa kuo, ninaona ni rahisi sana. Mtu anaweza kutoka ng'ambo anakuja anamwoa mwanamke wa Kenya, anakaa naye miaka tatu na anakuwa raia wa Kenya. Na hii draft haijatueleza ni nani anaoa. Unajua kuna watu wengi hata huko America, kuna homosexuals! Hao wakitoka huko waowane hapa wanaume kwa wanaume, hiyo tunaikubali hapa kweli?

Ya tatu, ni uraia wa naturalization nimeona hapa imeandikwa miaka saba. Mtu anajiandikisha na baada ya miaka saba anakuwa raia wa Kenya. Hata hiyo tena ni rahisi sana. Anatakiwa akae hapa kama miaka kumi na tano au ishirini. Sio mtu anakuja



hapa anakaa hivi na hivi na anakuwa raia. Kwa hivyo hiyo draft mkiangalia, mkienda kwa Conference, angaliene hayo mambo.

Hayo mambo ya Bill of Rights kwa children, nimeona hapo corporal punishment not for children. Sasa hii corporal punishment hata kwangu nyumbani nikichukua kiboko ni vibaya? Tuambie kwa hii draft Constituion habari ya hiyo corporal punishment.

Kuna haya mambo ya food, kila mtu ako na haki ya chakula, hata yule anakaa nyumbani analala tu? Draft haijatuambia kama hata yule ambaye hafanyi kazi atapatiwa chakula, imeandikwa tu hunger. Sasa hiyo pia iangaliwe pia kwa sababu hatutaki kuwa na watu ambao hawafanyi kazi.

Kuhusu devolution of power, tumeona iko na Village Council, Locational Council na District Council. Hii ni nzuri sana. Lakini draft itupatie guidelines, who qualifies to be elected to the Village Council. Tuwe na guideline kidogo kwa sababu tukiiweka namna hiyo tu, iandikwe hivyo kutakuwa na shida baadaye. Nitakomea hapo, nitarudi nikiona kitu kingine. Asante sana.

### *Clapping from the audience*

**Mercy Njoka:** Asante sana. Muwe mnayasikiliza hayo maswali vizuri ili mtu akija kuuliza, usirudie ile ambayo imeulizwa tayari.

**Dr Marion Mutugi:** *Nindamugeithia muriega, nii nguria na Gikuyu. Njitagwo Dr. Marion Mutugi na nii ndiretia giti kia Bunge kia Ndia. Ndirenda kwamba gucokeria Commission ngaatho niundu nitumuiguite muno na mwari haha na tukimwira Maundu maria tuendire na nimo mwikirite ho. Niwega niundu wa guthikiriria. Ndirenda kuuga atiriri, ati turenda guthii ithurano na Constitution iria njeru niundu wa riri, korwo ni Constitution iria njeru twinayori, tutingiikarite na ihoru riria twina rio. Niundu ona umuthi, tuetereire no tuigue ati Parliament ni ya dissolvwo tuitike githurano. Korwo niyo twinayo riu ri, hatingiri kiuria kiu ati ni ri, githurano nitungiramenya. Hau hangi, mawatho ma President uguo Constitution iyo njeru yugite no matinatinio. Matinatinio atiriri, ta riu tutiri na President, President angiona uria angiona tondu ni mwanadamu ta nii kana ta we, tungiikara ta ciana itari na mwana. Ikorwo ni Constitution iria njeru twinayori, nitungiramenya mundu uria wiha. Kiu kingi, hena undu mwatugwetera haha wina bata muno, uroiga ati, Constitution iyo njeru iroiga mundu wa Kenya wothe na ngwiciria nihagwetirwo ni mundu nohatinakindirwo, ati Mukenya wothe ena rutha to disobey, unlawful instructions. Ati ungiheo, wirwo wike undu, urona undu ucio nduagiriire no ureka. Ukorwo ni watho ucio twinaguo riu, ri borithi iria irahura andu guku ri noihure andu? Noirege ciuge, that is unlawful instruction. Hau hangi ni undu ucio wa gutuika President akirugama ekurugama na running mate, tumenye ati ni team turathura ti mundu, nigetha tukamenya nitugitirwo. Angiehera ri, uyu nieguthii na mbere na athii na mbere kinya miaka iria itano ithire. Kwoguo tuguikara twina confidence, tuguikara twina stability. Tutiguikara na wasiwasi. Riu ndirenda kuria atiriri, niundu ithui tungienda tuitike githurano na Constitution njeru na Commission muthii mwire Prof. Ghai ati niatukenetie. Niatukenetie.*

### *Clapping from the audience.*

**Dr Marion Mutugi:** *Niundu arutite wira mwega ona inyui nimurutite wira mwega na nikiu tuikirite tunyamu tutu. Tukoiga atiriri, mundu aheo wira, niarekererio arute, niatige ku-interfere nake. Riu turenda kuuga atiriri, turikanire haha, tigucira turacira. Turikanire haha. Umuthi uyu tungirwo tuitike githurano Constitution njeru itari iroima ri, tuguika atia? Nituaiguanira uguo?*

**Audience:** *Ii*

**Dr Marion Mutugi:** *Twarie giki kimwe ati nituarega niundu Constitution iria njeru ni iyo igutugitira ona tugithurana noyo igutugitira. Kwoguo twerwo tuthii githurano ini iyo njeru itoimite turege. Kiuria ni atiriri, tukurega atia, atungatiri, mundu wothe ndirona wina collar, wina collar tuiguanire. Atungatiri tuiguanire ati twerwo tuitike githurano na Constitution iria nguru ona inyui nimukurega. Ona inyui nimirite kanyamu gaka ka yellow na okorwo ni warega, ukarute tumenye niwarega.*

**Clapping from the audience.**

**Dr Marion Mutugi:** *Turoiga atiriri ati we na nii twerwo wiharirie na tuona uguo ni guthii kurathii, tukurehe maratathi guku tuikire signature na tukungania signature one million, milioni imwe. Ati gwatuika ati ni tukuirwo tuthii githuranoini na Constitution iria nguru, tuikire kiore ati nituarega. Na iria nguru, nituarega. Tuiguanire uguo. Nituaiguana?*

**Audience:** *Ii.*

**Dr Marion Mutugi:** *Marega ri, tugucoka twike atia, nonginya twarie giki? Niguo? Constitution iyo twerwo ni chaguo la mwanachi, mwananchi nuu? Tuiguanire. Ati gwatuika ati tuguthii githurano na Constitution iria nguru, twaritie uguo twarie, aya marutite wira uyu muritu wa thithino merwo wira ucio ni wa tuhu, tuiguanire uria tugwika. Tu-demonstrate turege.*

*Hau hangi, kaundu kanjiguithia uru nita muthuri uyu uria agweta, ati national holidays nicianyihanyihio. Niwega Jamhuri day na Madaraka day na hau nindirona uria mararega niundu wa Kenyatta day, Moi day uria uguka nake yake. Turigitindaga tuhurukite, wira tutikarute. No riu turoiga atiriri, niundu Kenyatta ni karia gaitu. Niguo? Kenyatta day icoke.*

**Clapping from the audience.**

**Dr Marion Mutugi:** *Niundu Kenyatta day yaga gucoka ri, tukuriganirwo ati nituaruire wiyathi na munyite tuariganirwo ati nituaruire uhuru, mumenye Gikuyu ni ithui turahurwo niundu ni ithui tuaruire ki? Kenyatta day, icoke. Andika hau. Icio ingi nicikare.*

*Undu ucio ungi ni the right to own land. Uhoro ucio wa gutuika ati Mwanakenya o wothe no uthii kuria wathii ugure*

ki? Mugunda. Niguo? Ucio ni undu mweka no turenda kumuria atiriri, aria mari na migunda Molo magitunywo ri, hau muroiga atia? Niundu muoiga kuuma umuthi no ngure mugunda haria ngugura ri, aria magurite magitunywo, naho hau muroiga atia? Nikumoria turamoria niundu tutinaigua.

Ha muico ni hau mwaageta ati nihekugia na Kadhi's court. Rekei ndimutaririe Kadhi's Court ni kuuga atia. Ati kwina igoti riria tuthiaga Barichu. Niguo? Mundu arikiya agatuarwo Barichu. Haha Constitution na mututaririe, murenda gutuira atiriri, kwina igoti ringi mwa-recognize ria ithiramu na ni wega ni Wanakenya. Turenda mutuire atiriri, aithiramu mena percentage igana atia nigetha mumathondekere igoti riao ria mwanya na tucoke turihage na mbecha ciitu. Tukariha acio maramacirithia na mbecha ciitu. Kai mena percentage igana atia. Njoke njurie atiriri, nikuria turoria, niguo? Githi mutiatuira turie ciuria. Mabururi maria manathondeka Kadhi's court. Kadhi's court ikagia na hinya, macokaga magakinyukia ikinya ringi makoiga ni Sheria law ta Nigeria. Makoiga ni Sheria law. Turenda kuria atiriri, tuekira hinya ithiramu, magie na magoti mao ri, moke haha Kibirigwi moige haha ni andu aingi mekire sheria ri, na ithi tutigutininio moko. Okorwo ni muguthondeka igoti ria ithiramu, mucoke mucarie ringi tuthondeke ria Akristiano niundu twina mathani ikumi tucirage namo.

### ***Clapping from the audience.***

**Dr Marion Mutugi:** Mwena uyu ungi, tikuaria turaria, kwaria tikwendana? Mwena uyu ungi tucoke tuthondeke igoti ria Hindu niundu onao mena mawatho mao. Mwena uyu ungi tucoke tuthondeke igoti ria aria metagwo animists, andu aria mahoyaga miti na mahiga. Nao mathondekerwo riao, no igoti rituika ni riri, rimwe. Gutigatuika kuri andu maheo igoti riao.

### ***Clapping from the audience***

Mercy Njoka: Thank you very much, : Thank you very much. Niwega nitondu wa Maundu macio mothe woiga. (*Murmuring from the audience*) Ke tukorwo twi bamwe. Tuwe pamoja ili tuweze kuelewana. Ebu tuwe pamoja tafadahali ili tuweze kuelewana.

**Wajohi Kavuitu:** Thank you very much aria mokite niundu wa uhoro wa Katiba na njuge ati; ndaigua aria megutuaragiria haha mena githweri kiria gitagwo Githweri sanifu. Nii ndi mwarimu no Githweri kiu menakio ndingihota kunyitana na kio. No ninguarua na Gikuyu. Njarie na Gikuyu tondu hihi Githweri ti kiega muno. Githungu nonjarie wega makiria no nguarua na Gikuyu. Ritwa riakwa ni Wanjohi wa Kavuitu na ngoragwo ngirutira wira kuria K.T.I ndi registrar. Hau hangi ningwenda kuheana maoni makwa uria ndaigua uhoro wa Katiba. Maundu mamwe ni Mario, maria mangi ninguthiite through document iria iraririo. Uhoro wa mbere ni ucio wa Chapter two, nindaigua mwaria uria uma mbere yakwa agweta uhoro wa Kenyatta day no ningwendaga tunyitanire hanini muno tondu tuarehe ritwa Kenyatta day, riahota kurehe Maundu mangi na nitui wega to Kenyatta wiki waruire wiyathi, ni andu aingi maruire wiyathi na monete uhoro ucio unyitanirwo witwo ta Freedom Heroes day nigetha tuma-recognize. Icio ingi national days

*ninguonaga niciagiriire o uguo ciigitwo no ningunyitanira na Katiba day, Katiba day tumenye ni muthenya umwe tuagirirwo ni kuririkanaga tondu ino ni tayo tungiuga second liberation, kunyita wiyathi ungi wa keru.*

*Hau hangi nigukugwetetwo uhoro wa citizenship na ninyonire kana uria Katiba iroiga ati mundu no atuike citizen arikia kuhikania na anina miaka ta itatu, ngona miaka iyo ni minini muno na nigetha atuike citizen tuhote kumuona makiria. Hau hangi ni uhoro ukonie presentation of people. Ni kaundu karia kagwetetwo ka uhoro wa kiwango gia gatatu kia atumia maheagwo maoni. Hau ninguona he na hinya maheagwo, iti iria ciaguthurwo. Ninguona hari hinya hanini tondu nonginya atumia onao merute monekane nimarenda iti icio, riria merutite hihi kaundu kau nokanyitanirwo no matakirutite ri, ndiui uria hau harithiaga. Eruta ta uyu wi haha na nimwaria mweka ucio riu niundu ungi. Hau hangi ndaigua he hega uhoro wa political parties kuheagwo tubeca nigetha ikahota kwirugamirira uhoro wigie ithurano. Niundu ithui nituim kuuma kahinda kanene ati hihi kiama kiria gikoretwo gigiathana, rimwe nikihuthagira indo cia thirikari, ringi gwiteithia riria ciama iria ingi, igukorwo ikihuthira mbia ciao. Na hau hagagikorwo na hinya makiria. Hau nindona he hega muno. Riu haria hangi ndi mwarimu, nondimucokerie ngaatho niundu wa Teachers Service Commission. Nimui Teachers Service Commission ni ikoragwo ikinyita uhoro ukonie arutani. Kwoguo igiitwo iri kando ga thirikari handu ha ikorwo I hana uria ihana igakoragwo iri under Ministry of Education. Niirihotaga gukorwo ina hinya nigetha hihi Minister ta uria ugaga uguo gutiguikika, agakoragwo akimenya ati, hau ndangiingirira tondu Teachers Service Commission niyugite hau ni hega muno.*

### **Clapping from the audience.**

*Hari hangi hatanengenia muno Constitution ni uhoro wa gukorwo na Bunge ta igiri, hena national council na national assembly. Hari nii mwene nindirona, tungigia Bunge igiri, twahota ku-politicize bururi muno. Tondu ni siasa na tuahota gukorwo na siasa nyingi muno no nguna iri national assembly o imwe iria tugukorwo na MP aitu magathiiaga mari hamwe, corner imwe iyo ta ingiiganira.*

*Ningi haria hangi haragueta uhoro wa ninety people marathurwo kiundu gitari straightforward. Nii ninguonaga tondu President arerwo ndari na powers. No kuringana na uria turarora Constitution ino, President ena powers nyingi muno. Ena powers njega no ninguona no aheo powers kidogo handu ha acio ninety tuma-reduce tuoige ota nominated members aria mari ho. No tuongerere kuuma twelve tumekire thirty nigetha haria nguguetaga uhoro wa atumia materutite guthurwo, tuhe one third ya acio thirty nominated MPs. One third iyo ikorwo iri atumia nayo one third megukorwo mari ikumi atumia. Nayo iria ingi one third ikumi, makorwo mari people representing special interests. Makorwo nao mari ikumi nao aya angi megukorwo mari ikumi, riu nake President. He handu nguandikite reke ndiharore. Nao aya angi ikumi makorwo me andu aria meku-represent people with disability. Andu with disability. Kwoguo turoiga ikumi atumia, ikumi with disability na ikumi ma-represent special groups including the marginalized lots. Nitui kuri andu makoragwo na kuria Turkana tuiguaga ni kunyiha maranyiha handu maingihe, riu nomaingirire*

*handu ta hau. Na aya maka-nominatagwo ni President. No nake President no nginya a-make sure nima-approve ni Parliament guthuraga andu ake aria ekwenda.*

*Haria hangi hatanangenia ndi murutani nii ni uhoro wa kuigua ati, tukagwetataga ati mundu uria uguthii Bunge agathuragwo na certificate ya form four ina pass. Constitution ndiroiga pass ni ki, nitui hari mundu urendaga kurmama Bunge Mombasa. Na niarathiire na areka xkigernaio n ena certificate riu turoia uguo no certificate iyo tutiui kana ni pass kana ni fail. Nokuringana na uria njuu uhoro wa kigeranio, nonginya tuge ta K.C.S.E mean grade D + no ti less than D +. Tond u D+ mundu ta ucio niekuhota kwiyaririria na Githungu na ahote kwaria Githweri kiega. Ona Sanifu ta kia mundu witu ugwitwo Wachira. Nindakenio ni uhoro wa Constitution ya kugaga ati; no kinya tukamenyaga riria ithurano irathuranwo niundu wa kindu gitagwo secret weapon. Ta America nitui kuuma 1789, ithurano ituraga ciikagwo twentieth November after every four years. Na riu Kenya tungimenya uguo niturikoragwo twina mubango mweka na tukeharagiriria muturiireini witu tukimenyaga ithurano igathuranwo hindi ina. Hau ni hega muno.*

*Haria hangi ni uhoro wa by-election. Ndiroiga ikagwo by elections, itigekagwo three months of holding a general election. Ngwiciria riu haha mararoraga niundu wa defections. No case hihi mundu akuite within three months ona okorwo ni rio elections irekwo. Niagiriirwo agathurwo. Reke ndigire hau no itarikiriirie biu reke ngwete uhoro wa appointment of Judges. Ino ni issue itureheire thina bururi. Judge nimui, ona elder Gikuyu, endaga mundu Mukuru Mukuru, na riu haha ha sixty five kuringana na nii woni wakwa, ingienda onayo yume haria seventy four, ikinye seventy five, maximum years. Tond u nitukwenda mundu wise. Na aria muthomangite nimoi kuri andu metagwo nobel peace prize winners na nobel winners a economics, physics, aingi ni tuthuri twa seventy five, eighties, tukuru twina wisdom tugi muno. Na riu Judges hihi kiria ingienda ni miaka inyihio, kuuma gutuika Judge yongererwo kuuma na hau thi, mundu agatuikaga Judge kuuma fifty years nondakahitukie seventy five years. Thank you very much.*

### ***Clapping from the audience***

**Mercy Njoka:** *Thank you very much niaheana mawoni make. Wa kana oima? Oima mutumia uyu and then wa gatano*

**Grace Wanyeki:** *Nii hakwa ndiuma na Maundu maingi nogucokeria ngucokagiria Ma Commissioners ngaatho niundu wa Maundu maria marutite. Njitagwo Grace Wanyeki. Na njuge ati andu aria maroiga ati; Constitution ithondeketwo ni Ma Commissioners mari aiki, mamenye yumite from grassroot. Andu nio methondekeire tondu Maundu maria mothe merwo hau ni maria twaiguire maheanwo views haha. Kwoguo gutiri undu wao methondekeire, ni Maundu maria ithui wananchi tuoigire guku. Na kwoguo ri makiuga ati; ni Ma-Commissioners methondekeire Mombasa, nikuhitia*

*marahitia, na acio maroiga uguo, ni aria maikaraga o Nairobi. Matimenyaga uria gukoragwo guku village ini tiga no gutuira meretaira ati, Commissioners nio methondekeire na Maundu moimire oro guku. Uguo noguo nyuma naguo.*

**Mercy Njoka:** *Thank you very much. Ningwenda kumuria oringi please, wona ndagutikiria warie, ukoya mathaa manini muno. Ndagika nini muno, nigetha please tuhote kugia na aria aingi o uria kwahoteka. Please.*

**Henry Kinyua Njoroge:** *Ngwambiriria na gucokia ngaatho ni wira uria urarutwo ni Comission na magithii kuria meguthii mamenye ati, aturi a Kenya kana citizens a Kenya me thutha wa Commission ino na nitumietereire na nituetereire Katiba njeru.*

*Ngwamba gukana uria guatuika ati Judges maikare miaka makiria ya seventy five. Nimui thiku ici, andu nimarakura na ihenya niundu wa mirimu na Maundu mangi, uguo sixty five ni enough. Na ningi andu nimaragithoma muno, uguo sixty five years niiganire na aria megukorwo makiritie sixty five, nimehere, meherere angi aria mena githomo. Undu uria ungi ni district elective councils ici cia kuuma Bunge ino njeru. Hari mundu ukugite elective district councils ithurwo ni President. Nii ingiuga turege uguo tondu angikorwo ndirathurwo njuke nguathe ri, githi tikaba ugithura we ndirathii guatha nigetha ngoragwo ndi accountable hari we.*

*Undu uria ungi wangenia thiini wa Katiba ino ithondeketwo kahinda ini gaka, ni uhoro wa ku-impeach MP aitu. Aremwo ni kuruta wira, tugoka tugaikara thi, thirty percent tukamueheria tondu andu aingi nimaremetwo ni guturutira wira ta Ndia tuturite na thina. Na thina riu angikorwo niturimeheragia maremwo ni kuruta wira, kiu ni kياما hari andu a Ndia na ngwiciria hau notunyitanire ithuothe na kunyita uguo.*

### **Clapping from the audience.**

*Undu uria ungi wigie land matters, land matters itinariririo uhoro wa ku-repossess. Tondu kuri migunda ingi-grabitwo. Rekei twambe tutige kuri grabbers aria mara-grab plot. Tuthii kuri grabbers aria mara-grab mundu. Ta riu nii nga-grab my sister mugunda. Ngamuima right ya ku-inherit. Kana my brother aka-grab mugunda witu agathii agatuika niwe uraugaya. Niwe wina kihoto kinene munono gia kunyita mugunda kana igai riitu. Ona ringi ni illegally kuuma kuri watho kana uhoro wa inheritory kana will iria muthee ringi angikorwo nigukua akuire. Tuge migunda iria yoyetwo na njira itagiriire kuuma ku-grab migunda ithiini wa family, icokerio ene na kuringana na Katiba ino njeru kuandikwo uguo ati, migunda kugie na kihoto gia gucirira iria I-grabitwo kuuma family igicoka guthii kuria kungi, plots na kuria kungi.*

*Undu wa muico naguo ni uhoro wa national council ino ya Parliament ino irerwo ni iguthondekwo, bururi uyu twina anake na airitu mari below forty five years ona reke tuge thirty five years. Na nio aingi. Angikorwo rights cia atumia*



*niiraruirwo ri na magatuika ni marginalized na mwanake na airitu aria anini. Gwatuika ati miaka ino thirty five niyo turithuraga andu nao mathii Bunge ino ingi nini, na nindirami-support ino irerwo ikorwo iri Lower House. Gugatuika Upper House. Gugatuika andu acio marithuragwo na thirty five years na aria angi a national assembly ni twenty one years. Turituraga o Bunge iria ungithii umuthi aria matari mathii Bunge. Ni athuri akuru muno ona amwe ni matirima maretha, angi marehagwo kinya hakuhi na wheelchair nigukaira. Uguo tukuenda anake a twenty one years, I unifiyo na ino ingi ya national assembly yuke twenty one years. Nigetha bururi wathwo ni andu mena hakiri, andu athomu na andu mena hinya wa kuwatha. Maritwa makwa ni Henry Kinyua Njoroge.*

**Mercy Njoka:** Thank you very much. *Nigetha mwarimu agie na ihinda riega, ekwamba gucokia ciuria icio. Nokorwo kiria urenda kuria niegucokaniria agicokia ici ingi no nitukugia na ihinda ringi wona ariki gucokia icio.*

**Eunice Gichangi:** Mimi nitaongea kwa lugha ya Kiswahili na ninatumai tutaendelea kuelewa. Lakini ukija hapa na ikiwa utapendelea kuongea kwa Kikuyu au pengine wewe Kiingereza ndio lugha ambayo utaweza kutumia ni sawa. Lugha ile ambayo unaona utaweza kujieleza vizuri, hakuna shida, uendeleo na hiyo lugha. Tuko Kenya mpya, Kenya huru.

Nitaanza kujibu maswali ya Mzee Joseph. Kwanza aliuliza juu ya freedom fighters, akauliza mbona hatuwatambui kikatiba. Bwana Joseph pamoja na watu wengine hata Dr Mutugi na wengine wameongea kuwa siku itengwe kuhusu freedom fighters. Nimeenda constituencies nyingi, nilianza safari kule Nyandarua, (inaudible), Engineer, Ol-kalaos. Tulikuwa na Bwana Njeru kule Muranga, tena tukaenda Kerugoya na sasa tuko hapa. Watu wengi, kutoka sehemu hizo zote wanasema ya kwamba tusiisahau siku ya 20<sup>th</sup> October, jina ndio wanasema libadilishwe. Wengine wamependekeza Nationalist Day, Hero's Day, wengine Freedom Fighters Day lakini I think I have got the message kuwa hiyo siku isisahaulike, na huo ujumbe utaenda.

### ***Clapping from the audience***

Tena, Bwana Joseph akauliza mambo ya ndoa. Tunasema ya kwamba yeyote ambaye ataoa ama kuolewa na mtu ambaye sio raia wa Kenya tunasema tunampatia nafasi au haki awe raia wa Kenya. Sasa akaniuliza kuna wale ambao kwa Kiingereza tunawaita homosexuals, kama inawezekana mwanamume amuo mwanamume mwenzake, mwanamke amuo mwanamke mwenzake.

Ukiangalia Katiba za nchi nyingi na tumezisoma na tukaangalia, na kuna Katiba za kule Europe na kadhalika ambazo zimekubaliana ndoa kama hizo na zimetambua ndoa kama hizo. Hilo jambo tulilijadili kwa sababu hakuna jambo hatukuweza kulifikiria. Hata hilo tulijadili na tukasema ya kwamba maoni ya Wakenya inaonyesha hawataki. Kwa hivyo hapo hatujaweka.



Ni kwa sababu hauoni haki kama hiyo kwa hivyo hakuna haki kama hiyo. Hatukubali ndoa baina ya mwanamume na mwanamume ama mwanamke na mwanamke. Kwa hivyo tikitaja ndoa, tunasema ni mwanamume ameo mwanamke au mwanamke ameolewa na mwanamume. Hapa hatuhitaji kuandika, tukiandika sasa tunaleta makosa kidogo. Kwa hivyo ikiwa ni hivyo unajua hatutambui. Kama tungetambua, ungeona haki nyingine hapo imeandikwa hivyo lakini hakuna. Tulilijadili hilo jambo sana.

Jambo lingine amesema, ile sheria ya naturalization, yaani mtu ambaye sio raia wa Kenya, amekuja huku Kenya na ameishi huku pengine anafanya business, na amekaa miaka saba, tunasema ana haki sasa ya kuwa Mwanakenya. Yeye anasema mtu kama huyo miaka saba haitoshi, ya kuwa tuongeze iwe kumi na tano ama hata ishirini. Hayo ni maoni yako na tumeyachukua.

Kuhusu haki za watoto, kuna sehemu nilisema ambayo inasema kila mtoto anahaki ya...katika Kiingereza kama ningesoma inasema every child has a right to be free of corporal punishment or all other forms of violent or cruel and inhumane treatment in schools and other institutions responsible for the care of children.

Yaani tunasema mtoto akiwa shuleni ama pahali popote ambapo watoto huwa wanawekwa, pengine kama Sunday School au pahali kama hapo ambapo kuna watoto kadhaa. Tunasema mtoto akiwa huko anahaki asichapwe ama asipewe treatment ambayo haifai. Kwa hivyo huyo mtoto akiwa pahali kama hapo alindwe vilivyo.

Hatujasema mtoto wako nyumbani eti akikosea, ninaona mzee anafanya, (gestures) hatujasema hivyo. Lakini tumesema akiwa shuleni ama institution yoyote anahaki ya kutochapwa. Maana ya kufanya hivyo, hata children's law vile ilivyo sasa ndivyo inasema. Tumekuwa na visa ambavyo ni vya huzuni ambapo mtoto anapitia akiwa shuleni na kadhalika na ndio maana tumeweka sheria kama hiyo kikatiba. Lakini already hiyo sheria is in force, ikiwa katika children's part.

Tena akauliza haya mambo ya devolution. Hii serikali ambayo tumesema inakuja mpaka kijijini, village, location district na kadhalika. Ni kweli Bwana Joseph hatujapeana specific rules kama kwa mfano ni nani atachaguliwa, atakuwa amesoma kama kiwango gani ama akiqualify uchaguzi utafanywaje, pesa zikija zitatumikaje?

Hivi sasa ambapo tuko hapa, kuna committee ya Tume ambayo imeketi Nairobi na leo kama sio hiyo Tume tungekuwa pamoja na Commissioner mmoja ambaye anaitwa Professor Kabira. Lakini wameketi sasa na hayo ndio mambo wanaendelea kuangalia. Hatukuwa na muda wa kutosha kumalizia hayo mambo yote.

Mlitupatia muda mfupi, tukamaliza mambo mengine na sasa hivi tunaendelea na hizo rules. By the time tutaenda kwa delegates conference, hizo rules za devolution, yaani serikali ya kuja mpaka kwa mwananchi itakuwa tayari, mtaweza kuziona, na kuzisoma na nitawapatia District Co-ordinators ambao watawaletea na mtazifahamu. Kwa hivyo hiyo ni kazi ambayo inaendelea.

Lakini hiyo sheria ambayo tunaendelea kutengeneza haitakuwa part ya Katiba, itakuwa Act, ama sheria ya bunge. Tunasaidia bunge kuitengenezea rules kadha na tumependekeza kutakuwa na Devolution Act. Na tumesema hatutaacha bunge iwe ndio itaendelea na hiyo sheria kwa sababu ndiyo ya muhimu. Sisi tunataka tuimalize, tuwaachie draft ambayo wataisoma na wakiikubali ndio itakuwa Act ya bunge. Kwa hivyo hayo yanaangaliwa.

Dr. Mutugi, asante kwa comments zako. Pia ameongea juu ya national holidays na hapo nimesema pendekezo hili nimelipata. Tena akaongea jambo lingine muhimu. Akasema ndio kikatiba tunasema juu ya haki za ardhi kuwa kila Mkenya anaweza kuwa na ardhi ama kununua shamba popote upendapo. Kuwa ukienda kule Coast na ununue shamba lako sawa, ukienda Nyanza ukinunua ni sawa. Lakini akauliza je wale ambao walipokonywa ardhi yao? Na tunajua ni wengi, tushasikia hadithi za clashes ama hata wengine wetu tumekuwa affected kule Rift Valley, kule Coast Province na hata hapa ninasikia hata hapa, ni kwingi.

Vile ambavyo tulifanya, tumesikia malalamishi ni mengi, hata kule North Eastern kuna mambo ya ajabu yametendwa huko na walitupatia maoni yao. Kwingine kunaendelea hata tukiwa hapa, ukienda sehemu zingine za Rift Valley, bado kuna hizo shida.

Vile tumesema ni hivi, kama shamba lako limechukuliwa na mwingine, awe ni nani ama hata kama mali yako yameharibiwa na mwingine, nyumba ikachomwa na kadhalika, ama hata mtu ambaye ni wa familia yako akauwawa ama wewe mwenyewe ukaumizwa. Njia ni mbili: kama ni shamba lako ulipokonywa, tumesema kuna ile Tume tumeiita National Land Commission. Hiyo Commission ni yako wewe Mwanakenya, ni Commission huru na tumeipatia uwezo wa kusikiza mambo yote ya kupokonywa kwa ardhi.

Pia kuna ile nilisema Commission on Human Rights and Administrative Justice. Hiyo Commission mkiangalie kwenye sehemu, hapo baadaye mtasoma sehemu za mwisho za hiyo katiba, transitional. Tumesema ya kwamba hiyo Tume ikibuniwa tu, miezi tisa ya kwanza ambayo hiyo Tume itafanya kazi, itakuwa ikiangalia ile tunaita past Human Rights abuses. Yaani wale ambao haki zao za aina yoyote zimepokonywa hapo mbeleni.

Kwa mfano ikiwa wewe shamba lako limechukuliwa na mtu mwingine, iwe ni huku au ni Burnt Forest au ni Likoni, hapo utakuwa na opportunity ya kukimbia kwenye Commission on Human Rights and Administrative Justice na tumesema inakuja mpka kwa district level. Hilo jambo litafanyiwa investigation na baada ya hiyo wale ambao watapatikana watakuwa wamekosea watafanyiwa prosecution. Tumesema tumeunda board mpya ya prosecution, Director of Public Prosecution ambayo ni office ambayo ni huru, haina uhusiano na serikali, bunge, au na majaji. Ni ofisi ambayo ni huru, na watafanya prosecution.

Ikiwa ni mali ya mtu imechukuliwa, atarudishiwa kikatiba na kisheria. Kwa hivyo ikiwa kuna mtu amepokonya ardhi ama mali, hapo ndio utapeleka problem yako. Miezi sita ya kwanza ya Commission on Human Rights, hiyo nido kazi kikatiba

tumewapatia. Miezi hiyo tisa itakuwa ni kusikiliza haki za Wakenya ambazo zilipokonywa hapo mbeleni. Tuko pamoja eeh? Hiyo ni muhimu.

Kutoka hapo, mambo ya Kadhis Court, vile ambavyo tumefanya ni kweli kuwa idadi imeongezwa, sasa zimekuwa sitini na sita. Lakini kazi ambayo korti za Kiisalamu zitakuwa zikifanya haijabadilika. Ile kazi ambayo korti za Kiislamu hufanya hivi sasa ni kazi ya kutatua kesi ambazo ni za kijamii. Kwa mfano mwanamke Muislamu akiolewa na mwanamume Muislamu na waamue kuachana, huko ndiko wanaweza kupeleka mambo yoyote ambaye yatazuka kama yule ambayo atachukua watoto na zinginezo. Lakini mambo yale mengine yote, bado yataendelea kupelekwa kwenye korti za kawaida.

Dr. Mario nimechukua pendekezo lako ya kwamba hayo makorti unaonelea ni mengi sana na yanalipwa. Na kuwa percentage ya watu ambao ni Waislamu, hayo ni mambo ambayo nimeyachukua kama homework. Hata mimi ninabeba kazi na kwa hivyo hiyo nimebeba.

Bwana Wanjohi, pia yeye alipendekeza hizo days, ndio nimechukua. Nimesema imeongezeka na maoni ya Wakenya wengi zaidi kote ambako nimeenda. Pia akasema wale ambao wanaoa ama kuolewa na raia Wakenya, tumesema wakae miaka tatu katika ndoa, iwe ni the time to test the seriousness. Yeye anaona hiyo miaka ni michache, tuongeze iwe tano. Hilo ni pendekezo lake. Tulijadiliana hata hilo jambo, wengine wakasema miaka tano, wengine wakasema hata mika kumi, wengine wakasema miaka tatu, wakasema kwa nini tumpokonye haki na pengine amempenda msichana wetu au amependwa na mwanamume wa huku kwetu. Finally consensus ikasema ni miaka tatu. Lakini pendekezo lako pia sitalitupa mbali, pia nimeliandika.

Kuhusu viti vya kina mama, Bwana Wanjohi anauliza mbona sisi sote tusipigania viti kisawa? Vile tulifanya kama Tume, tulifanya vile nchi nyingi hufanya. Kile ambacho tumefanya, kwa Kiingereza tunasema ni Affirmative Action. Yaani unaangalia sehemu mbali mbali ambazo pengine hao watu haki zao pengine kwa sababu za kihistoria, kimila au hata za kidini, hiyo sehemu ya watu hawajaweza kuwa na haki sawa na wenzao. Kwa hivyo vile ambavyo katiba inajaribu kufanya, ni kujaribu kuwavuta wale ili wawafikie wenzao.

Wakiwafikia wenzao hawaendelei kupewa hizo benefits, zinaondolewa. Kwa hivyo Affirmative Action ni kitu ambacho kinatumia kwa muda tu, ili pahali ambapo sasa tutaona ya kwamba sasa kina mama pahali wamefika, wao pia wapigania kama wenzao, wana nguvu ya kutosha na hakuna sababu ya kuwasaidia tena. Basi hayo mambo yataondolewa. Kwa hivyo, hiyo ni temporary situation, sio situation ya milele. Lakini nimeandika pendekezo lako.

Bwana Murage pia amezungumza juu ya viti vya bunge na akauliza kama kuna vile vimetengwa na anasema yeye pia anamuunga mkono mzee yule mwingine ambaye alipropose kuwe na viti vya watu ambao wako na disability. Hilo ni jambo ambalo hii draft haijafanya na ni jambo la muhimu ambalo tunaenda nalo. Hapo tena, mmetupatia homework ambayo ni ya muhimu sana na tutaenda kuifikiria. Sio hapa tu ambapo nimeambiwa hayo mambo, kila constituency watu wameongea juu ya viti vya the disabled.

Halafu kuna dada yangu pale ambaye ameongea juu ya ID cards, akasema kina mama katika ndoa wakibadilisha majina siku ya kuondoka sijui alisema inakuwa ngumu kubadilisha tena? Inakuwa ngumu kubadilisha tena? Pengine umepata jina la bwana

yako na sasa unataka kuibadilisha tena liwe jina la baba yako?

(Interjection) **Speaker from the audience:** Ninasema iwe inakaa na jina la babako kwa sababu (inaudible).

**Eunice Gichangi:** Tuko pamoja, thank you. Anasema ya kwamba mtu akiolewa awe na haki ya kuendelea kutumia, kama ni mimi niendeleo kutumia jina la baba yangu badala ya kubadilisha kwa lile la bwana yangu.

Hiyo ni haki yako hata sasa, hakuna mtu ambaye anakulazimisha kubadilisha jina lako. Ukipenda kutumia la babako, la bwanako, ama ukipenda kutumia lako moja tu, ni sawa. Hakuna mtu anakulazimisha kulibadilisha. Lakini ukibadilisha halafu tena katika ndoa muachane, sasa unahaki ya kwenda kubadilisha documents zako ikiwa kikatiba, kisheria mmeachana. Sasa utakuwa na haki ya kulibadilisha jina lako lakini itakubalishwa kulibadilisha jina ikiwa kikatiba na kisheria mmeachana. Sio ule ati pengine nimehama nikaenda kuishi kwingine, ni ile tumeachana kisheria.

Pia akauliza juu ya national disasters. Angependelea tuweke jukumu la serikali kusaidia watu ambao wako na disasters, kwa mfano kukiwa na flooding, ama kukiwa na ukame, serikali ipewe hilo jukumu. Hatujaiweka directly lakini jukumu za serikali, article 14, inaweza kuingilia hapo. Lakini hatujataja jina disaster na tutaangalia hapo.

Nafikiria nitakomea hapo na tuendeleo na maswali. Nitawaomba mkija kutoa swali liwe fupi kwa sababu ninaona tuko wengi ili kila mmoja wetu ambaye angependa kuongea apate nafasi. Ikiwa unaona pengine hautapata nafasi ya kuongea ama ungependa kuandika proposal yako, tuko na file hapa, unaweza kuomba kijikaratasi uandike proposal. Tutaisoma kabisa na tutaiielewa. Kwa hivyo njia ni hizo mbili, thank you.

**Mercy Njoka:** Asante sana. Wale wameongea tafadhali mtaturuhusu tupate wale ambao hawajaongea. Tutaanza na huyu, wa pili, wa tatu, nne, tano, sita na saba. Wengine mtaongea hiyo round nyingine.

*Noise from the audience*

**Speaker:** Sasa katika hayo makelele watu watasikia swali langu kweli?

**Mercy Njoka:** Wale ambao wanatoka, tafadhali mtoke ama mnyamaze.

**John Wahome:** *Nii hakwa ha ritwa ni John Wahome na kiuria giakwa no kinini ni tondu hari mundu athire kugweta haha no ndinaigua agweta uria, uria kiuria kiu uria ndoritie hindi ya kuandiithia maoni macio. Uhoru wa andu aria mena migunda minene irario ni hiti. Nao andu aria angi guku matura o icagi. Matura o thina ini kuria, angi maithe*

*mao matiri na migunda minene nayo migunda kuria irario no hiti. Handu hau nii nindoritie kiuria kiu haha hindi ya kwandikithia kiria na ndinaigua handu hau hagwetwo kana hafafanuo uria hagiriire. Haria hangi, uhoro ucio wa mbeba, akorwo ni mbeba nitige kwirwo kiria... niciirwo uhoro akorwo ni kirima ta Mt. Kenya. Ota uria naguo muthenya ucio wa wiyathi ukire uhoro wa kiria...tondu nitukwendaga utuike wa Mau Mau. Na Kenyatta ucio nowe mu Mau Mau. Uguo haha ri, ungituika uhoro wa public day. Nohatigatuike ati nihekwirwo ati ni ha mundu. Aca. No nihetwo okorwo ni kirima okorwo ni mbeba ciitwo kirima. Mbica ya kirima, kana akorwo ni uhoro wa muthenya ucio. Witwo o uguo witiirwo wa public day. Nii ndiri na Maundu maingi no macio. Ningi ha uhoro wa ngari guku, gukinya andu na Maundu macio, macira macio magacoka kuragira oro uguo. Okorwo ni ng'ombe yoka yahurwo, ng'ombe iyo mundu ucio niwe ugucoka kuriha na ng'ombe ndiri na hakiri na we uratuara ngari niwe wina hakiri. Na undu ucio wothe noguo nondandikithirie haha na ndinawuigua ho. Uguo Maundu macio nonyende makorwo makirumirirwo uria kuagiriire na niwega.*

**Mercy Noka:** Thank you very much. Wa pili.

**Joseph Mwaniki wa Muchiri:** *Ritwa riakwa njitagwo Joseph Mwaniki wa Muchiri kuuma Sagana. Wa mbere, I want to congratulate the Tume for the good job they have done. Mambiriirie guku kuri ithui na macoka moka kuri ithui for the second time. He mutongoria wa bururi uroigire atiriri ona atathomete Katiba iyo, ati Katiba iyo ndingiruta wira thiini wa Kenya, no arutire kundu gwitagwo atia? Europe. Nimuathomire uguo? Riu ithui twi haha ri, nitwetikira ati niikuruta wira Kenya? Mmekubali hiyo? Haya it goes down in history.*

*Secondly, hindi iria tukuaragiriria Parliament ini, he a very important position which has been omitted. Ndinaigua kuagwetwo anything to do wi the opposition. The leader of government business has not been mentioned thiini wa Katiba ino njeru. Tondu twina ciama nyingi next year, with the new Constitution, no onginya opposition ikorwo na position thiini wa Constitution. Hau nihega?*

*Haya wa keru, with the new President na runner up wake. He handu hatigwo hari pending na tihega tondu guatuika my running mate, if it is Mercy, the District Co-ordinator who is my running mate as President, ingikua, she comes in here, even if I die the first year, oke aikarire giti kiu nowe ndegukorwo na muteithia. Ingikua mwaka wa mbere ri, ekuruta wira ari wiki miaka ina. That position has not been addressed by the Constitution. You only said that the Vice President to take over no nake angikua, either the Speaker of the National Assembly a take over kana wa National Council, sindio? No uhoro wa Vice-Presidency, watigwo uri pending.*

*Pointi iyo ingi, nituaririe uhoro wa ceiling. Miaka ya President, tuaigua ikorwo iri kuma thirty five upto seventy. Limitation that is. Ceiling ya miaka ya Mpri, ndinaheanwo. Mundu ari na miaka ninety ri, no athii Parliament. So that is a position which has been left unattended. Kwoguo ri ona MP they should be given a sealing of years. Point iyo ingi, all*



Constitutional office holders, mabataire kuheo only two terms. Before the appointment position, *maka-appointwo first term, angikorwo ni approve* good second term. We have got an Auditor General today in Kenya who has worked for over seventeen years and that is a Constitutional office, and I believe it is very unfair. That should therefore be addressed. All appointments should be limited to a maximum of two terms of five years each, a maximum of ten years.

Lastly, I want to cater for the disabled, the marginalized groups. *Andu aya turutaga igoti. Ithui turi andu agima na igoti turutaga kamilifu kuringana na sheria na kuringana* na katiba. *No andu aya* disabled, they should pay 50% of taxation compared to the *and u aya agima*. *Nimuetikania no uguo? Githi uguo ti wega? Fifty percent. Muicoini ningucokia ngatho*, I want to thank the Commissioners because, *nda sub-mitire* twelve pages in writing to Patrick which was in print and 50% of it *nindaciona I thiini wa Constitution*. Thank you very much and God bless you and continue strong, we are behind you. Asanteni sana.

**Mercy Njoka:** Thank you very much. The third speaker.

**Kibuga:** Kwa majina ninaitwa Kibuga na ninashukuru sana kwa kupewa nafasi hii ya kusema jambo moja ama mbili. Swali langu la kwanza ni kwamba, tuna watu katika serikali na ni wakubwa na kusema kweli mwananchi wa kawaida ndiye analipa kodi ile kubwa sana.

Mimi wenyewe ninakaa Mombasa na huona vile watu wakubwa katika serikali wakitaka ku-import things kama magari hivi, wako na marafiki katika tuseme navy, na wale watu wakileta magari hawalipi kodi. That is what I think is called import duty. Mtu kama president ninafikiri akifanya mambo yake ama akileta vitu vyake kutoka ng'ambo pia yeye mwenyewe sidhani kama analipa kodi kama watu wengine. Swali langu ni moja, ni kwa nini hao watu hawalipi kodi kama sisi? Hilo ndio swali langu la kwanza.

Swali la pili, tuliambiwa ya kwamba hii Constitutional Review, imeonelea kwamba tuwe na nyumba mbili. Moja ikiwa na watu mia tatu na nyingine ikiwa na watu mia moja. Sasa tukiangalia uchumi wa nchi, ile kodi ambayo hutozwa kulingana na watu wale ambao wako na upper hand, wanasema tunaokota about Ksh 230 billion. Na nikiangalia hizi nyumba mbili, mkiangalia ile mishahara wale MPs wanapewe, ninaona itachukua a very big percentage of the Kenyan budget.

Kwa hivyo proposal yangu ama suggestion yangu ilikuwa kwamba, wale ma-MPs ama wale leaders ambao tutachagua wasiwe wengi sana kiasi ya kwamba watachukua budget kubwa. Wawe kama tuseme zile constituencies ambazo tuko nazo, 210. Kwa nini tuseme tuwe na MPs, wale wale, 210? Wale 90 ili wafike three hundred, sioni kama kuna haja ya kuwa na watu wengi kama hao.

Tatu, when we come to the National Council, ambayo inasemekana iko na watu mia moja na ambao kila district itakuwa na mtu

mmoja, ninaona hapo nina swali. Hiyoni kwa sababu, hapa tuna kina mama na kusema kweli tuna kina mama ambao wamesoma sana siku hizi na ni wazuri. Tukiangalia tukiona, tukiangalia sana tunaona ya kwamba wale kina mama ambao wako katika uongozi katika nchi yetu ni watu ambao wame-excel sana. Kwa hivyo kuna uwezekano kuwa kati ya hao watu seventy, kuwe na kina mama ambao ni wengi zaidi?

Swali langu ni kwamba, supposing out of the seventy members in the National Council tuwe na kina mama zaidi ya fifty, sasa hao wengine thirty, na inasemakana the rest thirty hao ndio watakuwa kina mama. Is that fair surely? Is that fair? I am not against kina mama, I love them. I have a wife, I have a mother and I know how caring they are. But sincerely speaking it is possible that we are going to have more than half of the seventy being mamas, sasa hao wengine thirty kwa nini tuwe nao? Kwa nini wasiwe half kina mama na half wazee? Asanteni.

**Mercy Njoka:** Huyo mwingine.

**Charles Wachira:** Asante sana. Jina langu ni Charles Wachira na mimi ni mmoja wa wale walileta maoni yao kwa niaba ya Wacatholic wa eneo hii ya Baricho Parish.

Kitu cha kwanza ningetaka kusema...

(Interjection) **Mercy Njoka:** Paza sauti.

**Charles Wachira:** Nipaze sauti? Ninasema hivi, mimi ningetaka kwanza kusema juu ya hawa ma-commissioners ambao wamekuwa wakifanya kazi hii. Nitarudisha shukrani sana kwa hawa Commissioners kwa sababu ya ile short version ambayo walitoa kwanza katika Sunday Nation, walitupatia picha za hao macommissioner wote. Halafu wakatuandikia wale ambao waliweka sahihi hii Katiba wakati ilitoka. Na kati ya wale ishirini na tisa, macommissioner wanne waliandikwa absent na kuna wengine walikuwa na apologies, kama Attorney General.

Haja yangu sio wale walikuwa na apology kwa sababu hao tunajua ukiwa na apology, unakubaliana. Kuna watu wanne na tunajua majina zao na hata pahali wanatoka na hata picha zao, nyuso zao tunazijua. Lakini kitu kinastajabisha ni kwamba mmoja wa wale waliandikwa absent ni mmoja wa wale tulipatia maoni yetu kule Kiburu. Hivi ni kusema yeye hakuweka sign.

Tangu hao watu waandikwe kuwa walikuwa absent, hatujasikia hao watu wakieleza ni kwa nini walikuwa absent. Na hao watu wameletwa ama waliwekwa kwa hiyo Commission na watu ama kikundi cha watu ama parliament. So they owe us an apology.

Mimi nilikuwa ninasema hivi, hawa Commissioner wanne, majina tunayajua, wanawake wawili na wanaume wawili. Wakati huu tumevaa utepe wa manjano kwa sababu ya mawakili, ma-advocates wawili na majaji wawili na tunayajua majina yao. Sasa hao

watu wane, pengine zile shida tunazo wakati huu, kwa sababu hata hawajaeleza ni kwa nini hawakusign hii document, pengine ni wale tulikuwa tunasikia ati hao ndio wanachukua simu kila mara, kila mara wanatoka, kila mara kuna watu wanawa-control. Hatujui na hatutaki kuwalaumu kwa sababu ya hiyo.

Kuna kitu ningetaka kuwauliza nyinyi ma commissioner, wale ambao wanafanya kazi hii nzuri. Kama tunaweza kuvaa utepe wa manjano kwa sababu ya watu wanne ambao percentage ile wana-represent ya Judiciary ni kidogo sana. Ukilinganisha na ile percentage hawa Commissioners wanne wanachukua kwa ile Commission yote, kwa nini tusivae utepe mweusi kwa sababu ya wale ambao wanaturudisha nyuma? Ningetaka Commission pia ifikirie haraka sana vile tunaweza kuvaa utepe mweusi, black ribbon, kabla ama wakati ile National Conference itakuwa inaendelea. Na hivyo itaonyesha ya kuwa, majority of us are against the four kwa sababu hawajatuambia ni kwa nini hawajasign document, why they were absent and they are using our money. Thank you so much.

**Mercy Njoka:** Asante sana.

**Geoffrey Gichangi:** Asante sana. Kwa majina ni Geoffrey Gichangi. Langu la kwanza ni kurudisha shukrani kwa sababu nilikuwa hapa na nikatoa maelezo yangu na nimeyaona kwa hiyo draft. Kile mimi ninataka kuongezea, ni kusema hii Constitution ikiwezekana ikitoka, iwe ikifundishwa kutoka Standard one up to university level. Hiyo ni kwa sababu ile old Constitution, watu wengi hawajui na hawajawahi kuiona. Ili tuwe conversant na hii Constitution, iwe inafunzwa from primary level ili mtu akifanya chochote awe anajua ni nini anafanya.

Cha pili, kile mimi ninataka kusema ni mambo ya presidential qualifications. Mimi kwangu ninaonelea, umri wa president uwe kutoka miaka ishirini na moja mpaka miaka kama seventy five. Kwa sababu tunaona kama hapa huyu kijana wa Kabila, tunaona anaongoza vizuri na ni kijana mdogo, na kuna wengine ambao wako na miaka kama seventy na tunaona uongozi wao ni mzuri. Kwa hivyo tusiangalie umri, tuangalie akili ile iko na mtu.

Ya tatu ni kuhusu nomination of district representatives, ama hii nimesikia inaitwa upper house, ama sivyo? Mimi maoni yangu ni kuwa kuna districts zile zilitengenezwa za political, na ikiwa tutatumia number kulingana na district, kuna watu wengine watakuwa na mileage kuliko wale wengine kwa sababu ya zile districts. Mimi maoni yangu nilikuwa ninaonelea, badala ya district, tuwe tukiangalia na constituency na population ile iko kwa constituency ili tuwe na usawa. Hiyo ni kwa sababu ukiangalia kuna constituency iko na watu kama elfu nne na kuna nyingine iko na watu kama mia moja na kitu. Sasa hizi tukizilinganisha, ile iko mia moja na kitu, iwe huyo representative awe anawekwa hapo.

Ya nne ni kuhusu ministers. Kulingana na hii Katiba, mimi ninaonelea badala ya ministers, nilikuwa nikisoma ile ya mwanzo nikaona ati watachaguliwa wale wako nominated in the upper house. Kwa maoni yangu, mimi ninaonelea ministers wawe wakichaguliwa kutoka na constituencies, wale wamekuwa wamechaguliwa...(incomplete) hivyo viti viwe vikiwa advertised, ili

tuwe tunapata wale watu wakiingia hapo iwe ni mtu ame-qualify na sio kuteuliwa. Ni hayo tu. Asante.

**Mercy Njoka:** Asante sana. Sasa nitawapatia wawili, huyu na yule halafu tutamalizia hapo.

**Joseph Thuita:** Asante sana. Kwa majina ni Joseph Thuita kutoka huko Mukore. Kwanza ni kurudisha asante kwa maafisa wa Tume hii kwa kutuletea hii draft. Nilikuwa nime-record mambo matatu huko Kiburu, lakini sikuyaona kwa hii draft na ninataka kurudia tena vile nilikuwa nimesema. I am a retired officer.

Kwanza ningetaka kusema kuhusu wale watu ambao wanakatwa ile pesa ya National Hospital Insurance Fund. Mtu akizeeka anakuwa na taabu nyingi, kama mimi. Anakuwa hana nguvu kwa mwili na magonjwa mengi, taabu za namna hiyo. Kwa hivyo, nilikuwa nimeomba ikiwezekana katika Katiba hii, iwekwe zile pesa ambazo mtu anakatwa na serikali ama parastatal yoyote ile, aki-retire ziwe zinaendelea kumsaidia wakati wa uzeeni. Vile nilikuwa nime-rocodi pale Kiboro na sikuiona kwa draft hii.

Ya pili ni kuhusu lile jumba linaitwa National Social Security Fund complex kule Nairobi. Hapa ninazungumza kwa niaba ya wale watu non pensionable, kuna watu wanaitwa temporary non pensionable people. Hilo jumba ni sisi tulilijenga, watu wa category hiyo na wakati mtu ana-retire hilo jumba tuliliacha papo hapo. Ijapokuwa nililipwa marupurupu yangu hivi na hivi, kwa nini hili jumba wale non pensionable, hawawezi kupewa certificate yake na wawe wanalipwa dividend? Hiyo nilikuwa nime-record Kiboro na sikuiona.

Ya tatu, ni kuhusu wastaafu wote. Kuna nchi zingine wastaafu wanapewa special priviledges, wakati wa kusafiri, hii pesa ya nyumba, house allowance wanaendelea nayo hata wakiwa nyumbani. Kwa nini hapa hatuwezi kuendelea hivyo? Asante.

**Mercy Njoka:** Huyo mwingine.

**Mbuchi:** Ningependa kushukuru Tume ya Ghai kwa kazi nzuri ambayo mmefanya. Jina langu ni Mbuchi. Ninayo mapendekezo machache ambayo ningeweza kufanya kuhusiana na hii Katiba. Kwanza, ninashukuru kwa sababu vile Tume imependekeza kuhusu elimu. Kwa sababu mimi ninafikiria kwamba hakuna raslimali kubwa kwa taifa kama elimu ya watoto, lakini kuna machache ambayo kwangu mimi ninaona yanahatarisha na pengine kudidimiza elimu nchini.

Ukiangalia sana, sana katika maeneo yetu, hasa eneo ya mlima Kenya, ama Mkoa wa Kati, sijui sana kuhusu maeneo mengine. Kuna wazazi wengi ambao wamekosa kutekeleza wajibu wao katika elimu, kuwaelimisha watoto wao kwa sababu moja ama nyingine. Kuna wengine ni kwa sababu ya umaskini na kuna wengine ni kwa sababu ya kukataa tu. Baadhi ya watu wametoka hapa na kutoa mapendekezo yao.

Kwangu mimi ningeonelea ya kwamba, iwapo mzazi anao uwezo wa kumelimisha mtoto wake na labda amekataa, ni vizui

kama serikali ingeweza kuchukua hatua. Yule mzazi labda achukuliwe hatua. Ndio tumeona katika Katiba iliyopendekezwa kwamba ni lazima mtoto apate elimu, lakini ni vipi ambavyo tutahakikisha ya kwamba kila mtoto amepata. Sheria ni kitu kimoja, na kutekelezwa kwa ile Katiba ni kitu kingine.

Ikiwa serikali inaweza kama tuseme mzee ana shamba, ile shamba inaweza kuchukuliwa na taifa. Iwe ni mali ya taifa ambayo itatumiwa labda kuwaelimisha wale watoto.

Kitu kingine ambacho ninaona kimedidimiza elimu katika mkoa wetu na sehemu nyingi za Jamhuri ni ulevi. Hapa labda wazee mtaniwia radhi kwamba watoto siku hizi, jukumu la malezi tumeliweka katika mabega ya akina mama. Kwa mfano mimi ninasema kama mwalimu, ukiangalia katika shule nyingi ama unapoambia mtoto akamlete mzazi kwa sababu moja ama nyingine, ni nadra sana kuwaona wazee wakifika mashuleni.

Wengine wameingia katika uuzaji wa pombe na labda ningependekeza ya kwamba swala la pombe lichukuliwe kwa undani zaidi. Kunazo pombe za aina nyingi, sitaki kusema kwamba pombe ni mbaya. Lakini kuna hizi pombe ambazo siku hizi zimeingia katika Jamhuri yetu na maeneo yetu. Kuna lile shirika la kukadiria ubora wa bidhaa, je linafanya kazi yake? Na kama linafanya kazi yake, kwa nini tukapata vinywaji vingine ambavyo labda mkinywa ama wazee wakinywa, vijana wakinywa, hawawezi kufanya lolote lile ambalo litasaidia uchumi wetu na hata familia zao? Kwa hivyo, ni vizuri jambo hili lichukuliwe ama litiliwe maanani. Ikiwa shirika lile litawekwa kwenye Katiba na lipewe nguvu zaidi.

Kitu kingine ni kuhusu haki za mtoto. Tumesema ya kwamba mtoto ndiye atakayejenga nchi kesho na tusipozingatia sana sana masilahi ya watoto, elimu, afya yao na mengine kama hayo hatutakuwa tukifanya chochote kile. Kwangu mimi ninaona ni vizuri tumependekeza mtoto awe na haki zile. Lakini, lazima sheria ambazo labda zitaundwa baadaye zihakikishe kwamba zile sheria zinafuatwa na mtu akikosa yale, labda kutakuwa na adhabu fulani.

Upande wa elimu, tumesema kwamba elimu ni ya lazima. Je katiba hii imehakikisha kuwa elimu ile itakuwa ya lazima ama tu ni mapendekezo tutaweka kwenye karatasi, kisha tuweke kwenye masanduku ama tuweke kule kwenye rafu katika maofisi ili hali tunaona kwamba watoto wako nyumbani.

Jambo lingine ambalo ninafikiria ni nzuri. Ikiwa tutahakikisha ya kwamba elimu ni ya bure labda kwa shule za msingi na za sekondari, ikiwa mzazi hawezi na pengine mtoto labda amepita kuendelea katika chuo, je serikali ina nafasi gani katika sehemu ile? Kwa hivyo ni lazima serikali ichukue lile jukumu. Ikiwa mtoto amepita, tuseme tu masomo ni ya bure katika shule za msingi tu lakini hata wale ambao wamepita katika vyuo vikuu.

Kitu kingine ambacho ningetaka tuangalie ni kushirikishwa kwa watoto katika kazi. Ndio jambo lile liko katika Katiba, lakini hata leo hii tunaona watoto wakifanya kazi. Ukienda katika mashamba makubwa, makubwa ya kahawa, ya pareto utaona

watoto wameajiriwa. Wengine wameajiriwa katika manyumba kama walezi wa watoto. Ni vizuri tujue, ni mtoto wa kiwango gani, mika mingapi ambaye ataruhusiwa kuandikwa, kwa mfano kama mtumishi wa nyumbani.

Hiyo ni kwa sababu mimi sioni ni vipi utamwajiri ama nitamwajiri mtoto wa miaka kumi na below. Kulingana na hii Katiba, mtoto ni yule ambaye hajahitimu miaka kumi na minane, hivyo basi anastahili kuwa shuleni. Kwa sasa hivi watoto ambao wako katika kidato cha nne, wako chini ya miaka kumi na minane. Hiyo ni kumaanisha yeyote yule ambaye ameajiriwa, haki yake imevunjwa.

Kitu kingine ambacho ningetaka labda tufikirie ama Katiba ifikirie ni kuhusu mfumu wa elimu. Mimi kama mwalimu ninaona kwamba elimu imebadilika sana siku hizi kuliko wakati ule nilikuwa shuleni. Leo hii unakuta mambo mengi yanayotendeka katika mashule ni kutokana na ule msongamano wa masomo na kule kutokuweco kwa wakati wa ziada kwa watoto. Kwa hivyo, elimu lazima iwe inashikilia na labda elimu inatizama masilahi ya mtoto nje ya darasa.

Kwa hivyo kama ni mashule, yawe ni ya kibinafsi ama yawe ni ya umma, kuwekwe muda maalum. Unakuta wengine wanaenda hata Jumapili, Jumamosi na ni mtoto wa darasa la kwanza. Kwa hivyo jambo hilo lifikiriwe.

Jambo lingine ni kuhusu ndoa. Kuna mmoja ambaye alisema kuhusu ndoa. Leo hii wale ambao wanafunga ndoa katika kanisa ndio tu wanaopata vyeti na labda wale ambao wanafuata ama wanafunga ndoa katika afisi za D.C. Je kuna uwezekano kwamba hata wale wamefanya harusi za kienyeji wapate vyeti kuonyesha kwamba hata hao wameolewa? Kwa maaana jambo lile labda baraza la wazee linaweza kuketi na wadhibitishwa kwamba hawa wameoana kirasmi na wapate vyeti. Kwa sababu hiyo mzee hawezi akaenda kuoa bibi mwingine ama labda akaenda kule nje kwa sababu bibi anacho cheti.

La mwisho kwa sababu sitaki kuchukua muda sana, jambo la mwisho ni kuhusu mazingira. Tume imezungumzia kwa kirefu kuhusu mazingira. Kwangu mimi ningefikira kwamba, tungepiga hatua zaidi kuhusu sana sana na maji na mito, na mmomnyoko wa udongo. Je ikiwa tunazo sehemu ambazo zimetengwa kwa mfano kwa ujenzi wa barabara na katika barabara labda kuna futi kama hamsini hivi ambayo ni sehemu ya umma mito mikubwa mikubwa, kwa nini tusizitenge tuseme ya kwamba hakuna shamba la mtu yeyote yule ambalo litaguzwa mito mikubwa. Hiyo ni kwa sababu utakuta wengine wanalima mpaka karibu sana na mto na wakati labda kuna mvua kubwa, udongo wote unabebwa.

Kwa hivyo labda tunganisema mito mikubwa kama vile Tana, sehemu fulani kutoka ng'ambo hii na ng'ambo ile nyingine labda kuwena futi kama mia moja, shamba ambalo ni mali ya umma? Kwa njia ile, tutaweza kuhifadhi mazingira. Asante.

**Mercy Njoka:** Asante sana. Tunataka kumalizia hapo kwa sababu lazima tuende kwa sababu kesho tutakuwa Gichugu na ni lazima mipango ifanywe kabla... Ninaona kuna watu wawili ambao wananisihia kuwa waulize maswali. Nitawapatia nafasi lakini tafadhali muulize kwa njia ya kifupi sana.

**Joseph Kiriti:** Swali langu ni kuhusu separation of powers. Mwalimu alitambua iko hiyo separation of powers. Lakini niliporudi hapa ndani niliona iko pahali president anaenda tena kwa supreme court ati kwa sababu Act sijui imefanya nini huko parliament anaenda ku seek advice. Sasa hiyo separation iko kweli na iko independence hapo? Hakuna.

Hii ingine ni mambo ya pesa, pesa ya serikali. Hii borrowing hii hatuwezi ku-limit, we give a limit and we say it is a certain percentage as you said 0.3% in something. We limit the government to an extent of how much they can borrow.

The other one is, huyu mtu anaitwa Auditor General. If it is a Constitutional office, can't we give him prosecuting powers? Akihesabu hayo mambo yote, akiona Kinyeki ameiba, tomorrow Kinyeki anaenda kortini badala ya kuenda huko kumtafuta prosecutor na inakaa miaka mitano, au hata kumi.

The other one ni haya mambo ya shamba. Hawa watu wako na nine hundred and ninety nine years lease na mtu ako ulaya. We should repossess this land. Hao wengine wa ninety nine years na mtu halimi, they should pay a tax. Mtu anaacha shamba hivi, anaenda America, miaka ninety-nine, alipe kodi for not developing the land. Au inyakuliwe, you repossess it.

Ma commissioner, haya maneno ya wazee ku-retire into poverty na pension iko. Why don't we say we give them their pension within the first three months after retirement? Thank you very much.

**Mercy Njoka:** Thank you. The last speaker.

**Rev Maringa:** I am Maringa, Reverend Maringa and I don't want to speak much because much has been said. On the Bill of Rights, there is the section for the freedom of religion of Kenyans, that section. Presently our land has funny things that are happening including secret movements and there is a talk all over about devil worshipping and all that.

I feel for sure it is good that as we have the freedom of religion and opinion, it is good that we also have limits on what can be allowed on our land and especially where issues can be released and people be taken over where they will be having other powers other than the right powers to rule on us. I don't have much, thank you.

**Augusto Mwangi:** *Ni ngatho ngucokeria Commissioner na inyui ndimugeithie. Muriega. Nituaririe uhoro uyu wa miunda muno na notugukiaria tondu niguo ututuragia. Nii ngwariria aikari a icagi, maikarite miaka makiria ya mirongo iri na gutiri mundu uri werwo, we ni waheo tite. Riu ona angi maroiga tuku-developwo na ni Mkenya. Na tiri uyu uratuika ni witu na mundu nonginya a own mugunda Kenya niguo. Riu hau ri nihekwenda harorwo. Kai mundu agiire guikara handua tege na hatuike hake na ni wa Kenya. Hau hangi nguarua uhoro wa Commissioner uria wa borithi. Niahetwo miaka mingi muno miaka ikumi na nimui mathina maria makoretwo kuo na Ma Commissioner ma*



*borithi na waganu uria ukoretwo bururiini. Kwoguo ndagiriirwo ni gukiririo miaka itano. Tondur riu nigukionania President arithuragwo niundu athii term igiri magatuarana nake kinya akarikia. Kwoguo gutiri undu matangika bururiini. Thank you. Augustus Mwangi.*

### ***Clapping from the audience***

**Mercy Njoka:** Ameniruhusu nichukue maoni ya hawa wawili halafu tumalize kabisa. Nimekumbushwa kama unajambo na unaonelea ni jambo la muhimu sana, tafadhali andika kwa kikatataji, ukienda kwa wale wanaandika pale nje wanaweza kukupatia karatasi uandike na hilo jambo litaenda kusomwa na itakuwa tu sawa na kama vile ungekuwa umeongea, asanteni.

**James:** *Asante sana. Niwega ningucokeria Commission ino ngatho. Ritwa riakwa ni James. Maundu maria ingiaria mamwe ni mahutie no nii nguarie undu uria nyonire hau. Athuri marorwo. Angikorwo Bunge niiciragirira ikaheo pension yathii retire ri, athuri aria maheirwo retire, matiri mongererwo, moyaga two percent ri. Commission ino ndingiandika handu yuge andu acio mongererwo kamucara ta uria yongagirirwo me wiraini. Kana ni ta marua maria maheagwo andu a thirikari ati, 'your serive is no longer required. Riu hau nomuturirie hau. Kiu ni kia mbere. Gia keru ni house allowance iria tuaheagwo. Na riu ndikiri ndagikua na nduraga ndiri o wiraini tondu noheagwo mucara. House allowance icio, ndegaga kurihwo niki, na njikaraga nyumba na ni yakwa. Gatatu, hospital insurance, nindatinagio mbecha ciakwa na ndari member. Na riu riria ndabutirwo kuria ri, hospital insurance niyathirire. Hospital insurance ino githi tiyo yagiriire ni guteithia ciana ciakwa hindi ino. Kana ni migunda iria ihenagio andu Nairobi. Gura migunda haha, gura migunda haha. Kai migunda iyo iri yau tondu thirikari iri okuo na tutiri twaigua manyitite andu acio. Macokaga kuuga andu nimaraiywo mbecha. Kana ni uhoro wa cooperative. Cooperative niikuhota kwira andu marute mbecha magure nyumba ta ino. Yarikia gukinya hana, makoiga ongererai share na moigite ati itikwendio ringi share. Yarikia kugura share ikera mundu andike tumarua nigetha oige acokerio mbecha ciake. Nigetha andu acio mekuu, makue nyumba icio. No njurie Commission yandike hau yuge andu acio manyakuite nyumba icio cia cooperative mathitangwo ni thirikari maturihe. Uhoro wa migunda iyo notukuhutahutia kidogo tondu migunda guku Kirinyaga ni itureheire thina. Kuri migunda ina title inya na no migunda umwe. Ithatu. Riu hau mwarie, mutuandikire hau mutuire uria tuguika ni undu wa andu acio. Asante sana.*

**Mercy Njoka:** Okay, thank you.

**Munene Gakuiya:** *Nindamucokeria ngatho Commissioner niundu wa wira uria muraruta wira wina hinya na wira wa guthiururuka Kenya yothe. Nindacokeria Commissioner ngatho niundu wa wira uria mararuta wina hinya wa matuku maingi. Niundu wa guthiururuka Kenya yothe. Kwoguo handu haha hena uru muingi muno niundu wa ciana citu guthira ni murimu uria uretwo ukimwi na ndawa ina thirikari. Na thirikari ndingihota kuruta mbecha cia ndawa na mbecha cia harambee nimarona. Cia kuruta harambee nimarona, magathii magetharia na ciana ciitu igathira*

*makionaga. Uguo murore muno Commissioner tondu wira ucio ti mwega. Riu nigucokia bururi na thutha. Tondu ciana iria nyinyi ciakirikia guthira ri, bururi uguthii ku na ma. Nonginya Commissioner mugerie na hinya muno, thirikari irute mbeca iria marahuthira nyingi, nyingi, ciana icio itige kuruara ringi kana gukua. Na thibitari ciothe igairwo ndawa nyingi tondu ndawa irikuo ni mbeca ciayumbiirwo ni andu aya. Uguo ndawa niimenerere ciana cia Kenya tondu Kenya hingo iria twathiite kurua, korwo tuaiganaga uguo nitungiaruire muno nitungiahotanire na muthungu muno kumunyamaria muno. Kwoguo Kenya ni ndongu no ithinitio ni andu amwe niundu wa kwienda muno. Niundu wa kwienda muno, maheagwo mbeca nyingi gukira aria angi nao aria angi mature mahinyiriirio. Ta arui a mbara gutiri kindu ona kimwe monire, matigirwo uguo, no thina mariire wa kuethera Kenya wiyathi uyu na mbeca nyingi nyingi na gutiri undu ona umwe mateithirio nicio. Nimuetikania na uguo?*

**Audience:** *Ii.*

*Gutiri kindu mateithirio nikiu no kurua maruire. Twetirwo imaramari. Uguo Commissioner wikire undu ucio thiini wa watho tondu ithui gutiri undu tuonire na andu riu marathii o mundu na nituaheirwo wiyathi. Mundu akorwo ni mugeni wake nake, agoka akorio umurehete niki na ni Mukenya. Kai twaheirwo wiyathi uriku? Tukorwo ithui gutiri undu ona umwe tungiyonera na ni ithui tuethire wiyathi uyu. Ngukinyia hau.*

**Mercy Njoka:** Thank you very much. Riu nituguita mwarimu na nigetha aturikiririe, akorwo wina undu uroiga, angikorwo wina undu waku na niurenda kuandika, please andika na undu ucio niuguthii guthomwo na nitukurikaniria hamwe wega. Kwoguo Madam Gichangi welcome.

**Eunice Gichangi:** Asante sana, tumeendelea kurudia maswali na kupeana maoni ambayo ni ya muhimu sana na vile nilivyosema maoni yenu ni ya muhimu, tumeyachukua, tumeyaandika, na tunaendelea kuyaweka kwenye case pia.

Nitaanza na mzee John Wahome, aliuliza juu ya wale ambao wako na shamba kubwa na akasema pengine hata hiyo shamba sio yao waliuchukua kutoka kwa wengine. Bwana Wahome vile tumefanya, tumesema kwamba tumeunda Tume mbili, mmoja ni ya Lands Commission. Ukiwa pengine unatashwishi, kuwa shamba yako pengine imechukuliwa, unahaki ya kwenda kwa hiyo Tume na kupeleka shida ambayo umeipata. Pia kuna ile Tume ya haki yako, ya Human Rights, ambayo unaweza pia kuipelekea shida yako. Kwa hivyo hivyo ndivyo tumeona.

Kuhusu mambo ya pengine wale ambao wako na shamba kubwa au shamba ndogo, hatujaweka sealing ama maximum ya land ownership. Vile tumesema ni kwamba serikali lazima iendeleo na hapa ndio tunasema kila mwaka wanatoa repoti. Katika sehemu ya ardhi tumesema wanaendelea kuonyesha kile tunasema kwa Kiingereza equitable distribution of land. Yaani kila Mkenya ana haki ya kupata ardhi kama yule mwingine na serikali tumeipatia jukumu kwa sababu mambo ya ardhi ni magumu. Tunajua pia Tume ya Njonjo inaendelea na kazi lakini hatujaona yale mapendekezo kwa sababu hawajamaliza.

Lakini, tumesema serikali iendelee kuonyesha ya kwamba kila Mkenya amepata njia ama namna ya kupata ardhi. Hiyo kupata ardhi waendeleo kuisawazisha, ndio iwe ni equitable. Mimi nisiwe na acre elfu tano na wewe huna. Kwa hivyo, tumeipatia serikali hiyo juhudi na hilo jukumu la kuonyesha ya kwamba kila mwaka wanaendelea kubuni sheria ambazo zinatusaidia kuonyesha kila Mwanakenya amepata namna ya kupata ardhi, equitable distribution of land.

Mambo ya national days, hapo tulikuwa tumesema na mzee anaunga mkono. Pia akaunga mkono sehemu ya pesa kuwa isiwe na picha ya mtu yeyote. Mambo ya wanyama akasema kama ni mnyama ambaye amekufa, huyo mnyama huwa tunaulizwa tulipe pesa nyingi, kama ni binadamu pesa zile analipwa ni kidogo. Mzee vile tumefanya tumepeana mapendekezo. Kuna sheria ambayo kwa sasa ndio inasimamia mambo ya compensation. Ikiwa mtu, binadamu ameuwawa na mnyama pesa zile ambazo familia yake ama jamii yake italipwa. Tumependekeza kwenye repoti na hizo ndizo sheria ambazo tunasema zitaendelea kubadilishwa na bunge na wataendelea kubadilisha kupitia mapendekezo yetu.

Bwana Joseph Mwaniki amesema kuwa hatujatambua vyama vya opposition, vyama ambavyo havitashinda viti vingi bungeni. Kwa kweli pengine nilisahau, vile ambavyo tumefanya ni kwamba tumesema Prime Minister atatoka kwa chama kile kimepata viti vingi zaidi bungeni. Hicho chama tumekiita the majority party, kitatambulika kama majority party bungeni.

Kile chama ambacho ni namba ya pili, ambacho tunakiita the main opposition party bungeni, tumekipatia jina the minority party. Hicho ndicho chama ambacho kimepata viti vingi lakini hakijashinda kile cha majority, the second in place. Kwa hivyo hilo ndilo jina ambalo tumelitambua.

Mambo ya running mate, Bwana Mwaniki alisema ya kwamba sasa tukisema ya kwamba rais akiondoka mamlakani kwa sababu fulani, za kikatiba ama kisheria, tumesema makamu wake ndiye anachukua kiti hicho. Lakini tukisema hivyo, je hicho kiti cha makamu kitajazwa na nani? Katika article 156, tumesema ya kwamba makamu akichukua kiti cha urais ama kwa sababu yoyote kiti cha makamu kiwe kiko vacant, basi rais ni lazima atateuwa yule ambaye atachukua hicho kiti.

Akimteua, and that is mandatory, hilo jina analipikisha kwa bunge. Kwa sababu tumesema ya kwamba tukimchagua rais tunajua tumemchagua pia makamu. Sasa tumefika wakati ambapo kiti cha makamu kimekuwa vacant, kiti cha urais tumeshakijaza. Tumesema yule ameketi katika hicho kiti cha rais iwe ni yule rais ambaye tulikuwa tumemteuwa ama yule makamu ambaye amechukua hicho kiti, lazima ateuwe mtu mwingine ambaye atakuwa makamu na hilo jina alifikishe kwenye bunge ili bunge litoe idhini.

Mambo ya age ya MPs, anasema angependa kuwe na maximum age ambayo mtu anaweza kuwa mwanabunge. Proposal yake ni gani, sijui? Miaka mingapi, sabini? Seventy-five? Sawa hiyo ni proposal yake na tumeichukua ni ya muhimu.

Tena kuna mambo ya Constitutional offices, tume ambazo tumezibuni kikatiba ama afisi ambazo ni za kikatiba. Mtu ambaye atakuwa akifanya kazi katika hizo afisi amesema ya kwamba angependa huyo mtu ashikilie hiyo ofisi kwa miaka mitano na pengine akiongezea iwe ni mingine mitano. Ukiangalia article 281, sikuwa nimetaja, lakini hivyo ndivyo tumesema. Mtu ambaye ni Constitutional office holder, ofisi ya kikatiba ako kwenye hiyo ofisi kwa miaka mitano mara ya kwanza.

Hiyo miaka mitano ikiisha, ikionekana kwamba amefanya kazi vizuri inaweza kuongezwa tena aendelee kwa miaka mitano. Ikiisha wakati wake umeisha, na tunampatia mtu mwingine. Kwa hivyo there is a renewable tenure of five years. Hiyo ingine ilikuwa ni proposal kuhusu disability.

Bwana Kibuga aliongea juu ya kodi akauliza mbona watu kama rais hawalipi kodi kisheria? Kikatiba wanalipa kwa sababu wameajiriwa kama watu wengine mbunge wako analipa kodi, kila mtu analipa kodi kwa hivyo hata hao wanalipa kodi. Hivyo ndivyo sheria inasema.

Tena akauliza nyumba hivi za bunge kuwa zitakuwa zinatumia pesa nyingi, mbona tusikate hivyo viti viwe ni vichache? Vile ningesema ni hivi, kwamba sababu ya kuongeza hivyo viti ilikuwa ni sababu kubwa. Sio tu kuongeza viti, la. Ilikuwa kama ni ile nyumba ya pili nilisema ni kuangalia ile serikali ambayo imeanza kutoka kwa villages. Vile viti tisini tulisema ni vya kuangalia maneno ya vyama vya kisiasa viendelee kuwa vya kitaifa.

Lakini tukasema kuwa mishahara ya wabunge inaangaliwa na tume ambayo ni tofauti na hiyo tume inauwezo wa kuongeza, kupunguza na kadhalika. Kwa hivyo hiyo tume ndio tumeipatia uwezo ili iangalie kweli Wakenya wako na pesa ngapi za kuwalipa wanabunge. Na sasa tunawabunge kiasi fulani, sasa tugawane hiyo pesa ili kila mwanabunge awe akilipwa pesa kiasi fulani. Kwa hivyo hatuoni kwamba ama hatutaki eti Mwanakenya awe ati atalipa kodi zaidi, la! Tunataka tuongeze hivyo viti na mshahara wao uangaliwe na tume ambayo ni independent. Lakini proposal nimeichukua, ya Bwana Kibuga.

Tena akauliza mbona tutenge viti hivi vya kina mama? Nilikuwa nimeelezea hapo mbeleni kuwa ni mambo ya Affirmative Action, ni mambo ya kujaribu kurekebisha hizo sababu ambazo zimewafanya pengine kima mama wasiwe na haki sawa. Pia nimesema ni kwa muda mdogo, ni kwa wakati mdogo. Tukifika pahali tuone kwamba sasa haki zao ni sawa, basi hiyo inaondolewa. It is a temporary action, inaitwa Affirmative Action.

Bwana Charles Wachira aliongea mambo ya black ribbon hajauliza swali. Na hiyo tumeichukua, ni proposal yake amesema tubadilishe rangi tuvae ribbons ambazo ni nyeusi na sababu zake akazipeana, asante.

Bwana Dominic amefurahi kuwa mapendekezo yake yako kwenye Katiba, lakini akauliza mambo ya katiba yafundishwe kutko Darasa la kwanza hadi University. Bwana Dominic ukiiangalia repoti yetu tumesema kila Mwanakenya ana haki ya kuijua katiba kwa sababu tumempatia jukumu ailinde katiba.

Kwa hivyo tumependekeza katika repoti, ingawa hayawezi kuja kwa katiba ya kwamba ifundishwe kutoka primary mpaka mwisho, mambo ya katiba. Hata huyo mtoto wa Standard One awe akijua katiba, na awe anajua mambo ya taifa lake na katiba yake. Pia sisi wanatume ndio tumetoa example, mtindo kwa kusema ya kwamba tunataka tuwafunze Wanakenya ili wajue haki zao na waendeleo kuzijua haki zao.

**Note: Last tape missing. All work from this point is lifted from the Programme Officer's notes**

Pia anapendekeza kuwa umri wa mtu anayegombea kiti cha urais ipunguzwe kutoka ile miaka tumependekeza ya thelathini na mitano, iwe ishirini na moja na isizidi umri wa miaka sabini na mitano. Ningependa kusema hivi, kutoka kila constituency tumepata mapendekezo mengi, hata wengine walipendekeza kuwa umri uzidi sabini, wengine wakasema rais atawale mpaka wakati atakufa, yaani tusiwe na limit yoyote kwa miaka. Hayo yote ni maoni yenu na tumeyachukua chini. Tena ningependa kuwakumbusha ya kwamba hii ni draft tu, huenda baada ya National Conference umri ukabalika. Nimechukua maoni hayo na tutayaangalia.

Kuhusu nyumba mbili za bunge, unapendekeza kwamba representatives wasichaguliwe kutoka kwa districts kwa maana kuna districts ambazo zimekuwa created for political reasons. Kulingana na maoni yako unaona kwamba uchaguzi ukifanywa hivyo wengine watakuwa na mileage kuzidi wenzao. Unapendekeza kwamba district representatives ambao wataenda kwa Upper House wasichaaguliwe kulingana na districts bali iwe based on population. Hayo ni maoni yako, tumeyachukua na tutayaangalia.

Pia unapendekeza kwamba senior Public servants wawe selected kupitia advertised positions badala ya vile inafanyika sasa. Kuhusu jambo hilo tumependekeza katika hii draft section 183 kuwa Tume ya Huduma kwa Umma ndio itakuwa inashughulikia mambo hayo. Section 183 (1) inasema kwamba Tume hiyo ndio itashughulikia kuundwa au kuvunjilia mbali afisi yoyote ya umma. Section 183 (2) inaendelea kusema kuwa uwezo wa kuwateua watu wanaoshikilia na kuhudumu katika ofisi zilizoundwa kwa Jamhuri ya Kenya, kuidhinisha uteuzi na kutekeleza uwezo wa kuadhibu watu wanaoshikilia ofisi hizo, unawekwa katika Tume ya Huduma kwa Umma. Hayo ndiyo mapendekezo yaliyowekwa katika huu mswada. Lakini nimesikia maoni yako na pia hilo tutawasilisha ili lipate kujadiliwa katika National Conference kwa vile sio wewe tu uko na maoni kama hayo.

Joseph Thuita, asante sana kwa kupongeza Tume kwa kazi nzuri tumefanya na tunafurahia kwamba mmefurahishwa na kazi hiyo. Maoni yako ni kwamba malipo ya uzeeni yalipwe mara moja mtu anapostaafu badala ya vile inafanywa sasa. Tumeyasikia maoni yako na tutayaangalia.

Kuhusu masomo, Bwana Mbuchi anapendekeza kuwa Katiba iwashtaki wazazi wale ambao hawapeleki watoto wao shuleni.

Pia Katiba itaje mfumo wa elimu ambao tutafuata nchini mwetu yaani kama ni 8-4-4 au ule mfumo wa zamani. Ukiangalia section 58 katika huu mswada, inazungumzia mambo ya elimu inasema kwamba kila mtu ana haki ya kupata elimu hasa ya kimsingi na ya upili. Hiyo tayari inaonyesha kuwa wazazi wote bila shaka wanajukumu la kuwapatia watoto wao elimu. Bila shaka nimesikia maoni yako na hayo pia tutayawasilisha katika Tume ili tuweze kujadili zaidi na tuone hatia gani ambayo inatajikana kuchukuliwa kwa wazazi wasiwapeleka watoto wao shuleni na pia kama elimu itafanywa iwe ya bure na mfumo wa elimu tutakao tumia nchini.

Pia unapendekeza kwamba ungependa kuona serikali ikifutulia mbali pombe hizi za haramu. Kwa kweli mswada huu haujasema chochote kuhusu pombe za haramu. Lakini ukiangalia katika main report, tumeweka kwa Consumer rights kuwa mnunuzi ambaye ni wewe na mimi tuko na haki ya kusema kile tunataka tuuziwe na kudai haki zetu. Jambo hilo ninakuahidi kwamba tutalijadili na tuone vile tutafanya, lakini maoni yako nimeyachukua na tutayaangalia.

Bwana Kanyeki ameuliza kuhusu Auditor General, kwa nini asipewe prosecuting powers. Jambo hilo tumelisikia kutoka constituency zote ambazo tumetembelea na ninakuahidi ya kwamba ukisoma katika huu mswada utaona kuwa Auditor General amekuwa provided for functions ambazo atatekeleza. Lakini nimesikia swali lako na we shall give it further research to include your suggestion.

Mambo ya land, ningependa kusema kwamba it is a very sensitive issue. Tumesikia malalamiko ya aina hiyo kutoka kila sehemu pia. Ningependa kusema hivi, jambo hilo limeshughulikiwa vizuri sana katika huu mswada na pia vile nilisema hapo awali, Tume ya Njonjo bado haijawasilisha mapendekezo yao kwetu hivyo basi sitaweza kukupatia jibu kamili. Nimechukua hiyo observation na tutazidi kuiangalia pia.

Freedom of worship, mswada huu umeshughulikia jambo hilo kwa undani. Lakini ningependa kusema hivi, kila mmoja wetu ako na huru wa kuabudu chochote au yeyote apendaye. Mswada huu au sheria zetu haziwezi kulazimisha yeyote kuwa anafaa kuabudu kwa njia hii au ile ingine. Pia tunafaa tufahamu kuwa, na nilisema hivyo hapo mbeleni kuwa Kenya is a secular State, hatuna dini ya serikali hivyo kila mmoja ana uhuru wa kuabudu vile anapenda mradi tu asiingilie au kukatiza haki za wenzake. Reverend Maringa nimesikia concern yako na ninadhani umeridhika na hilo jibu, na pia asante for the observation.

Bwana Augusto anapendekeza Katiba ihakikishe kuwa kila mtu anahakikishiwa kupata kipande cha ardhi. Kwa jambo hilo ningependa kusema tutangojea maoni ya Tume ya Njonjo ili tuone mapendekezo yao ni vipi. Nimechukua hilo jambo na tutalifanyia further research, asante.

Kuhusu Commissioner of police, mswada huu unasema kuwa tutakuwa na Commissioner wa police na kuwa atateuliwa na rais kwa idhini ya bunge kwa kipindi cha muda wa miaka kumi. Tumeweka mapendekezo yetu kuhusu ofisi hiyo, lakini tutachukua hilo pendekezo lako na tuliwasilishe kwa Tume yetu na kwa National Conference for further debate.

